

Msimulizi, 1890¹

Edited and corrected by
Arvi Hurskainen
Department of World Cultures, Box 59
FIN-00014 University of Helsinki, Finland
arvi.hurskainen@helsinki.fi

Abstract

This is a corrected version of Msimulizi, the first periodical written and printed in Swahili language. The periodical was established to be an information channel between scattered mission stations of the Universities' Mission to Central Africa, and also between the supporters of the mission work in Great Britain. The periodical was originally scanned and made available by SOAS (School of Oriental and African Studies, London). Obvious scanning errors were corrected. Also, clear errors in original print text were corrected. However, nonstandard spelling was not corrected, if it was possible to assume that the writer intended to write in the way it was done.

The file follows the original pagination. A page in the original publication is a page in this file. Page numbering is continuous from year to year, and it is printed at the top of the page.

This file contains the text of year 1890.

MSIMULIZI. February, 1890. IX.
Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,
katika "Universities' Mission to Central Africa."

MIMI HAPA, MSIMULIZI!

Je! rafiki zangu, habari gani mwaka huu 1890. Ndio marra ya kwanza nimewafikia mwaka huu. Mkanitazame safari hii ginsi nilivyo, nimejaa maneno na maongezi hatta kujaa saaaana kwelikweli. Kwani

¹ The text is issued under licence CC BY-NC

pangine mambo yote ninayowasimulia yamo katika karasa zangu 16, leo nimekuwa mtu marudufu, kwani nimejaa hatta karasa 32. Sijui kama sikuzote nitanenepa kama hivi, nathani siyo, lakini, Bwana, nimekuwa na habari kubwa sana na njema sana kwa sisi watu weusi na tena nimekula siku kuu nyingi sana siku hizi ndio maana nimeshiba sana. Soma niyasimuliayo, utatambua maneno hayo.

Nafurahi sana kusikia kama katika miji mingi ya Upelekwa wetu kuna watu wengi wanitakao kuliko mwaka jana, haswa pande za Nyassa na za Wayao. Watu wa Magila na Misozwe hawajasema bado watu wangapi watakaonitaka, natumaini nao watazidi kuwa wengi, bassi safari hii nakwenda kwao na habari zangu kama kupiga safari za kubahatisha tu, kujaribu watakuwa wangapi watakaonikaribisha mwaka huu.

Lakini mnijie rafiki zangu mnaonikaribisha kwa furaha nataka niwaarifu kama kuna namna moja ya watu wasiomfaa Msimulizi mwenzenu hatta kidogo. Ndio wasionikaribisha wenyewe wakinisema, "Huyu Msimulizi ana gharama kubwa sana pesa sita kwa mwaka, naona choyo kutoa" kumbe, nikija zangu kuwasumulia ninyi mnaonitaka, wao husimamisha sikio kupeleleza habari zangu zote nizitoazo hujifurahisha nazo, lakini mimi hawanitaki hatta kidogo. Nao watendao hivyo, walio wengi hawako mbali nako ninakotoka. Labda ninyi mnipendao mtaweza kuwashawishi kunikubali. Ndipo nitazidi kusitawi. Msimulizi.

MSIMULIZI. 129

Huyu mwenzetu, Msimulizi asema mafumbo kidogo, lakini tafsiri yake ndio kama watu wengi wakikataa kutwaa Msimulizi kwa mwaka wakitamani kusoma Misimulizi ya wenzao pasipo kulipa, hawazidi kusitawisha shauri la Msimulizi lakini wanalithoofisha. Mtg.

KUAMRIWA KASISI WETU MWEUSI WA KWANZA.

"Siku hii ndiyo Yahuwa aliyoifanya; tupendezewe, tufurahi leo." Zab. CXVIII. 24.

January 22, Juma a tano ilikuwa Retreat mpaka Juma a mosi assubui kwa ajili yake Rev. C. Majaliwa. Sikuya Juma a mosi Jan. 25, Kuongoka Paolo, ndiyo siku Bwana Cecil alipopokezwa daraja ya Ukasisi. Assubui saa thenashara tuliondoka sisi kwenda Mkunazini, watoto na watu wazima wa Mbweni pia walikuja pamoja na Wazungu wao, na Makasisi wanne wa merikebuni pia walishuka siku hiyo. Bassi kengele zikalia, na watu wakajaa sana kanisani, na jumla ya Makasisi waliokuja ni wasita, wanne wa merikebuni, wawili wetu wenyewe Archdeacon Jones-Bateman na Mr. Dale, sala ya taratibu ya kuamuru Makasisi ikaanza saa kwanza, tukaanza kwa kuimba uimbo wa 191, tena Archdeacon Jones-Bateman akatoa khutubu akianza wosia huu utokao katika Zaburi, Siku hii ndiyo Yahuwa aliyoifanya, tupendezewe, tufurahi leo. Yakuwa imepita miaka thelathini tangu Mission yetu hii ya upande wa Mashariki wa Afrika, tangu Bishop Mackenzie hatta marehemu Bwana Bishop Steere, wote hawa na wengine wengi waliofariki waliikusudia waione siku hii, mbegu nyeusi ikilishana yenyewe na kuchungana kwa siri za Kanisa alizoziamuru Masiya mwenyewe, lakini wasidiriki, bassi siku yenyewe imeanza kuja Bwana aliyoifanya tupendezewe, tufurahi leo, na ndilo jambo la kukumbukwa sana hatta mwisho wa maisha yetu. Kiisha khutubu,

MSIMULIZI. 130

Bwana Askofu akasema sala na mawosia mengi, tena ikawa Litania, kiisha ikawa sala, nyaraka na Anjili na mangineyo. Baadaye akapokezwa daraja ya Ukasisi, kiisha ikaanza taratibu ya Usharika Mtakatifu, hatta mwisho tukatoka kanisani, tukapewa chakula chetu, kiisha tukarejea hapa Kiungani.

Alasiri saa saba u nussu watoto wote wa hapa Kiungani, wa Mkunazini na wa Mbweni tukaenda katika nyumba ya simu, kutazama mashindano ya mashua kule pwani, kwani kuna manowari kumi na 'nne za Waingreza bandarini hapa, hatta panapo saa kumi u nussu tukarudi.

Bassi katika siku hii kubwa ya Padre Rev. C. Majaliwa tulikuwa na siku mbili za kucheza tu ndizo Juma a tatu na Juma a nne. Jan. 26, Juma a pili killa mmoja wetu tukaenenda Mbweni assubui saa thenashara kwa Usharika Mtakatifu, na aliyeufanya si Bwana Askofu (kwani alikuwapo), illa ni Padre Cecil Majaliwa, ndio marra ya kwanza upande wetu wa Mashariki ya Afrika, siri hii Mbarikiwa kutolewa na mtu mweusi, bassi si furaha hiyo kuu tuliyonayo? Kiisha tukarudi zetu hapa. Jan. 27, Juma a tatu tulicheza sana, na Jan. 28, wote tulienda Mbweni kwa siku kuu, hatta jioni killa mtu akaenda kwake. Mtg.

HABARI ZA WARENO.

Bwana Askofu ametusumulia hivi habari ya safari yake kutoka Nyassa kuja pwani, na ya uthia wa Wareno pande za Zambesi.

"Labuda utapenda kusikia habari ya matendo ya Wareno pande za Nyassa, na tena kwa sababu gani merikebu nyingi za Waingereza zimekusanyika siku hizi huku Unguja. Mimi nilipokuwako Nyassa, twalisikia habari kama Mreno mkubwa, jina lake Serpa Pinto, anakuja njia ya mto Zambesi na asikari weusi wengi sana. Bassi barozi

MSIMULIZI. 131

Mwingereza wa Msumbiji alikuja Likoma, naye mtu aliyesafiri sana katika inchi nyingi za Afrika, akaja kwa mashua yetu ya moshi Charles Janson, Alipofika, alituambia ya kwamba ametumwa na Serkari ya ngereza kuja kupatana na majumbe wote upande wa magaribi wa Nyassa na wa mto Shire, kama wakitaka wenyewe kufanya urafiki na Waingreza. Tena akasema, yule Mreno Serpa Pinto amefanya kituo kando la mto Shire, karibu na mto Ruo. (Nao huo mto Ruo ndio siku zote umejuliwa kuwa mpaka wa milki ya Wareno. Nao majumbe wa ng'ambo ya Ruo ndio watu walioletwa huko zamani na Livingstone, wanaitwa Makololo. Livingstone akawaacha akaenda zake pwani, akakaa siku nyingi, akarudi, akakuta Wanyanja wa Shire wameendewa na Wayao vitani, Wanyanja wakachagua hao Makololo kuwa wakubwa wao. Bassi hao Makololo siku zote wamefanya urafiki na Waingereza kwa ajili ya Livingstone.) Bassi bwana Johnston akamwambia Serpa Pinto, Usiingie katika inchi ya Makololo na asikari zako wengi, kwani Makololo watasema unaleta vita, ndio itakuwa uthia mwingi na mashaka. Akathani Serpa Pinto amekubali kwenda Nyassa kwa njia nyingine wala si njia ya Makololo, akaja zake Likoma. Halafu akatoka Likoma, akaenda katika 'Charles Janson' upande wa magaribi wa Nyassa.

Alipokwisha kwenda zake, mimi nikafunga safari kwenda Unguja kwa njia ya mto Zambesi na watoto watatu wa Likoma pamoja nami, Yohanna Chanamila, na Tito Kung'ulukutu, na Mattiya Kangati, na bwana Janson akatusindikiza mashuani. Tukafika mtoni Shire, tukakuta vita iko, hatta Mponda aliye mtu mkubwa sana amekimbiza waanake na watoto wake wote kwa visiwa na kwa ng'ambo ya pili, kwa hofu ya vita, wakasalia mjini waume watupu wenyi selaha. Mponda akatuomba tusikae pale, kwani watu wake wamekasirika wote. Bassi tukaendelea tukafika

MSIMULIZI. 132

hatta mji pasipo watu illa wachache tu, tukalala, tukaamka tukaenda zetu mtoni. Tukawasili hatta Blantyre, marra nikasikia kama majumbe Makololo wote wamepewa bandera za Kiingereza, ndio dalili ya kuwa marafiki na watoto wa Waingereza. Lakini Serpa Pinto alikuwako kule kule, kwani fitina imetukia, watu wawili watatu wakajeruhi, mji mmoja wa Mlauri umeteketea. Ndipo yule Mreno amesema, nitawapiga Makololo, bandera moja ya Kiingereza ikang'olewa. Hatta akawapelekea Wazungu khati kusema, Ninyi nyote mkaao pande hizi, jitieni chini ya hamaya yangu. Msipojitia, labuda mtapata shari. Wasikubali Wazungu wa huko; wangelikubali, wangelikiri inchi hiyo ndiyo ya Wareno, lakini sivyo. Hakuna hatta Mreno huko, illa Wazungu walio rayia zake Mfalme wa Ingereza.

Palikuwa katika Blantyre bwana Buchanan, yule yule aliyekwenda kwa Makanjila zamani pamoja na bwana Johnson, naye rafiki wetu, naye ameagizwa na barozi Johnston kuwa mahali pake kitambo, mpaka arudi mwe hivi, Tulia kwanza, mpaka habari hizi ziwawasilie Serkali yenyewe. Bassi huyo bwana Buchanan akamshauri Mlauri ya Waingereza. Mlauri akamwambia, Mji wangu umeteketea, na watu wamejeruhi, nisipate msaada hatta kidogo. Tena bandera ya Kiingereza imeng'olewa na Wareno, Waingereza wasifanye neno lo lote. Labuda wamepatana na Wareno kutuharibu wote. Tusipojipigania mimi na watu wangu, tutaangamia na inchi yetu pia.

Na mimi nikaona khati hizo za Serpa Pinto. Najua hakika amesema, sifanyi vita mimi, natembea tu. Kumbe sasa ameandika kama Makololo ni chini ya Mfalme wa Wareno, wamemzuia asipite inchini mwao, bassi atawarudi. Na mimi nikataka sana kudiriki kwa meli ya Kilimeni, wala mashua ya African Lakes Company haijaja. Bassi

MSIMULIZI. 133

nikaingia mashuani mwingine nikaenda mtoni hatta Ruo. Tulipofika, watu wenyi mashua wakakataa kwenda mbele, nikawa sina buddi kurudi nyuma, marra mashua ya moshi ikaja, tukaingia. Nikaenda kwa mji wa Mlauri, nikamwomba atoe mtu wa kunisafirisha salamu mtoni, akasema, Siwezi. Naye na watu wake hawakututendea vema, kwani wakasema, Tumedanganywa na Waingereza.

Bassi nikarudi Blantyre, nikaenda Kilimeni kwa miguu njia nyingine. Lakini kabla ya kutoka, twalisikia kama Mlauri amepigana na Wareno, watu wake wengi wakauawa kwa bunduki za midomo mingi, (zile za kuguruta kama merikebuni.) Bassi wakajua haifai kupigana na Wareno, wasiposayidiwa na Waingereza.

Pale Kilimeni nikakutana na mtu Mfransa, aliyetoka pande za Kongo akawasili hatta Nyassa akaja Blantyre baada ya vita ile ya Mlauri na Wareno, akapata kupita njia ya mto Zambesi. Alipokipita, aliwaona Wareno wako ndani ya boma lao, akawauliza. Wataka kufanya nini tena? Wakasema, Sisi tutakula inchi yote pia mpaka Nyassa. Wakamwambia nakhotha ya mashua ya moshi, Tua bandera yako ya Kiingereza, hatukubali illa bandera ya Kireno tu mtoni mwote mwote.

Bassi Serkali ya Waingereza walipopata habari hizo, marra wakaamuru merikebu zikusanyike, maana yake hawakubali mambo hayo ya Wareno. Wallakini wanajaribu kwanza kuyatengeneza pasipo kufanya vita.

Charles Alan Smythies
Askofu.

HABARI ZA NYASSA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Hizi habari za kwanza ndio zitokazo kwa Augustine, ameniambia kidogo katika barua yake, bassi nami najaribu kukuambia.

MSIMULIZI. 134

Asema: - Mreno anazidi kufanya uthia huko chini, ameleta watu kumi na tano na zayidi, hapo pa Maendaenda &c, lakini wanakaa mahali pangine panaitwa Kuilyaza huko chini ndiko walikofikia, bassi wakaja hawa 15 mpaka kwa Maendaenda wataka pembe, walipofika Walikuwa hawana hatta chakula kwani huyo Mreno aliyewapeleka aliwaambia waende kwa rafiki yake Maendaenda, huyo atawapa chakula. Lakini walipoona kama hawapati hatta kidogo pembe ao chakula marra wakarudi zao Kuilyaza. Ndio habari.

Tena wanakaa kwa furaha kwa upande wao, naye Augustine amepata mwana mwanamke siku ya 15 ya mwezi wa July 1889 ndio habari zetu njema hizo.

Habari za safari ya Bwana Askofu, nimepata habari kwa Charles Sulemani na wangine: - Safari ikatoka Newala na panginepo, wakaja zao hatta mto mmoja, jina lake Lichiringo, watu watatu wakataka kufa, haswa huyo mmoja alichukuliwa na maji, akazamisha marra mbili tatu, tena alipojaribu kuogelea akafika ng'ambo ya pili lakini maji yamejaa sana tumboni mwake, lakini alikuwa mzima kwa rehema zake Muungu. Bassi wakatoka zao hapo wakaja mahali karibu na Mponda na hapo hapana hatta kituo tangu zamani watu wameacha kufika hapo, kwani pana hatari sana, lakini hawa wakafika wakajenga hapo, wakakoka moto hatta wakaisha yote, imekuwa usiku tulale tupumzike; marra akaja simba hatta kitwani kwa Charles Sulemani akanyemelea, akarukia kwenyi kitwa cha Charles Sulemani akatwaa chungu cha chuma akakitupa huko, kwani alithani kama ndio kitwa cha mtu, marra akarudi tena akaja kwa mtu mmoja wa Mbweni naye alikuwa akisali kitwa chini, alipoinuka akatazamana na yule simba hakufanya neno, akageuka akaenda zake kichakani, watu wasema kama alipotelewa akili zake ndio maana

MSIMULIZI. 135

akafanya hivyo. Sulemani na mtu mwingine karibu wangekufa, lakini kwa rehema Za Muungu wakaokoka wakafika hapa petu salama, lakani taabu wameiona katika njia, kwani alienda siku 16 pasipo chakula, mpaka bwana mkubwa akapiga nyama jina lake Ngozi huyo ndiye alikuwa chakula chao. Tena wakafika mahali penyi mji lakini wenyewe hapana wameisha hama kwa sababu ya vita, lakini wao wakakuta mtama, mhindi, na vyakula vingi, hivyo wakapata chakula, wakapata kufika hapa salama; ndio habari.

Je? mkuu wetu wa Msimulizi siku ya June 28 uliona nini kama saa 3.30 p.m. hatta labda saa 5.30 p.m.? Sio kupatwa kwa Jua (Eclipses of the Sun and Moon)? naona ndio, waonaje? giza huko lilikuwapo ao si sana? kwetu huku giza kubwa sana kama ndio usiku wa manane ginsi ilivyokuwa, ndio ajabu hiyo. Bassi mimi nikawauliza watoto wangu wa school, lakini hawakunipa maneno mengi, illa wakasema, ni vita kati ya jua na mwezi, bassi jua ndiye mwenyi nguvu sana, ndio maana kushinda. Lakini siku ya kupatwa mwezi, husema hivi, (haya ni mawazo ya wazee wanawaambia watoto wao) Tazameni leo siku mbaya sana kwani watu walio pwani hawakuwindia vema mwezi bassi ndio ndege ameumeza, sasa bassi tufanyeje leo? bassi wanatwaa majembe, mitungi wanavunja, majembe hugonga pamoja apate ndege kuacha katika kudonoa. Tena, pale assubui jua linapotokea husema kama wameungojea vizuri ndege huyo wala hakuweza kulidonoa: hivyo ndivyo wasemavyo, na pana mengine tena. Ndio upuuzi na upumbavu wa huku.

Habari hizi za sasa ndio za uthia tu, ridio wevi siku ya Ijumaa assubui yake kama saa kumi August 23, wakaja wevi wakaiba nguo zote za pa mathabahu hizi wakaiba wala hawakuacha kitu, msalaba, vinara, mapazia &c. vyote

MSIMULIZI. 136

vikaibiwa wala hawakuacha kitu cha mathabahu, ndio hasara yetu. Lakini panapo siku ya Sept, 2, 1889, msalaba wakaurudisha, lakini vitu vingine hatta sasa bado kuviona, ndio habari.

Panapo siku ya August 3 walibatizwa watoto na watu wazima na waanake wazima na watoto wa school pamoja kama arobaini, ilikuwa karamu kwa Wamasihya hao wanafunzi waliokuwapo hapo. Na wakatiwa mikono kama pamoja hamsini, majina ya waana waume wa school yetu waliobatizwa ni hawa:

Henry Filipo Shame, Barnaba Uledi, Richard Tomaso Mnyeta, Wm. Yona Kao, Danieli Wino, Arthur Chalunda, Kristofer Simion Mjeleka, Cyprian Msatila, Leonard Mattiya Kangati

Hapa ni majina ya watoto wa chuoni tu, siwezi kuandika majina ya wote kwani siyajui yote, ndizo habari zetu hizi. Panapo Aug. 18, 1889, bwana Alley ametiwa Msomaji (Reader), kazi yake ni sermala.

Naona kama umesikia kama pana mwivi huyu mkuu ndiye jina lake Kanje, siku moja akaja humu Likoma, bassi akaambiwa Archdeacon wetu ya kuwa Kanje yumo humu "Kumbuzi" si mbali sana kutoka hapa na huko kama nussu saa, bassi akapeleka watu kumkamata watu sita, sio washenzi illa ni sisi (Ch. Nasibu, Peter Selenge, Farijalla, Feruzi, Musa, Stefano,) hawa wakaenda wakamkuta nyumbani, marra mtwana alipoona kama wamemjia yeye akatoka ndani na visu viwili mkononi, akajaribu kumpiga mtu lakini kikafikia katika kifaru na yule mwenyi kifaru akamwandika nacho, kisu kikaanguka, mtwana yule alipoona ni watu wengi huyo, huyo, akakimbia, nao wakajaribu kumpiga kwa bastola lakini hazikumpata zikamkosa tu, nao wakaona kama hawampati wakarudi zao petu ndio

MSIMULIZI. 137

habari za Kanje huyu mtwana mbaya sana kwa wivi, yabis kabisa. Bassi sasa wengi wanafuata matendo yake ya wivi.

Sasa habari za petu hapa pa Mzungu karibu wote hatujambo, illa Dr. Hine ni mgonjwa marra kwa marra; bassi tumempeleka Bandawe anga ajaribu kupata nafuu na afya ya ugonjwa huo: kwani hewa ya hapa si nzuri sana kwa akina bwana hawa. Watoto wa kusoma wanakuja kama haiwaji kwa sababu wengine wakija hujaribu tu, na marra hutoroka zao. Lakini wengine wanajaribu sana kudumu katika kujifunza. Ndio habari zingine, mitambo ya mashua imefika, na bwana W. Williams amejaribu kutia mahali pake lakini bado hajaisha. Akina bibi kwa kadri yao hawajambo, lakini wana uthaifu kidogo. Bwana Askofu yupo hapa hatta leo hivi Sep. 16, lakini punde hayupo tena, na labda atakuja na watoto wawili ao watatu wa huku Kunyanja: lakini Bwana Askofu hakupata afya sana huku Kunyanja sijui sababu gani, hatta naona mimi ni vema baba yetu apite njia ya bahari, anga apate nafuu kidogo. Hizo, ndizo habari zetu sisi.

Siku ya Sept. 14th, amefika Balyozi yule yule aliyekwenda kutengeneza upande wa Kilimanjaro, sasa amekuja huku 'Consul JThnsto' na Mzungu mmoja na watu wa huko pande za Unguja na yule Shongwi wa Mkunazini: bassi huyu Balyozi amekuja huku kwenda huko na huko na kutengeneza inchi hii kwani haina amani wala haina furaha, ni uthia tu siku zote. Bassi ataazima steamer yetu O. Janson aende nayo, huko upande wa kaskazini akaangalie habari zake na kutengeneza. Bassi yupo hapa anapita njia tu: na kufanya kazi yake,

Siku ya Ijumaa twasafirisha ndugu zetu ndio Yohana Chauamila, Tito Kungurukutu, Leonard Mattiya Kangati,

MSIMULIZI 138

ni Watoto wa huku Nyanja pamoja na Bwana Askofu na Peter Selenge.

Hii habari ni ya huku nami nataka kukuambia ginsi naswi tulivyokuwa na kulia tu, na Bwana Askofu ni kulia na huzuni tu kwani mwenyewe alituhubiria kama hajamwona mtu kama Padre Bwana Goodyear. Bassi na mimi nakuandikia maneno haya kama ukipenda kuyapiga chapa ni vema sana.

MACHOZI YETU KWA BWANA GOODYEAR.

(Shairi); 1. Huzuni sana kwa Bwana Mwaka Mwema, Aliyekuwa Padre Mwingreza mzuri na mwema; Kwa watu na kwa killa kitu; Asiyefanya kazi yake kwa kitu; Illa yote ni kwa busara na heshima, Pamoja na bidii, wala si kusifiwa.

2. Padre aliyependwa na watu wote sana, Watu wa karibu na mbali sana; Na wote wakamwona Yee ni wa bidii sana, Ni Padre wa kweli wa Yule aliye juu, Apendezaye sana chini na juu, Asiyefanya thulumu kwa mkubwa wala kwa mdogo. sana.

3. Bassi je? kwetu sisi aliyetuchunga? Hatuna huzuni, wala kulia, kwa wema ule wa kutuchunga? Wala hatuna namna yake ya kumfuata? Kwani Yee ni wa kutazamiwa na kufuatwa, Si kwa kutuchunga tu wala si kwa ajili ya wema; Illa kwa maisha yake, yenyi kujaa dini na kujua kuomba vema.

4. Bassi tuombe siku zote Mwenyi yote atujalie siku zote njia tuone.

MSIMULIZI. 139

Tupate kufuata maisha ya imani na yenyi kweli, kusudi tupone; Si kupona kwa inchi wala kwa mwili; Illa kwa roho, na pamoja na mwili; Siku yetu ya kulala ikifika, tulale kama yee kwa amani, Wala si kwa kuogofya na isiyo na kweli wala imani ya kutumaini.

5. Sasa sifa iwe kwa Yee wa kutupa na kutuondolea, Kwani vyote ni vyake na vyatoka kwake na apendavyo hutuondolea, Aviondoa katika dunia hii ya taabu na huzuni, Apata kuvistarehesha pale penyi raha, amani, wala si huzuni; Asema mwenyewe, Njoooni kwangu wenyi mizigo na kulemewa nami nitawapumzisha. Bassi haya twendeni wote tuonane naye kwa furaha wala si kwa kumhuzunisha.

W.E.K.

Likoma, Nyassa.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Baada ya salaam, naona safari hii sina mengi ya kukuambia. Illa nitajaribu tu, kwa kadri niwezavyo.

Kunako Sept. 14, Consul H. H. Johnston amefika pamoja na watu wake na karani wake mmoja (Mzungu). Bassi akapata kuonana na Bwana Askofu, kwani Askofu hakuacha Nyassa illa kunako Sept 19 naye amekwenda na watoto watatu wa huku Nyassa, Balyozi kaenda Bandawe na miji mingine ya huko. Bassi 'Steamer' iliporudi ndipo ikampeleka Bwana Askofu pande za chini huko, na sasa leo hivi Oct. 10 'Steamer' yaenda Bandawe kumtwaa huyo Balyozi, ilitoka Juma a tatu hatta leo Alhamisi bado kurudi. Tunangojea tu, labda ikija nta kuwa na habari za kujaza karatasi.

MSIMULIZI. 140

Lakini haya twende mbele sasa. Chapa yetu ya hapa Likoma inaendelea kidogo kidogo, naona tukipata fundi tutakuwa naswi na vitabu vyetu. 'Gharlotte' mashua yetu sasa ni 'steam boat', imeanza kwenda kwa moto kunako Sept. 28, tangu siku hiyo hatta leo hivi imefika huko na huko, Bandawe, Chisumulu, pa Kungo, &c. Kwani wakati usio na pepo sasa ndio sababu kutia moto.

Kunako Oct. 6, wamefanywa Waanafunzi watu sitashara wa kazi watupu. Na panapo Juma a pili Oct. 13, naona watatiwa waanafunzi waana chuoni, waume na wake.

Naona itakuwa huzuni sana kwetu ya kuwa mganga wetu Bwana Hine anakwenda zake Ulaya, kwani huku hakumpendi, labda hapo Unguja patamfaa, labda atajaribu kukaa kwa kitambo kidogo.

Siku ya Juma a pili wametiwa waanafunzi 13 watoto wa Chuoni wote. Na katika siku hiyo hiyo Juma a pili usiku wakaja usiku wevi watatu, lakini marra tukawaona tukawafukuza, hawakuja tena hatta leo Juma a mosi bado. Siku ya Juma a tatu 'Steamer' ilishika safari ya kwenda kaskazini pamoja na Archdeacon, kwanza ikaenda Bandawe kwa kutaka kuni, marra ikashika njia ya Kumagomero, hatta leo Juma a mosi Oct. 19 ipo hapa, lakini Balyozi hawakuja naye, yuko kuko huko.

Habari za huko ni njema, illa nasikia kama ndui ndio nyingi huko Kumpoto hatta watu wanakimbilia mwituni. Na habari zingine za vita ile ya Kopa Kopa naona hapana habari nyingi illa Wazungu wamepata kushinda marra kwa marra; na habari zingine ndio 'Steamer' yetu imerudi, bassi imekuja na Wazungu wanne, watatu watoka hapa Bandawe, na huyu mmoja ndio kwanza atokea kutoka pande za Ulaya, Bassi yee ajitembea toka Senegal kwa miguu na mitumbwi kwenda siku zote, walikuwa wawili lakini, bwana, kama ujuavyo inchi yetu hapana amani, bassi ameuawa na washenzi

MSIMULIZI 141

kati ya Lake Tanganyika na hili letu Lake Nyassa. Bassi yee peke yake tu amefika pamoja na watu wake wawili tu kwani wajua uthia wa Afrika, watu wasiomjua Muungu bado hawa. Bassi yee peke yake amesalia anarudi kwake naona atapita hapo Unguja, sijui vema lakini. Habari zingine, watu wa pande za Bandawe wana shauko sana kwa kujua kusoma hatta wazee pia wataka, bassi sasa wana watu wengi sana waana chuoni. Sijui kwa sababu ya Wazungu wao walifika tangu kale, na sisi ndio kwanza tuanze, labda baadaye watakuwapo watu watakao kusoma.

Ndugu zetu wafundishao pwani pwani ya bahari hii bado kusikia vema habari zao, lakini tunatumaini kama hawajambo na wanafanya kazi yao vile vile; wanaye bwana Johnson pamoja siku zote hizi, kwani yee ni mtu asiyeacha kitu chake hatta kwa dakika moja pa peke yake; bassi yee yupo pamoja nao siku hizi zote. Barua zenu bado kupata, naona meli ikirudi italeti, yule Balyozi yuko huko pande za Bandawe anafanya kazi yake ya kupatanisha watu weusi na Waingereza na wafanyao kazi yetu ya Upelekwa.

Kesho Juma a tatu Oct. 21 twamsafirisha Kasisi na Daktari wetu Hine, pamoja na Wazungu wangine waendao paride za huko chini. Na Mr W. Williams atampelekeza mpaka Blantyre, tena yee arudi. Salaam wote watendao kazi hii ya Bwana. Wasalaam.

Tumepata habari nyingi zilizotoka kwa Paul Wickham Mambo kama waliibiwa sana huko, lakini habari yenyewe sasa imekuwa ya kale, imepita miezi minane, na tena safari hii Msumulizi umejaa, bassi awe rathi sana. Tuna tumaini kama sasa vitu vyenyewe vimeisha kupatikana. Mtg.

HABARI ZA CHISUMULU.

Oct.26, 1889.

Na sasa kazi yetu inianza kusitawi, watu wanakuja killa

MSIMULIZI. 142

Juma a pili na Bwana Williams anahubiri, akiisha anasimama mtu wa humu anauliza. Na sisi hapa, tunakaa vizuri sana, lakini watu wenyewe kama mnavyojua mambo ya kishenzi si mema na sisi Wamasihya watu watano tu bassi. Lakini najua kwa rehema yake Mwenyiezi Muungu hawana buddi kugeuka, na desturi yao ni kama katika Efeso wakati ule Paolo Mtume alipokwenda kwa siku ile ya kwanza kwa maabudu yao, najua katika Efeso waliacha, vivyo na hapa wataacha kwa rehema yake Mwenyiezi Muungu, na kumwabudu yeye Muungu wa kweli. Lakini kisiwa chenyewe kinatufaa kwa afya sisi wote na Bwana Williams pia, na Bwana Archdeacon Maples anakuja hapa petu killa Juma tano kwa kungoja Alhamisi kwa Usharika Mtakatifu Bwana Williams na sisi. August 2 Bwana Askofu akaja hapa petu, akalala, aththuuri wakatoka na mpishi Luka Sajiwandani na mkewe kwenda kubatizwa, hapa akakaa Charles Sulemani kumpikia Bwana Williams mahali pa L. Sajiwandani, wakabatizwa wakarudi. August 17 wakaitwa tena kwa kutiwa mikono, hapa wakatoka watu watatu mpishi na waanake wawili. Mimi nikaenda nao tu, hapa akakaa Bwana Williams na Mwalimu Denys Sayite alitoka Likoma kuja hapa mahali pa mimi, na Peter Selenge alikuwa akimpikia Bwana sababu Charles Selemani alikwenda zake, yeye akatangulia, Bwana Askofu akamwacha huku Nyassa. Bassi sisi tukatoka hapa kwenda Likoma August 17, tukalala siku nane. Juma a pili August 25, wakatiwa mikono wenzetu watu 60. Bassi siku yetu ya kurudi ikawa Juma a tatu alasili tukaenda pwani tukapakia vitu vyetu, tukarudi kwani hatukupata pepo. Mimi nikashika kazi yangu ya kufundisha na Mwalimu W. E.Kapyopolea, kwani Mwalimu Denys ndiye aliyekwenda Chizumulu mahali pangu. Assubui saa ya kwanza tukaagana na ndugu zetu, tukaja zetu hapa, Mwalimu Denys na Peter Selenge wakarudi Likoma.

MSIMULIZI. 143

Sep. 24 Archdeacon Maples akaja hapa kututwaa kwa arusi ya Musa Kalulu, baada ya kutoka Askofu, tukaenda katika mashua Juma a nne Sep. 24, Alhamisi Sep. 29 ikawa arusi, wakaozwa vizuri, W.E.K. na mimi tukawa rafikize Musa Kalulu, wakaisha, wakafanyiwa karamu mezani, sisi Waalimu wote watatu tukaitwa, tukaenda kula tukatoka. Archdn. Maples akatuambia, kesho Jumaa ndio safari yenu afathali jioni mkalale pwani kwa kungoja upepo, sisi tukaenda na Mr Williams wa pili, assubui tukaja zetu hapa.

HABARI ZA MLOLELA AO CHITANGALI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Siku kuu hii ya Uzaliwa hatukupata kustarehe kwani ulikuwa uthia haswa vita kati ya sisi na Maniamba.

Alitoka mtu wa Maniamba akaja hapa pa mzee Barnaba Nakaam; huko kwake amefanya kama kutoroka. Na Maniamba akapeleka watu wake kuja kumtaka mtu wao, na wale watu hawakumwendea Mzee Nakaam wakaenda hatta mji wake mmoja wakakamata watu wawili. Naye Mzee Nakaam alipopata habari akanena, ah! wamenitharau sana, kwa nini hawakuja kuniambia kama wanataka mtu wao kwani ni desturi kumwendea kwanza Mfalme wa mji. Bassi akapiga ngoma yake ya vita wakaja watu wake wote, akawaambia, nendeni hatta kwa huyo Maniamba mkakamate watu wake mwaleta hapa. Wakaenda majeshi matatu, wakarudi wamekamata watu 4 na jeshi hilo lililokamata ni la mwanawe mmoja anaitwa Daudi Chiwilime. Na assubui tukasikia kama mtu mmoja wa kwetu amekamatwa, akawaita tena watu wake akawapeleka kama kwanza, na safari hii jeshi lililokamata ni la mtu wake mgine anaitwa Isaak Asasu, akakamata watu 5. Na yule Maniamba alipoona kama vita itaendelea, akajaribu kuwalalika watu wangine nao wakakataa, wakasema, "Kama B. Nakaam

MSIMULIZI. 144

angekuja kutulalika tukupige wewe tungekubali kwani yeye ana asikari wengi na tukienda tutakwenda kufa burre" bassi akajaribu kukopa baruti kwa watu wakakataa. Bassi akapeleka mjumbe kuja kumwambia B. Nakaam anyamaze asifanye vita illa turudishiane wafungwa.

Na wakati huo ndio karibu na Uzaliwa naona Dec. 24, na wafungwa wakarudishwa. Na Wamasihiya na Waanafunzi walio waume walienda Newala kwani waliitwa huko na Rev. W. C. Porter. Na Mr. J. Hainsworth pia akaenda nao.

Na hapa nyuma Wamasihiya na Waanafunzi walio wanaake wakachinjiwa mbuzi wakapewa na mchele.

Watoto wote wa hapa walikwenda Newala na Mr. J. Hainsworth pia illa mtoto mmoja aliyekuwa hawezi kidonda akabaki pamoja na Mwalimu. M.H.

HABARI ZA MAGILA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaamu. Siku ya ashirini na sita ya mwezi wa December akatumwa mwalimu Lawrence Kombo, pamoja na watu wawili wa mfalme Mdami, kumpa mfalme habari kama Wazungu wanakuja; akatoka mwalimu siku ya Alhamisi baada ya siku kuu ya Kuzaliwa Bwana wetu.

Hatta katika Jumaa na Juma a mosi zikawa siku za kufunga vitu tayari kwa safari. Hatta Juma a pili wakatafutwa wapagazi wanane wakaambiwa kuja pale-pale Mission kwani safari itaondoka mapema sana siku ya Juma a tatu. Bassi Juma a tatu assubui mapema kama saa kumi na moja, watu wakaamka wakaanza kujifanya tayari, Wazungu wakala kidogo, hatta saa kumi na mbili tukatoka Magila watu kumi na tano: Dr. Castle, Mr. Wilde, Hugh Peter Kayamba, Leonard Pesa, Herbert Martin Feruzi, Nicholas Kanu, na wapagazi 8. Ndio siku ya Dec. 30,

145 MSIMULIZI.

Tukaenda kadri ya saa moja Mr. Wilde akapiga ndege mzuri sana kama tausi kwa umbo lake, lakini yeye mdogo tukamchukua; tukaendelea mwendo wa nussu saa Dr. Castle akampiga ndege mwingine tukamchukua. Tukaenda hatta ikatimia athuuri tukatua penyi mto Kihulwi kupumzika pale hatta saa nane, kwani Wazungu hawawezi kwenda na jua kali. Tukapewa posho yetu killa mtu pesa sita kununua chakula, lakini hapana kitu cha kununua illa kwa bahati akapita mtu na mkewe wamechukua ndizi mbichi na mihindi mibichi, tukanunua tukachoma. Ni desturi ya Wabondei marra nyingi wakisafiri mahali pa mbali hawakosi kuchukua ugali wa baridi, nao hauharibiki hatta muda wa siku mbili ao tatu. Bassi katika safari yetu ulichukuliwa ugali mwingi, tukala pale tulipotua mchana, nussu ukachukuliwa tena. Bassi tukashinda pale mtoni na mto hauna maji yamekauka, nayo yaliyosalia si mengi kidogo tu nayo si safi, lakini tufanyeje ikatupasa kunywa maji yale mabaya kwa kiu na jua kali.

Hatta saa nane tukaondoka; pale-pale kabla hatujaondoka tukampata mtu wa kutuongoza mpaka Zavuza kwa rupia. Bassi tulipoondoka tukaenda hatta tukaupata mji, marra tukaingia mjini kunywa togwa, tukatoka tukaenda hatta tukafika penyi mji uitwao Potwe ndio mwanzo wa kusema Kizigua kitupu wala hapana kuamkia Kibondei tena. Tukajenga hema pale tukanunua ugali pale tukala, jumbe wa mji ule akatoa kuku akawapa Wazungu. Hatta assubui mbele ya kuondoka akapewa kipande cha nguo. Tukashika njia tukapita pahali paitwapo Nkele ya mahondo ndipo mahali kati ya milima miwili, ukiwa pale juu utaona inchi ya Wazigua yote inchi sawa kwani katika Uzigua hapana milima iliyo mikubwa, tukapumzika pale pale juu kati ya milima napo mwitu mkubwa sana pale. Tukashuka mlima, tukaenda hatta tukafika penyi mji wa Malomo, jumbe wa Kizugua, mtu yule mrefu, na mnene, mwekundu,

MSIMULIZI 146

ndiye babaye yule kiongozi wetu, tukatua pale tukashinda hatta saa nane, Wazungu wakawaonyesha bunduki za kubandua na bunduki ya Dr. Castle yenyi mishindo minane wakaistaajabia sana. Tukaondoka pale tukaenda na killa mtu mwenyi chupa yake akajaza maji tayari Tukaingia katika nyika yenyi miti, mwisho tukatokea nyika isiyo na miti hatta kidogo waweza kumwona mtu hatta akiwa mayili moja ao zayidi.

Tukaendelea hatta mto Luvu ikaonekana na njia ya Pangani wafuatayo wakienda Masai tukaifuata njia ile kubwa hatta mto Lwengela, mto wenyi hatari sana wakati wa masika, maji mengi sana na mamba wengi hatta ni shidda kuuvuka wakati huo wa mvua. Lakini tulipopita maji haba sana yanafika magotini tu, hatukukaa sana tukaondoka tukaenda hatta mji wa Kwamngumi ukaonekana. Lakini kitambo kidogo kwani ni inchi sawa, bassi kwa macho ni karibu kwa mwendo ni mbali, tukawaona ndege wanakwenda kundi pamoja wakubwa, Wazungu wakajaribu kuwapiga lakini hawakuweza kwani ni mbali nao hawawezi kuwaendea karibu kwa kuwa peupe kabisa majani madogo kama yale ya Mnazi Mmoja. Tukafika mji ule wa Kwamngumi, nao mji mkubwa katika kisiwa cha mto Luvu una ng'ombe nyingi na ngome yao ni maji, kupita kwa daraja. Na daraja lao namna hii: Wametia miti mikubwa iliyo imara ng'ambo hii na ile wakatia mbao hodari sana sana mwanzo huu na upande wa pili, katikati wakatia ubao mwepesi sana mtu akipita unatikisika kama utavunjika, lakini wenyewe wamezoea sana hatta wanawake wanapita na mizigo ya kuni na watoto wanakimbia juu yake. Hatukulala pale tukapita tukaendelea kidogo tukaona mji wa pili katika kisiwa cha mto Luvu, mkubwa sana mji ule, ndipo anapokaa mamaye Wilfred Madudu, mji ule unaitwa Nkologwe ndipo alipojenga Mdachi zamani, tukaona masalio ya nyumba yake. Tukapita tukaendelea hatta

MSIMULIZI. 147

Zavuza tukatua, yule kiongozi akapewa rupia yake akaenda zake, ilikuwa saa kumi na mbili jioni tukajenga hema pale, wangine wakajaribu kuvuka daraja lile waende mjini wangine hawakuweza kwani hawajazoea nao ni usiku, ndio siku ya December 31. Juma a nne January 1, Juma a tano hatukusafiri tukashinda pale pale Zavuza; hatta alasiri tukavuka upande wa pili wa mto kupita katikati ya miji, tukajenga hema kule; tukanunua ugali na killa kitu tutakacho kwa safari yetu, tukania kutoka alfajiri kabisa hatta usiku kama saa nne mpagazi mmoja akawa hawezi sana akapewa dawa hatta assubui akafuata pasipo mzigo. Tukawa naye mtu mmoja wa mfalme akatungoja pale Zavuza tukaenda hatta karibu saa 4 ao 5 tukafika penyi mji uitwao Kinamo tukatua, watu wa mji ule wakatuuzia vitu ghali sana hatta mtangi wa maji pesa kumi, tukakaa pale hatta saa 10 jioni tukaondoka tukaenda hatta kati ya usiku tukalala kidogo, tukaamka tukaenda tukafika mahali tukatua tukalala, hatta assubui tukaondoka tukaenda hatta kama saa 3 tukafika kwa mfalme tukapiga bunduki nyingi, ikajengwa hema akaja mfalme kuwaamkia Wazungu, akatoa ng'ombe kwa kitoweo chetu tukamchinja, mfalme yule malidadi sana, ana upanga na ala yake ya fetha, amevaa kanzu kubwa ndefu ya kazi kwani ni mtu mrefu sana ndio siku ya Jumaa Jan. 3, Juma a mosi na Juma a pili tukawa naye pale akatoa mwanawe mdogo akafundishwe Magila.

Tukaondoka Juma a tatu assubui Jan. 6, tukaenda hatta tukafika penyi mji, wenyewe wakataka kufanya vita nasi kwani hawampendi yule mfalme tuliyemwendea adui yao, tukawabembeleza tukapita tukafika mji uitwao Mbibu tukalala hatta assubui mzee wa mji akaja akawataka Wazungu wamfanyie dawa katika kisima chake maji yasikauke, tukamwambia haiwezekani. Tukaondoka tukafika mji ule ule Kinamo tukanunua maji mtungi pesa 9, tukaondoka alasiri tukafika Zavuza, tukavuka mto,

MSIMULIZI. 148

tukapita mjini tukavuka ng'ambo ya pili ya mji tukajenga hema ndio Juma a nne Jan. 7 Juma a tano hatukusafiri illa tukaondoka Zavuza kwenda kwa miguu mwendo wa saa moja tukajenga hema pale, hatta saa nne ya usiku Mr. Wilde alilala alipoamka akaona saa 4 akathani saa 10 assubui, akatuamsha tukaangusha hema tukafunga, na balamwezi inawaka tukaona duka tukaenda tukapita mto Lwengela hatta njiani kabisa akaangalia saa akaona inakwenda saa 6, hatukupendezewa sana lakini tufanyeje? hapana mji karibu, tukaenda hatta tukafika kwa Malemo saa 7, tukalala hatta assubui tukaenda tukapanda kilima kile Nkele ya mahondo, tukashuka Potwe tukanunua miwa tukaondoka hatukutua wahadi mto Kihulwi, hatta saa nane tukaenda hapana kusimama hatta kidogo tukafika Magila saa kumi u nussu. Lakini Hugh P. Kayamba na Lawrence Kombo tumewaacha kule kwa mfalme Mdami kwa maneno. Tena Jan. 5 Wakabatizwa watu, 14 wawili wao watoto wa Mission. Juma a tano Jan. 15 wakatiwa mikono pamoja na wangine waliobatizwa zamani. Ile ile Juma a tano saa 9 Bwana Askofu akatoka Magila kwenda Unguja pamoja na Rupert Mwarabu na mkewe, Andrew Yakuti, James Ramathani, Richard Kambaku, Antonio Mjsimile, Ackworth Baruti, Mattayo Dafa na Robert Feruzi na Samuel Sehoza. Watoto wengi wangine walioingia Missioin.

Siku kuu ya Kuzaliwa ilikuwa karamu kwa watoto wengi wajao kusoma waume na wake.

Siku kuu ya Kuzaliwa, tukapamba siku ya Juma a nne hatta Juma a tano siku ya siku kuu yenyewe, assubui ukawa Usharika Mtakatifu, watu wengi walishariki, tulikaa sana kanisani tangu saa ya kwanza hatta saa ya tatu kassa robo, tena tukaingia kwa sala ya pili ndiyo ya waanafunzi na watu wote, kanisa likajaa yetu kabisa, Bwana Askofu

MSIMULIZI. 149

akahubiri kwa Kiingereza mwalimu Ackworth Machaku akafasiri kwa Kibondei.

Mr. Woodward hakuwapo alikwenda kufanya siku kuu Mkuzi na kuwalisha ndugu zetu Chakula cha roho, tena akapita Umba na mwisho akarudi Misozwe akaja Magila tena. Siku ya Alhamisi baada ya siku kuu ya Kuzaliwa watoto wote wakapewa ruksa ya kwenda killa mtu kwao kuwatazama jamaa zao tangu Dec. 26 hatta Jan. 4 wakarudi wote lakini wangine walijiongezea siku. School ya watoto wanaake inaendelea sana hatta wangine wao wamebatizwa siku kuu hii ya Kuzaliwa. Mr. Allen na Bibi Smith wamefika salama Magila wote hawajambo. Mr. Allen amekwenda kukaa Mkuzi. Mwalimu Richard Mhina amepata mtoto mke, jamaa zake wakafanya uthia sana wakitaka kumwua mtoto kwa sababu babaye hakuvingia Galo (ndio mchezo mbaya wa Kibondei) lakini hawakuweza.

Mbele ya siku kuu ya Kuzaliwa watoto walitazamiwa kusoma na Mr. Mercer pamoja na Mr. Woodward, aliyeshinda kwa killa kazi ndiye Basil Mhada na wa pili akafuatana naye kwa killa kazi ndiye Richard Kambaku. Mr. Roberts aliugua mbele ya Christmas na Mr. Wilde na Mr. Wride lakini sasa hawajambo. Kisima kinajengwa Magila karibu kwisha. Bibi Townshend akaugua sana hatta Dr. akamwamuru aondoke. Alipoondoka Sisters wote wakawa wagonjwa pia lakini sasa hawajambo.

HABARI ZA MKUZI

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Na baada ya salamu nakuarifu kama Dec. 13 tumesikia habari ya kufa kwake Mwarabu yule aliyewauthi sana Madachi, jina lake Bushiri, naye ameuawa hivi. Huko alikokimbia akajificha ndani ya paango la jiwe huko Zigua, bassi marra akikimbizwa

MSIMULIZI. 150

huku na yeye huenda huko paangoni hujificha. Bassi Major Wissmann akawaambia Wazigua wafanye shauri hatta wamkamate. Bassi Bushiri alikwenda huko paangoni akajificha kumwogopa Mdachi, na Wazigua wakamwendea kwa urafiki wakamwambia, wewe umekuja katika inchi yetu nawe umemkimbia Mdachi. Bassi utaacha hatta sisi Mdachi atatupiga, bassi twende mjini tukafanye urafiki (tikasogane) ndio kuahidiana kama hatutaachana. Bushiri akasema, Haya twendeni, wakaenda hatta wakafika mjini, wakafanya karamu wakachinja kuku mbili, marra pale wale Wazigua wakatazamana, wakaondoka ghafula wakamshika Bushiri wakamfunga. Major Wissmann akaenda kuitwa, marra hiyo alikuja na frasi wake hapo, akauliza, Yuko wapi? wakamwambia huyu, akasema, ndiye huyu? Wakamwambia, ndiye huyu. Marra hiyo tena akavuliwa nguo zake akapewa mashiti mawili akaambiwa, sasa mwanamke wewe. Haya ondoka twende Pangani, alisema Major Wissmann. Bushiri akasema; mimi siendi kwa miguu illa unipe punda na kama hutaki nichinje papa hapa, bassi akamfunga mnyororo wa kiuno tena akampa punda. Kwani akasema nafsini mwake hatta akitoa maridadi mengi illakini atakufa. Bassi wakaja zao Pangani. Hatta walipofika watu wengi aliokuwa akiwaonea wakawa na furaha sana, hatta wake wa asikari wa Dachini wakapiga vigelegele kwani alikuwa akiwaua waume zao. Bassi siku ya pili Bushiri akafungwa mnyororo wa kiuno akatembezwa mjini mwote hatta Daani pia. Bassi tena walipokwisha Wadachi kumtembeza wakamvika nguo zake kanzu, na kilemba chake, na panga, na akashika jamvi mkononi, hivyo Bushiri akapigwa chapa. Hatta Dec. 15 alasili akahukumiwa kufa, askari wakaweka kamba katika mlingoti na chini ya mlingoti wakaweka pipa, (zile nguo zake nzuri zimeondolewa, amevaa zile za kwanza) bassi wakamwambia, panda juu pipani, akapanda. Tena juu ya mlingoti kulishuka kamba ikaja hatta karibu na

MSIMULIZI. 151

kitwa chake, nayo ilikuwa na tanzu. Bassi wakamwambia, ingiza shingo yako ndani ya tanzu, akaingiza. Tena wakamwambia, rudisha hilo tanzu mwenyewe, akalirudisha. Bassi asikari mmoja akaenda akaondoa lile pipa pale chini, bassi Bushiri akawa ananing'inia tu, na kamba shingoni, akaning'inia vile hatta akafa. Alipokufa Waarabu wenziwe wakaomba mwili wake, wakaenda wakauzika. Bassi hivyo ndivyo tulivyohadithiwa.

Bassi tena siku hizi kwa siku ya Dec. 22 Juma a pili tulipotoka kanisani ya kwanza asubui tukakaa kidogo, marra hiyo tulimwona Bwana Askofu pamoja na Mr. Mercer. Ah! tukawa na furaha mno kabisa kwani hatukuwa na habari, akakaa pale hatta karibu na alasiri wakaenda zao Magila. Y.M.M.

VITA YA PWANI.

Hatuna habari nyingi. Imetulia pande za Boonde. Lakini Saadani vita imekuwa kubwa, kwani Bwana Heri amepigana sana na Wadachi saa nyingi, boma lake likavunjwa, wengi wakauawa, mwenyewe akakimbia.

HABARI ZA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu habari hizi za petu.

Sisi wa Chama yetu ya Mchungaji aliye Mwema twafurahi sana kwa kuongezeka kwetu Dec. 5, wakaingia Chama ndio Annie H. Songolo, na Margaret D. Mariasa. Siku kuu ya Kuzaliwa Bwana wetu, wengi sana 195 walikwenda kushariki: na hatukupata kwenda kushinda popote, lakini tulifurahi papa hapa. Siku kuu yao Wasiokosa tulipata hatari ya nyuki, mtoto mmoja aliumizwa sana nao, hatta tuliogopa wote, na bibi yetu Miss Thackeray na watoto wengine pia, nyuki hizo zilijenga juu ya nyumba

MSIMULIZI. 152

yetu katika mfereji mmoja, lakini wote sasa hawajambo; nyuki hao wamechomwa sasa na Bwana Madan na wanaume watatu. Siku kuu ya Tohara tulipata usiku 'Christmas Tree' katika School, tukapata furaha sana si kwa zawadi tu, lakini kwa furaha ya moyo, na nussu ya wageni ndio Balyozi mdogo na Bibiye na Bwana Cecil na Bibiye na Waalimu wa nje na waume wao.

Jan. 9 ndio Alhamisi, palikuwa na harusi katika kanisa letu kubwa, ndio hawa, mwalimu Martin na Mildred, mwalimu Sona Annie, naye Peter na Josephine, nao wote wanakaa hapa Mbweni. Dec. 81 Miss R. Berkeley na ndugu yetu Blandina wamesafiri Ulaya, watakaa kwa mwaka mmoja. Jan. 25 Siku ya kuongoka kwake Paolo Mtume, wote Mbweni Mission tukaenda Mkunazini kwa kutiwa kwake Kasisi wetu wa kwanza mtu wa inchi hii Afrika.

Sala zilipokwisha, saa nane u nussu tukakaribishwa na Kasisi wa marikebuni Rev. J. A. Dougherty nyumba ya Telegraph kutazama mashindano ya mashua za Manowari za Kiingereza. Alasiri saa kumi tukarudi kwetu. Juma a pili Bwana Cecil akatoa Usharika wake wa kwanza hapa Mbweni; Mission zote na Wazungu pia wakaja kusharikishwa naye, na Askofu pia alikuwapo, na Archdeacon Jones-Bateman alimsayidia kusharikisha. Watu 96 wakashariki siku hiyo, kanisa likajaa watu sana.

Juma a tatu na Juma a nne tukapata siku kuu, Juma a nne wote Mission wakaja Mbweni kushinda. na bendera zilitundikwa nyingi pande zote, tena alasiri Wazungu wa merikebuni wakaja kwa chayi.

HABARI ZA MKUNAZINI

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu, nakuarifu yakuwa Dec. 27, twalikwenda Bawe sisi

MSIMULIZI 153

watoto wa kazi wa Mkunazini pamoja na Mr. Beetham, na Mr. Mallender.

Mimi na W. Boga, na Benny tumetoka kwa William Bishop, kwani amesafiri Mvita pamoja na Giles.

Benny na Willie Boga wamepata fundi Baniani, na Jan. 23, twalienda karamuni Mbweni. Feb. I, watoto wawili hapa walibatizwa, mmoja Yohana Mnubi, na wa pili Daniele Abdallah. Andrew Yakuti na James wamefika hapa, Andrew Yakuti amekuja kuoja pamoja na Clement Singano, na James Ramathani kuchagua mchumba. Mtoto mmoja jina lake Lizzy mtoto wa Florence wa Mombasa kafa jana Feb. 5.

HABARI ZA SHAMBA LA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Uwe rathi kwa barua za shamba la Mbweni safari hii si nyingi.

Watu waliooa January 9 kama ilivyo wanakaa hapa wote watatu. Jan. 19 palikuwa Ubatizo wa mtoto mmoja wa kike aliyetoka shamba la pili la Bibi Thackeray. Twalikuwa na habari ya huzuni nzito, sasa imetengenea ndiyo ya ndugu yetu mmoja aliyetumbukia katika habari ya kuuza na kununua watumwa, sasa tumempata tena, kwani amelirejea kundi lake la Umasihiya.

Furaha kuu tena tumemwona aliyethaniwa amelala Karthbat Othmani, mmoja wa wale waliopotea alipouawa Mr. Brooks Saadani. Huyu aliuzwa na Bwana Heri yule mkorofi wa Saadani kwenda Pemba, akawa huko Pemba kama mwaka mmoja. Hatimaye yule Mwarabu aliyemnunua alimwaminia vyote, hatta alimpa shauri afuatane naye kwenda Mrima kununua watumwa, bwana akasema, twende kwanza Zingibari baadaye twende Mrima. Bwanawe alitangulia kutoka Pemba kuja Zingibari akitumaini mtumwa atafuata

MSIMULIZI. 154

baadaye. Asijue kama yule mtumwawe aendako ndiko kwao, bassi naye akafuata tena akawasili bandarini January 28. January 29 tukamwona kwetu tukafurahiwa, kwani ana mke na mtoto wake aliyewaacha hapa akisafiri.

Siku hizi tunajengewa vizuri School yetu ya watoto wetu wa shamba. Salamu. M.F.

MCHEZO WA VITA KATIKA MNAZI MMOJA.

Katika Jan. 28 tuliondoka watoto wote wa Kiungani, billa wagonjwa, kama bado saa edashara ya usiku, tukaenda Mnazi Mmoja.

Tukakuta asikari wengi sana wa Kiingereza wamevalia vizuri vizuri, na mizinga pia wanajaribiwa na kujiweka tayari, katika njia kuu wamezunguka asikari za Sayid kuzuia watu wasipite na kuingia katikati, hatta General Mathews mwenyewe alikuwapo.

Bassi na katikati bandera nyingi sana zimewekwa za vita na zinginezo pia. Bassi baharini tukaona mashua nyingi sana zimejaa baharia wenyi selaha. Na walio Mnazi Mmoja nao wakawaenda na mizinga yao na bunduki. Na merikebu j zikapiga mizinga sana, maana yake ndio kufukuzia mbali adui walio pwani wasiwapige wale adui zao walio mashuani, na mizinga ipigwayo haina risasi illa baruti tu hatta bunduki zenyewe pia. Bassi merikebu zikipiga mizinga kufukuza adui, nao pia hawakubali wanapiga mizinga yao kuwapiga walio mashuani. Lakini marra mashua zikafika pwani baharia wengi wenyi selaha wakashuka, bassi wakapigana nao walio pwani, ikawa kama vita kweli katikati, wangine wamechukua vitanda tayari vya kuwachukua wanaopigwa, na wangine majembe pia wamechukua ya kuzikia.

Bassi walipokutana walipigana kwa bunduki na mizinga pia, wangine kuanguka kusudi na kuchukuliwa, wakipigana sana, hatta nafasi hapana ya kuwatazama wote, lakini marra

MSIMULIZI. 155

wakajipanga sawasawa tena, asikari mbali na baharia mbali.

Tena wote pia wakaamrisha kupumzika, na kunywa maji na kula kidogo, kwani killa mtu alichukua vitu vyake. Wakakaa kidogo tu, marra wakaamrisha killa mtu na bunduki yake wawe tayari, na yee apigaye tarumbeta akiwaamrisha ni mtoto mdogo tu.

Na marra ile akaja Sayid mwenyewe na asikari wapandao farasi, na yeye katika gari akitoka Chukwani. Akapita akaenda mbele kidogo, asikari wakaenda zao, yeye akaja peke yake katika gari: watu wengi kabisa wakajaa Mnazi mmoja. Tena Balyozi na Admeli pia walikuwapo, Balyozi akapanda farasi na upanga wake kiunoni: bassi Balyozi akamtwa Sayid akampeleka katikati karibu na asikari wake penyi alipo Admeli na General Mathews. Bassi mahali pale pamewekwa milingoti miwili kama mlango. Alipofika Sayid, Balyozi alimweka katikati ya milingoti hii miwili, marra zikapandishwa bandera ya Sayid na ya Mngereza, na watu wakubwa wakubwa wakimzunguka, na Balyozi na Admeli na Askofu pia, wote hawa walisimama, kwani Sayid alishuka katika gari, na lile gari likasogea mbele kidogo.

Bassi marra akafika Sayid akasimama. Matarumbeta yakalia na ngoma pia, wakampigia wimbo wake kwa kumsalimia. Tena wakapiga wimbo mwingine, ndio baharia wakipita mbele yake Sayid wakienda zao. Bassi baharia wakiisha kutoka, ukapigwa wimbo mwingine ndio walio asikari haswa wakaja mbele yake Sayid, na wakasimama. Bassi hawa ndio waliocheza sana, nao wengi sana. Wakasimama sawasawa, akatokea mkubwa wao: akawaamrisha killa kitu kama wakiwa vitani kweli, ilikuwa vizuri sana mtu akiangalia, hatta Sayid mwenyewe akaangalia yote haya. Wakaamrisha kwa bunduki wakichezacheza kama wanapigana kweli: bassi walipoisha, wenyi kazi ya ngoma

MSIMULIZI. 156

na filimbi, wakapiga; na asikari wakipita wakienda zao sawa sawa, hatta wakiinua miguu yao, utawaona wote kama mtu mmoja. Bassi walipotoka hawa wakaja baharia wenyi mizinga nao kucheza mbele ya Sayid kama wale wenzao: na sasa watu wamezidi kuwa wengi sana, asikari wapo pote wakizuia watu.

Bassi wakaamrisha wakajipanga sawasawa, wakapiga mizinga marra tatu, na hii ndio bunduki tu nyingi pamoja killa fungu na zao bunduki, lakini ni kama mizinga kwani zalia pamoja sawasawa: Sayid akiangalia tu. Tena wakaamrisha, killa mtu akakongoa mizinga, mwingine ameshika baruti ao gurudumu, ao vingine pia wakakimbia navyo. Maana yake ndio kama labuda wamezidiwa, nguvu hawana, watakongoa mizinga yote wakimbie na vitu, na adui akija hawezi kuuchukua ule mzinga ulioachwa, kwani killa kisayidiacho wamechukua.

Tena wakaamrisha, wakajipanga sawasawa, wakatoa panga. Bassi wakaamrisha kwa kupigana kwa panga tu, wakajaribia killa kitu kama adui atakavyomjia, na atakavyompiga kwa shoto na kuume pia, na kumkanyaga. Bassi walipoisha wakarudi penyi mizinga yao wakaichukua wakienda nayo, na Sayid akapanda garini mwake akaenda nyumbani kwake; wenyi matarumbeta na filimbi na vingine wakaimba, na sisi tukiangalia, ndio mwisho tukajirudia kwetu Kiungani saa pili. J. B. M.

HABARI ZA KIUNGANI.

Dec. 14, Bwana Askofu aliwasili Unguja akitoka Nyassa pamoja na watoto wanne, Peter Selenge, Yohana Nshanamilla, Tito Kungurukutu na Leonard M. Kangati, muda wa siku tano Bwana Askofu akaenda Magila. Dec. 24, tulipamba nyumba yetu. Dec. 25, ndio Siku kuu ya Kuzaliwa Bwana wetu, assubui tulienda Mkunazini kwa

MSIMULIZI. 157

sala kuu ya Usharika Mtakatifu, na kwa sala ya assubui pia; kiisha saa tano tukarudi hapa. Dec. 26, Siku kuu ya Stefanor Shahidi wa kwanza, saa tatu unussu tulitoka hapa wote tukaenda Mwera; hatta alasiri panapo kama kadiri ya saa kumi tukarudi zetu.

Dec. 27, tulishinda papa hapa, na wengine walicheza mpila. Dec. 28, Juma a mosi, saa saba unussu za mchana tulipewa zawadi wote chuoni.

Jan. 20; Bwana Askofu aliwasili tena Unguja akitoka pande za Bonde pamoja na watoto wanne, Samuel Sehoza, Archibald A. Semmanyi, Antonio Misimile na Richard Kambaku, nao wote wanakaa hapa Kiungani. Mtg.

HABARI KUBWA YA UGANDA.

Tumesikia leo hivi, ikiisha tengenezwa Msimulizi, habari kubwa sana itokayo Uganda. Umesikia zamani kidogo kama yule Mwanga aliwatesa Wamasihya, halafu akafukuzwa katika ufalme wake kwa fitina ya watu, alikaribishwa na Wamasihya, alipokuwa mtoro hana kitu, halafu akapata kutubu sana na kubatizwa kuwa Mmasihya mwenyewe, tusikiavyo; bassi tena Wamasihya wengi na wengine wakaenda wakajiunga naye wakakaa katika kisiwa kimoja kinacholekea mji mkubwa wa Uganda kinakwitwa Sese, wakangoja kuuawa na Waarabu na watu wake Kiwewa atawalaye wasipodiriki kuwafukuza. (Tazama katika Msimulizi wa December)

Bassi Waarabu kwa upande wao wakakusanya watu wengi na baruti tele na jeshi wakasema, tuwafutie mbali Mwanga na Wanazareni wake katika inchi hii, wasitokee tena kabisa.

Bassi Waarabu wengi wakuu wakaingia katika chombo kikubwa kilichojaa asikari na baruti tele, na wengine katika mashua ngine, walete vita huko Sese, lakini walipokaribia

MSIMULIZI. 158

ikapigwa bunduki ya pwani ikapata chombo kile kikubwa na baruti kwa pigo lile moja ikapata moto, marra chombo chote kikapasuliwa vipande elfu kwa nguvu za baruti ile na watu waliomo wakafa marra.

Marra watu wa Mwanga wakiona hii wakaingia mitumbwi yao, wakarudi hima hatta mji mkuu, wakautwaa wakapigana sana wakatwaa inchi yote wakawaua Waarabu wote hatta ni watatu tu waliosalia hayi, na wakatwaa pembe za adui zao hatta thamani yao ni £400,000.

Na sasa Mwanga anatawala Uganda yote, na rafiki zake ni Wazungu na Wamasihiya.

Hii ndio habari kubwa sana, nasi twatumaini kama sasa Anjili itapata nafasi ya kuendelea na kuenea huko.

Habari hii imeletwa katika barua za Waarabu wenyewe wa upande ule wakiwaandikia ndugu zao hapa Unguja. P.L.J.B.

Feb. 13, Alhamisi tumepata habari yakuwa Seyid Khalifa amefariki saa saba ya usiku, akazikwa usiku, bassi sasa amemiliki mahali pake ndugu yake Seyid Ali, ndiyo habari. Mtg.

MSIMULIZI. 159

Mtu mmoja mtani ameniletea sanamu hizi sijui zitapendeza.

Watu wanaonikaribisha mimi, Msimulizi, kwa furaha!

Watu wanaochungulia tu vitabu vya wenzao!

Msimulizi.

MSIMULIZI. April, 1890. X.

Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,

katika "Universities' Mission to Central Aerica."

LIKOMA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Nov. & Dec.

Katika hiyo iliyokuja nimekwambia kama sina habari tena nimesema kama nakwenda pande za chini kumtafuta Bwana Johnson, kwani siku nyingi zimepita bado kuonana naye. Bassi sikia, Mtengenezaji. Twalitoka hapa juma a tatu Nov. 18, tukaenda wee hatta pa Pachia. Tukatia nanga kwa kununua kuni, mimi nikapewa ruksa na Nakhotha (Gaptain) ya kushuka pwani. Bassi nikashuka sikumkuta mtu, illa John Padyela, kwani wote wako Likoma pamoja na wake wao. Bassi nikauliza habari za vita ya pa Msumba, wakasema, Wangoni wamepita kwenda pande za chini kuelekea Msumba, na habari za wale waliotoka kwangu mateka wa pa Msumba, wametoka pia, hawakufanya thulumu sana illa wameng'oa mihogo ya watu kula wao. Jahazi (Steamer) ilipokwisha pakia kuni tukaingia tukaenda kidogo hatta pa Msumba pa mzee Augustine na Daudi aliyeitwa zamani Benyamin. Hapa pia nikashuka nikaenda kumtwaa mzee Augustine kuja jahazini, nikaja naye. Akina bwana wa humo wakamuliza, habari zote ni njema? je za Wangoni? Wangoni. Bwana, Ah, wameuawa watu kumi, hamsini ao thelathini, wamekamatwa mateka na umbu lake mfalme Masanehe pia amekamatwa. Bassi tena tukashuka pwani nyumbani pake, tukaongea wee, kwani kwa miezi ile kenda sijaonana naye, na hapo Nakhotha alinipa ruksa kukaa naye kwa kadri niwezavyo. Kama saa tatu unussu nikarudi jahazini, tukalala. Hatta assubui mapema kama saa kumi jahazi ikang'oa, tukaenda wee hatta

ilipotimia saa kumi ya alasiri tukafika pa Livingstonia. Nakhotha peke yake akashuka kuuliza habari za Bwana Johnson marra

MSIMULIZI. 160

akaambiwa kama yu mzima naye, yu hapa pa Monkey Bay (kwani Monkey Bay ao Mlambuzi ni upande wa pili wa mlima karibu sana na Livingstonia mwendo wa saa tatu ao mbili), amekuja jana. Bassi Nakhotha Belcher akarudi akatupasha habari hiyo yakuwa yupo! wala hatuna kazi ya kwenda chini. Kwani bwana Johnson yupo hapa pa Monkey Bay. Tukashukuru sana kwa rehema za Mnungu. Siku ile tukatua pale pa Livingstonia na kupakia mizigo iliyotoka pande za chini nayo ililetwa na jahazi moja ya Lakes Company (kwani hawa Lakes Company wanayo Steamer mpya kati ya Ilala na Lady Nyassa, na ingine tena hii mpya walianza mwezi wa Nov. 1888 kuunda, bassi imekwisha mwezi wa Nov. 1889, ndio ikatokea huku juu kwenda pande za kaskazini. Bassi ndivyo wakapakia wee hatta wakaisha. Assubui tukang'oa kwenda Monkey-Bay tukafika, Bwana Johnson tukamkuta yu mzima, lakini si mwenyi afya, illa kwa sababu ya kustahimili kwake tu, ndio kuonekana kama mzima. Tukaamkiana pale, tukafurahiwa sana kwa kumwona. Na hapa pia tukapakia mizigo iliokwenda katika mashua, napo pia tukalala. Assubui mapema tukang'oa nanga kukimbilia pande za juu kwani vitu vinatakiwa.

Habari zingine kidogo. Ndio huzuni sana kusema, nimekwambia kama hivyo mwezi wa Oct. 15, 1889 Bwana Dr. Hine ameshika safari ya kuja huko. Bassi bwana kwa uthia huo wa njiani amekaa hapo pa Livingstonia, bassi sisi tukamkuta, naye amethoofika sana kupita cheo. Bassi siku hiyo ya Juma a tano tukampakia katika hiyo 'Steelboat', na Bwana Johnson akatafuta watu wakuvuta makasia, akaingia pamoja na Mr. Williams na mtoto mmoja tunayemleta huko jina lake Jack, na Mmasihiya mmoja wa huku huku, jina lake Musa Kalulu wa Mission, amejikomboa mwenyewe kwa kusayidiwa na Mission. Bassi huyu akarudi pamoja na Mr. Williams wakiishamfikisha huko

MSIMULIZI. 161

Blantyre. Bassi sisi tukawafanyia rathi hiyo kidogo marra tukang'oa nanga ya kukimbilia mbele, kwani Bwana Johnson baada ya kusikia habari ya vita hiyo ya pa Msumba alitaka kwenda upesi upesi, apate kuona hali yake. Bassi siku hiyo ya Juma a tano tukapiga mwendo wee hatta alasiri tukafika pa Msumba, mimi na bwana Johnson tukashuka kwenda kwa mzee Augustine na kumpa barua, kwani meli ya Unguja ndio kwanza ije, kwa miezi miwili twalikuwa hatujapata barua zenu wala huyo Msimulizi! hatta hivi nisemavyo, huyo Msimulizi bado kupata. Sijui yuko wapi! bassi ndugu Mtengenezaji, wasikia? Hapo tukalala, mimi nikalala kwa Augustine inchi kavu, Bwana Johnson akalala jahazini. Bassi siku hiyo twaliongea mimi na mzee Augustine hatta saa sita ya usiku, kwa sababu kwa miezi kenda bado kuonana, bassi ndio hivyo hatukwenda kulala upesi mpaka nikashindwa mimi nikasema afathali tulale, ndipo tukaenda kulala kwa saa nne hizo zilizobakia. Assubui ulipokuja tukaongea tena kwa kadri, marra tukaingia jahazini, tukaenda marra tukafika Pachia pa akina waalimu Paul Mambo. Hapo hapana mtu, sababu hii: mwalimu Eustace yuko pande za chini mahali panaitwa Monkey-Bay, na mkewe yuko Mlikoma, Paul Mambo yuko Mlikoma pamoja na mkewe, alikwenda nao pale walipokimbia vita, bassi hapana mtu illa John Padyela tu anangojea nyumba hizo. Tulipotoka hapo tukaja pande za pa Chisanga akaapo Aruffo, tukamkuta yupo, lakini peke yake kwani mkewe alikwenda pande za Likoma. Bassi tukashuka mimi na baba Johnson, tukamkuta Aruffo yupo vile vile. Bwana akamwambia, awaite waanafunzi, wakaja, lakini kwa nussu saa kuwaita, kwani yuko mlango wa pili. Bassi walipokuja baba Johnson akaongea nao wee na kuwaambia sababu yake nini kukawia hivi pande za chini na kuwaambia, Sasa nakimbilia Likoma kuonana na Bwana mkubwa wa humo, kwani

MSIMULIZI. 162

kwa mwezi huu bado kuonana naye. Bassi tukatoka tukaingia jahazini tukaja zetu hapa Mlikoma. Furaha kuonana na bwana Johnson. Bassi hizi ndizo habari nilizo nazo. (Steamer) jahazi ya moshi yarudi tena pande za jamaa zetu pande za Pachia kuwarudisha wenzetu waliokuja Mlikoma kwa kukimbia vita. Sasa wamerudi katika miji yao vile vile. Bwana Johnson alipofika hapa, na waliposoma barua za kote kote wakaona kama Bwana Frere haji upesi, Bassi wakaanza kufanya shauri, ndio Bwana Archdeacon Maples aende zake hatta Ulaya marra moja, kusudi mwaka huu wa pili ukija arudi papa hapa. Bassi ndivyo ilivyo. Panapo kesho Bwana Archdeacon anapanda milima hiyo pande za mashariki, kwani anapita njia ya juu pamoja na watu kama sitashara hivyo. Sisi hapa tutasalia na Wazungu haba tu; kwani wamekwisha kwenda zao. Bassi tumekuwa masikini kama ninyi mlivyokuwa mwezi wa jana. Lakini tufanyeje? hayana buddi yawe, fanyeni bidii kwa sala zenu kazi yetu isilegee.

Kweli sala zenu zinatakiwa sana pande hizi kwani sikieni. Mwajua kama baba Johnson ni mtu wa kwenda killa mahali. Bassi pale alipoendea mashua ya chuma (kama niliyoandika katika Msimulizi ingine), pale aliporudi nyuma kwa bahari ya Malombe, wakashuka wakaenda njia ya inchi kavu, Bass humo njiani Baba huyu alipata mashaka sana, kwani alikuwa hawezi, na tena siku moja alishikwa na kiu sana, na nguvu hana, marra akawatuma watu wawili kwenda kutafuta maji, kwani wako mbali na bahari ya Malombe. Na pale walipotumainia maji kama yapo mbele yetu wakakuta pamekauka kabisa. Bassi yee bwana akajitupa chini penyi miiba na kivuli kidogo tu kipo, na macho ya kopeakopea, wale watoto walio naye wakaogopa sana, wakathani kama atawafia tu hapana shaka. MarrA akafunua macho akaitwaa asali akaionja, lakini haimfai, akauliza,

MSIMULIZI. 163

Je! Ulaya na Milonje wafika? (haya ndio majina yao walio kwenda kutafuta maji), wale watoto wakajibu, bado kabisa, Bassi wakangoja hatta kama saa kumi alasiri wakafika watu wale na maji upesi upesi, marra akaamka pale akanywa, akanywa, akapata nguvu ya kwendea mbele, bassi hivyo ndivyo, na mambo mengine. Bassi mwaonaje? na maneno haya nimeambiwa na watoto waliofuatana naye. W.E.K.

HABARI ZA MBWENI

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Safari hii hapana habari, illa hizi chache tu. March 25. Mngoje wetu Mr. G. Dale ametoka hapa kwenda Magila kufanya kazi kule. Na sisi tuna bwana Mr. J. E. C. Key mahali pake.

Na pamoja naye amekuja bibi Miss M. A. Boyd. Safari moja wametoka Ulaya wakaja Mbweni wote wawili March 23 na huyu Bibi afanya kazi ya School.

Na siku kuu ya Pasaka, tumekula papa hapa tangu Juma a pili hatta Juma a nne, na alasiri ya Juma a nne watoto wa Kiungani na bwana Ven. Arch. Jones-Bateman wakaja kushinda kwa saa mbili hapa Mbweni. R.M.

HABARI ZA SHAMBA LA MBWENI

Rwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Yule Farijalla aliyenenwa yuko Nyassa pamoja na barozi Con. Johnson karejea hapa Mbweni, Feb. 25,

K. Othmani tuliyemnena sasa kasafiri kwenda kulimia njia itokayo Mvita hatta Kilimanjaro, pamoja naye Edward Juma, Palmer Majaliwa, Hugh Kambenga, Philip Mpande, Kikafa na Hamisi. Pemba na mkewe Siwema kasafiri kwenda Magila kwa kazi ya kuvunja

MSIMULIZI. 164

mawe. Paul Changwe aliyetoka Magila na mkewe wanakaa Mbweni na Rupert Mwarabu na mkewe. School yetu tulioinena mwezi wa juzi imeisha, imezinduliwa April 9, sasa tunaitumia.

Siku kuu yetu ya Pasaka ilikuwa hapa petu. Pana watu wajao hapa Mbweni wakiwa wagonjwa kwa dawa, maana bwana zao huwatupa wakati wao wa ugonjwa, mmoja wa hawa kafa April 9. Furaha kubwa kwa wote Mbweni waliosafiri wote wamerudi salama, ndio hao:

Ibrahimu Mbaruku, Augustino Kamwendo, William Chawanda, Salimu, Sokoroko, Mitawa, Hassani, Mwanza, Sulemani, Uledi, Farijala, Muoa, Mpenzeni, Tiwale, Buheti, na Farijalla, hawa wamerejea wote, April 8. Waliobatizwa siku ilio mbele ya Pasaka, Yakobo Chaneema, Godfrey Mitimingi, Klementina Laiti.

Taabu za Afrika zitakwisha lini?

Habari zetu kama ilivyo juu ndio nyingi katika zote. Ikawa siku ile ile ya harusi ya C. Singano na Emily Beza na A. Yakuti na M. Shantu, mmoja wa watu wa Mbweni, jina lake Nicholas Neiluwa alikilima katika kikonde chake, alipoinuka aona mtoto kama wa umri wa miaka labda 6 ao 8, naye hajui Kiswahili akamwuliza, habari zake, mtoto akajibu, Mimi ni mtumwa, nalikuwa katika chombo tukienda Pemba tukafika karibu ya pwani upande wa Kusini Zanzibar ndio Chukwani, ikawa usiku mimi nikaruka majini nikaogelea hatta pwani, Chombo kikaenda joshi, na sasa natafuta ulindo. Mtu akamtwaa mtoto akaja naye kwake nyumbani, hatimaye akamleta kwangu nisiweze maneno nikaamru aende kwa Mr. G. Dale, naye akampeleka kwa Lieut. Smith, naye hatujui alivyoona, akamrejeza akampa Bwana G. Dale, akaamru akakae naye yule mtu;

MSIMULIZI. 165

na jina la mtoto Mambo, kabila Mbemba, siku hizi anajifunza kusoma pamoja na watoto wa shamba.

Ilikuwa siku ya 11 ya March, nalienda tembea nionane na watu wa Mpakani, mimi na Nicholas Faraji, tukirejea tukapewa habari ya kuwa kama mtu mwanamke kaja kwa Bwana G. Dale, tukifika kwangu tukamwona, tukamwuliza habari, akasema, Mimi ni mtumwa nimetoka pwani, bwana wangu na bibi yangu amekufa, nami sina ulindo sasa, natafuta kwa Mzungu huenda nikapata. Bwana akaamru alale, hatta asubui atakwenda kwa Lieut. Smith. Kukicha akapelekwa kwa Lieut. Smith huko akapelekwa kwa barozi mkubwa hatujui lililompata tena.

Ikawa siku ya 20 ya March, nikasikia ya kwamba kumekuja mtu mwanamke kwa Bwana Bev. Gr. Dale, yuko nyumba ya serkali, nikaenda nikamwona, nikamwuliza habari. Akasema, Mimi nalikuwa na bwana wangu jina lake Sulemani tukikaa Bagamoyo, bwana akafunga safari kwenda Nyenyembe huko akafa, tukakaa tusirithiwe. Hatta wakati wa vita ya Wadachi ilipoingia, akaja mtu tu Mswahili akasema, Mimi nitawakimbiza vita hii kwenda Unguja, wakakubali, nao ni watu tissa. Akawaleta Unguja hatta maweni, alipowaleta akakaa nao siku chache akaanza kuwauza, wakasalia wanne, nao wakasema, Loh! habari gani hii? tuende zetu tutafute ulindo. Wakashika njia ya mjini, mmoja wao akaulizauliza akaambiwa ulindo mwema ni kwa Mzungu akashika njia hatta Mbweni. Siku ya pili yake Ijumaa March 21, Mr. Dale akampeleka kwa Lieut. Smith, huyu akasema, Vema, nitakwenda nawe hatta kwa barozi mkubwa. Hatta siku ya March 22 tukampeleka, alifuatana nasi kwenda kwa barozi mkubwa Con. E. Smith. Hatujui tena la huko.

Pana mtu mshukhuri Mbweni jina lake Adamu, kwa taifa Mnyassa. Kwao ni mtu wa ndugu wengi, akapotea

166 MSIMULIZI.

kama tulivyo wa Afrika, kwa wema wake akafika serikali hii ya Ingreza, kupotea kwake na nduguze pia. Wangine kaonana nao hapa Unguja, wangine huru, wangine siyo. Na mmoja yupo hapa illa anakaa Unguja Kuu, ndiko bwana wake akaako, na bwana huyu ana watumwa wengi na shamba kubwa sana.

Huyu akafika hapa Unguja siku moja akapata sikia jina la nduguye linatajwa, naye akafanya bidii kutafuta. Hatimaye akatokea Mbweni akaonana na nduguye ndiye Adamu, naye akatafuta apateje kumwondoa utumwani, akamtwaa akampeleka kwa Bwana Askofu wetu, akampa habari zote zao. Bwana akasema, Wema, wallakini twende kwa mkuu wa askari General Mathews atafute askari waende hatta kwa bwanawe tusikie atakavyonenewa. Wakafika kwa mkuu wa askari, wakapatana vema, Nitapeleka kesho watu, wallakini leo nendeni naye kesho mlete hapa. Akarejea naye, hatta keshoye akampeleka kwa mkuu wa askari naye siku hiyo anaondoka kwenda Momboi, akaamuru apelekwe kwa Mohemedi Ibun Seyid ndiye aliye wa pili. huyu asipeleke watu, la! akatafuta watokao kule awape khati asiwapate kwa siku mbili, hatimaye akamwambia Adamu, kakae naye hatta wajapo wa kwa bwanawe. Akakaa naye hatta kurudi General Mathew Mombei. Ilikuwa siku ya Alhamisi March 13, akaja mmoja wa wajoli wake ndiye noko wao, pamoja naye Adamu hapo yu nyumba kubwa Mission. Yule akiwaona wajoli wake, akafuta kisu apigane, hatimaye akaenda mbio, wajoliwe hawakufanya neno wala hawakusema naye, la? vyote walimtazama tu. Hatimaye akaja Adamu akapewa habari zao, Je? yule ndugu yangu wapo? wakamjibia kakimbia, wakamwonyesha njia alioiendea akafuata akamkamata akaja naye, yeye akasema, Mimi huko kwa bwana siendi na hawa sitaki kuwatazama hatta

MSIMULIZI. 167

kidogo, Ndugu amjibia, Ukiwa hali hiyo, mambo yatakuwaje tena kama hivyo? Wajoli wake walisema, Tupe mtu wetu, aliwajibia La! twendeni kwa General Mathews, huko ilivyo mtapata vyo vyote.

Ikawa saa ya tatu ya mchana, wakashika njia ya pwani kwa pwani, hatta kwa nyumba ya Missioni ya Wafransa, yule aka watoroka, wakamtafuta, wasimwone, hatta kwa majira ya saa 7 wasimwone. Aliyekimbia akaenda hatta nyumba iuzwayo tembo akanunua akanywa. Kiisha akashika njia kurudi Mbweni, akawasili hatta kwa njia kuu palipo mwembe mkubwa penyi njia ya pande moja yatoka Kiungani kwenda wanda wa Foot-ball, kubwa yaenda kote ya tatu yaenda Jang'ombe. Hapo alikutana nao wachukua zambarau, nao ni watu sita akawachokoza, wakampiga sana, hatimaye wakamwacha wakaenda zao. Yeye akajikokota hatta palipo kisiti cha mzambarau akalala, nguvu hana. Hatta saa 9 Adamu anarejea kutoka mjini saa hizo akafikia pale pale naye alithania labda kafa, akarudi kwa watu wa pale mwembe akawauliza, wakampa habari zao pia, naye akatwaa mtu akamleta kutwaa kitanda kwa yule athaniwa kafa kabisa kwani alipigwa sana. Wakaleta kitanda wakamtwaa juu ya kitanda hatta saa ya kwanza usiku akafika Mbweni. Akatiwa dawa na Bibi mganga, akashinda siku ya Ijumaa, hatta siku ya Juma a mosi ikaamriwa tumpeleke kwa mkuu wa askari, tukamtia garini mwa ng'ombe na yule noko wake yupo nasi pia. Tukamchukua hatta Mkunazini tukamtoa garini akaenda kwa miguu illa kwa shidda sana, tukampeleka kwanza kwa mganga mkuu wa Kiingereza kuona kama sehemu ya viungo vimevunjika. Hatimaye tukaenda kwa mkuu wa askari tukatoa khati, akapewa, akatumania tuende kwa Mohemedi bin Seyd. Tukapewa askari kufuatana nasi, tukaenda, hatta kwa

MSIMULIZI. 168

saa ya 8 akatokea barazani tukaingia kwa hukumu. Ikahukumiwa arudi kwa bwana wake, maana kaharibu kutaka kupigana, tena kutoroka njiani, kulewa pia. Akapewa nokoa wao, sisi tukarudi kwa duka la Hosseni, kwani ndipo tutiapo nanga yetu killa Juma a mosi. Tukikaa kidogo twaona mtu wa jamaa ya Adamu, aleta habari ya kuwa yule mtu katoroka tena sasa ikaja kwangu. Tukamwambia, Mmpeleke kwa Mohemedi bin Seyid. Saa kumi tukatoka kuja kwetu tukawasili saa thenashara unussu, hatta asubui twamwona mtu yule yule ametoroka tena akaja kwa Adamu. Tukamwambia haiyamkini tena kukaa maana umeharibu wewe mwenyewe. Tukamfunga akapelekwa kwa Mohemedi bin Seyid. Hatujui tena yamekuwaje.

UWAREHEMIE WAISLAMU WALIO VIPOFU ROHONI.

Kuna watu walio hadimu Balyozi, wanakaa kati ya shamba la Mfalme wa Zingibari, maana ni halali kwa awaye yote kukaa. Katika hawa pana mmoja aliyejulika nami, naye appenda sana kujifunza ya Kimasihiya, jina lake Sahela. Siku moja nikatembea pwani kwa bandari ya Kapepha, nikamkuta Sahela, na pamoja naye mtu mmoja, nikamwuliza Sahela ya kwamba yu nani? akaniambia, Ni mwalimu wa Kiislamu jina lake Mzee. Nalimtazama sana huyu mwalimu, akanitambua ya kwamba twalionana Bagamoyo yeye alipokielemishwa nami ni mtoto wakati huo. Hatta mwenyewe nikamtambua na pahali alipoelemishwa nalipaona kweli hakika.

Siku zote nimezowea kwake kwa Sahela, karibu killa siku jioni kama saa 11 ao saa kumi unussu na huyu mwalimu humkuta kule, nami humwuliza kidogo neno moja ya Imani yake, nami hujadiliana naye kwa wakati. Siku moja nalienda na sehemu ya Ilkoran, ile ianzayo. Wamemwuliza

MSIMULIZI. 179

marra nyingi wathanije nikamwuliza, Maandiko nusu ya Ilkoran na desturi zimetoka wapi? Akanijibia, Katika Teurati (Torati), maana yake kwa Wayahudi. Nikamwuliza tena nikamwambia, Waonaje? sio hiyo tulionayo sisi Wanazareti, mbona hamuungani pamoja nasi mkiwa nayo Teurati yetu? Asiwe tena kushindana nami. Kwa wakati mwingine nalimuliza maana ya Ukafiri nini? Akanipa jibu jema ya kwamba ni wale wasiomjua Mola. Nikamwambia Ni vema, walakini mbona sisi Wanazareti mwatuita makafiri nasi tukiwa twamjua Mola kathalika nanyi. Akanijibu, Sababu ninyi mwachanganya Dini ya Mola pamoja na kuabudu miti (maana yake Msalaba) na tena sanamu Wazungu wanachonga, hii ndio sababu tukawaiteni makafiri. Nikamwambia Vema, walakini je? waonaje, wewe waweza kutangua Maandiko ya Ilkoran? Asema, La! siwezi, maana maneno yote ni ya Muungu. Nalimtolea maneno ya Muhamadi katika Ukoran hivi, 'Bassi mataifa wawili waliopewa kitabu ndio Wayahudi na Wamasihya, na tena nyie watu wa kitabu hamna ya kusimamia msiposhika Teurati na Anjili. Nalimwuliza, Ukiniita mimi mkafiri, maana yake umetangua maneno ya Muhamadi. Akasema, Kweli. Na tena nalimwambia habari za msalaba nalimwambia, 'Waliona wapi ufalme usio na bandera zake, uko wapi? Nikamwuliza tena, Bassi nionyeshe bandera ya Dini ya Kiislamu kama unayo? Asiwe na neno illa, kushangaa tu, na kusema, Ah! mkafiri huyu amejaliwa.

Sasa nimemwona anaanza kutaka kujifunza ya Umasihya. Akizidi kutaka labda atajaliwa naye avipaye vyote uzima. M.F.

HABARI ZA NEWALA.

January 27, 1890.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu, nataka kukuarifu habari kidogo za Christmas.

MSIMULIZI. 170

Juma a tatu hatukusoma, twalitengeneza nyumba na kanisa letu. Juma a nne twalienda kufua nguo zetu na nguo za kanisani, na watoto wengine wakapewa visibao, tena tukachinja mbuzi kwa waanake.

Juma a tano ndio Siku Kuu ya kuzaliwa Bwana wetu, asubui na mapema Mwalimu Daudi Machina na Samwil Chiponde, na Enoch Mtaiwa na watoto wanne Luka Lichinga, Bernado Mpungu, Bikarito Sulemani na Leonardo W. Liwenga, walitwaa vitabu vya nyimbo za Kuzaliwa wakaimba asubui na mapema. Halafu Saa kenda waanake wakaja kula, na jioni tukafanyiwa sanamu za taa, na zilipokwisha wakaimba wimbo.

Alhamisi wakaja watu wa Chitangali saa tano pamoja na mfalme wao Maluchila, tukachinja mbuzi wawili kwa waanaume Wakala Wamasihya na Wanafunzi tu. Ijumaa ilikuwa mashindano ya kukimbia, kuruka, na kutupa risasi, lakini hayakuwa mashindano makubwa, illa yalikuwa mashindano ya watoto wadogo tu. Juma a pili ya Wonyeshe tumepokea zawadi, wengine kofia, wengine mishipi, na wengineo lesu. Hapa tulifanyiwa Examination, nao walioshinda katika darasa ya kwanza ndio, 1. Cecil Majula, 2. Bernado Mpunga, 3. Daniel Usufu. Katika darasa ya pili, Johana G. M. 2. Tomaso, 3. Siluano, 4. Lulenje. Watu wa Masasi walikuja hapa, lakini walikuta karamu imekwisha. Mr. Hainsworth na Mr. Smith walikuja hapa, tena watoto wa hapa Newala walienda Masasi pamoja na watoto wa Chitangali. Mr. Porter amekwenda Masasi. Mwalimu Daudi Machina na watoto wengine walienda kuwinda Mtangala, Daudi Machina ameua ndogolo. C.M.

HABARI ZA MLOLELA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Tumefurahi mno hapa MlOLELA kwa kumpata Kasisi aliye wa kabila letu

MSIMULIZI. 171

la Kiyao kama sisi. Tumempokea kwa furaha mno tunajivuna sana sisi kwa kupata Kasisi wa kabila letu kuliko ninyi mnaokaa katika miji ya upelekwa mingine yote. Tena mzee Banaba Nakaam siku hizi amejenga maboma mawili kuutengeneza mji wake tayari kusudi wakija Makwangwara apigane nao, miji yake yote miwili iitwayo Msokosela na Msati ameiweka ndani ya boma.

School yetu inaendelea sana, watoto wameongezeka sana wapata 77, na wale wajao kufundishwa pia wapata 54. Y.B.A.

HABARI ZA MASASI.

Salama kwa Mtengenezaji. Baada ya salamu, ninapenda nikuhadithie tangu tulipotoka Unguja hatta Lindi. Bassi Juma a pili Dec. 5, 1889 tukawa tukipita Mbweni asubui hatta Juma a tatu tukaingia Darsalam na miji ingine ya pwani pwani, hatta tukawasili Kwale ya Mlima, chombo kikavuja kidogo tukashinda pale siku oja. Tukatweka pale tukapita kwa Kisimani (Mafya) tukaenda mpaka kuwasili Kilwa Alhamisi. Bassi naye nakhotha Nasibu mkorofi mno na mthia pia, hatta vitu vyetu haweki taratibu, sisi tumekaa juu ya paa, mvua yetu jua letu. Kwanza mbele tumemwambia kama angalia tusiingie Kilwa, akanena, Kwa nini? mimi na kme wangu na watoto wangu nisiingie kwea nini? Bassi akamwambia mke wangu sharti avue nguo za Kizungu asivae illa Kiswahili tu, kwani tukijulikana kama tumepakia vitu vya Mzungu, jahazi itapandishwa pwani, killa kitu kitaangamia nami nitafungwa. Bassi tulipowasili Kilwa nikamwambia, Bassi heri tusishinde, kesho tutoke. Oh! nikimbie nini na hapa ni petu? Kama vitu vya Mzungu, mimi kee! ningekataa kule kule, isipokuwa tamaa tu ya Banyani ya fetha ndio maana mimi nimekubali kupakia vitu vyenu, kee! kuna mtu atakayempendelea kafiri? Nikamwambia, Angalia bado

MSIMULIZI 172

tena, matini haya ya chuma umeyaweka juu kama haithuru, lakini haya mali ya watu jee? hatta wewe ukiuzwa hupati kima cha mali yaliomo humu jahazini. Akanena, Mpuuzi wee! mimi nashinda kesho, potelea mbali.

Akashuka. Mambo ya Waswahili mwajua maana ya kushuka wote, ndio desturi yao killa bandari. Bassi mimi ikanitoka kauri kama, Angalia wewe jahazi hii kuionelea watu wa Kilwa; ukija wewe nao utaona nawe pia papo hapo. Akashuka.

Bassi asubui Ijumaa nikasikia habari kama nakhotha anena atakaa mpaka Juma a mosi, nikanena, Vema. Marra akaja mtu wa chombo chingine alikuwa amemleta baharia wetu katika mashua yake. Akauliza, sasa matangi haya ya nani na yaenda wapi? baharia wetu akanena uwongo, akanena, Ya Baniani yaenda Lindi-Mgao. Akajibu Eeh! Banyani na Mzungu si mamoja? wote kathalika mfano. Akanyamaa yule mtu. Mimi nikaandika barua ya Kiswahili kwa siri nikampa baharia aliye amini ampelekee Banyani, kwani nalisikia kama tajiri nduguye mwenyi chombo yupo Kilwa, lakini burre tu, kwani hakumkuta Banyani mwenyewe. Halafu akarudi akanipa barua na mashauri kama barua si kitu cha siri, heri uniagize kwa maneno tu. Bassi nikamwagiza akaenda akamkuta akamwarifu yote pia, Banyani akanena, Bassi ukamwambie Inshallah kesho atatweka, lakini atulie wala asishuke kabisa.

Bassi tukasikia kijana amefungwa, alifuatana zamani na Wazungu merikebuni amekuja Kilwa ndiko kwa wazee wake. Hatta usiku tukasikia ngoma za vita zikilia, watu wakakusanyika penyi walipoweka mizinga yao ya siri mahala, pa nne ya kuvizia wasiwaibie usiku. Kwani ilikuja khati kutoka Unguja kunena, waangalie kama Wadachi watakuja karibu kupiga Kilwa ndio maana mji ukataharuki sana killa mtu, zayidi watu wa Mlima ndio wenyi nguvu

MSIMULIZI, 173

Kilwa, Wayao waliotoka tangu zamani kwa Makanjila na Mataka pia. Bassi assubui kama saa ya kwanza Juma amosi, tukatweka, kwani Banyani mwenyi chombo alimhimiza sana asikae tena, kwani hatta leo mjini hakukutulia, uthia mtupu. Bassi nakhotha akaingia akanena vilevile miye nikanyamaa, tukawasili Lindi, akaenda kumwambia Premji kama nimefanya uthia njiani, kumbe hatta pale akataka tena kunitoza kama reale mbili, kwa uthalimu mtupu, lakini mimi nikamwacha nikaepuka, kwani nimewasili nilikotaka, tukaenda zetu kwetu Juma a tatu. P.K.

HABARI ZA MKUZI.

Feb. 26, 1890.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu, sasa hivi kama saa kwanza unusu twaona Sehiza na Sekimwaga waingia hapa kwangu na kusema, Ondoka, wageni hawa wa Madachi. Nikatoka naona asikari mmoja wa Madachi na barua mkononi nikapokea, nikampa Mr. Allen akaipasua. Ikatoka na yangu ya kusema, Madachi watakuja kesho Alhamisi asubui na watu waambiwe kuleta unga, ndizi, mayayi na vitu vingi, kuuza, na tena Sehiza asijifiche, salamu. Na asikari yule akauliza maji, tukamwonyesha kisima chetu, wakasema, Tutakilinda mpaka wengine waje tupate maji, kwani hapana maji mangine illa haya karibu. Mr. Allen akanipa taa ya mkono, marra nikaenda mji wa Mkuzi kumwambia yule Sehiza kupata watu kuenda Kwebara, Hemwae, Kibanda, na miji ya kichaka hiki, na watu wa hapa walikuwa wakisikia tu, bado kumwona Mdachi. Bassi leo imekuwa kitisho, kwa saa tatu ya assubui twaona marra asikari mmoja mbele, tena farasi wa akida wao, ndiye Mr. Schmidt, naye frasi wake mweupe na asikari wakipita nje ya boma yetu, mkuu

MSIMULIZI. 174

wao tu ndiye aliyeingia ndani ya boma, na asikari wakipita kama maji, na akida wadogo, wamepangwa ndani mwao mpaka mwisho, nao wote kusikia kama watu mia tano au mia tatu. Ugeni uko sasa kule mzambarauni karibu na kisima kile walicho kizuwia watu wasiteke. Hatta athuuri haikufika kimekaushwa na matumbo ya watu na kupika bado. J. S.

HABARI ZA MKUNAZINI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu, nakuletea habari hizi. Pasaka Juma a tatu yake tulikwenda Bawe pamoja na Mr. Bishop, tukashinda huko hatta jioni tukarudi. Andrew Yakuti na na mkewe Maria Shantu amekwisha kurudi Magila. Francis Limamu amefariki siku ya Juma a tano kuamkia Alhamisi April 2. Mr. Beetham na Sisters wawili wamekwenda Magila, tena meli hii Miss Shaw amerudi pamoja na Mr. Key.

Herbert Selenge amekuja kukaa hapa kutoka Magila pamoja na Hugh Peter Kayamba na George Songolo na Mr. Wilde, wamekwenda Kiungani, na Mr. Wride kaenda zake Ulaya. Edward Nyongo na Richard Kambaku wamekuja huku Mkunazini kufanya kazi ya mabati, Barnaba Kiwisi na Kadu wamerudi Unguja kutoka barra. General Matthews kaenda Ulaya, Mhomed bin Seyidi yupo mahali pake.

Juma a tano ilikuja mvua nyingi sana, hatta usiku saa tissa umeme ukaja ukavunja kilele cha mnara wa Christ Church Mkunazini, yapata thiraa tatu na msalaba wake umeanguka chini, lakini haukuharibika. Usiku uleule nyumba moja ya Malindi imeanguka imeua mtu mmoja, tena upande wa Michonzani zimeangukwa nyumba mbili. S.U.

MSIMULIZI. 175

HABARI ZA MAGILA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu, kama katika mwezi wa March akaja yule Mdachi mkubwa wa Pangani na watu wengi wapata thalatha mia na Wadachi wangine, naye alikuwa akitoka kwa Semboja kule Mazinde na Vuga, wasikae mjini mwetu, wakatua mahali petu tunapocheza mpila wakajenga hema zao hapo, illa yule mkubwa wao akakaa mjini, akasema, kama yule Semboja amekubali kulipa mali yao alionyang'anya.

Tumefurahi sana kupata Kasisi mwingine hapa Mr. Dale. Pasaka hii Mr. Woodward akataka Wamasihya wote walio miji ya Upelekwa huko Bonde waje Magila, navyo vikatendeka, Wamasihya wengi wakaja. Siku ya Juma a mosi mbele ya Pasaka wakabatizwa watu kama wanane, wawili walikuwa wazee mume na mkewe. Mke akaitwa Elizabeth, mume Zakaria. Ilikuwa siku ya furaha sana kuwaona wale wazee wakibatizwa. Siku ya Juma a tatu baada ya Pasaka watoto wakapewa ruksa kwenda kwao kwa mda wa juma tatu, na mwalimu mkubwa Mr. Roberts amekwenda Mvita, akiweza apitie na Unguja kwa siku kuu zake, na Mr. Wilde amekwenda Unguja kupumzika, kwani hakuwa na afya njema hapa, na Dr. Castle amekuja Unguja kupata afya. H.P.K.

WONYESHANO WA KAZI, APRIL 17, 1890.

April 15, vitu vya killa mahali tukaapo hapa Unguja vililetwa vyote hapa Kiungani, na vitu vingine vya Mkuzi vililetwa pia. April 16, vitu vyalizidi kuja tu vitokavyo Mkunazini na Mbweni na vitu viwili vya Magila. Bassi ndipo vikawekwa Chuoni kwa uzuri na utaratibu, mikeka mingi ya kazi nayo yote ilitundikwa ukutani, na vitu vinginevyo vyote vyaliwekwa juu ya meza. Namna za vitu vilivyokuwapo ndivyo - vitu vilivyofanywa kwa

MSIMULIZI. 176

mibao, mabati, vitu vilivyoshonwa, kuandika sanamu, sanamu za rangi, karatasi zilizopigwa chapa, kupiga pasi nguo, vitu vya fetha ao shaba vilivyofuliwa, namna za vitu vilivyosukwa kwa ukindu ao uzi ao makuti, majahazi, mijeledi ya chukuti, namna ya darizi, mitego ya sanamu na mangineyo. Hatta alasiri panapo saa kumi likaja gari la frasi ndani yake mkewe barozi mkubwa, na barozi mdogo wa Mbweni Lieut. Smith na mkewe, wakaingia chuoni kuangalia vitu vya Wonyeshano, kuamua nani astahiliye kupewa zawadi kwa kitu alichokifanya, wakaangalia hatta jioni kabisa saa thenashara unussu wakaisha, wakaingia garini wakaenda zao. Lakini assubui ya siku ileile ya Juma a tano April 16, sisi tuliipamba nyumba yetu vizuri tayari kwa Alhamisi.

April 17, Siku ya Wonyeshano, assubui saa tatu unussu watoto wa Mkunazini wakaja hapa na Wazungu wao, saa nne tukapewa ruksa kwenda chuoni kuangalia jamii ya vitu vilivyokuwapo navyo jumla ya vitu vyote ni 600. Siku hiyo mvua ilikunya tangu assubui hatta jioni, bassi Wazungu, na watu na watoto wa Mbweni hawakuweza kuja mapema illa wakawasili hapa saa sita urobo na mvua yao, tena wakapewa ruksa kwenda chuoni kutazama namna za vilivyokusanyika. Saa saba chakula kikawekwa tayari, na siku hiyo tulicheza sana tinge. Panapo saa saba urobo tukapewa chakula chetu, kiisha tukawa katika machezo, na wengine kuzungumza na rafiki zao. Saa tisa unussu kengele ikapigwa, ya nini? Wote pia waliokusanyika hapa Kiungani waje ndani mstarini, Wazungu wakakaa vitini, ukaletwa mfuko mkubwa umejaa rupia 157. Bassi wao waliostahili kupewa zawadi kwa kazi zao kama waamuzi walivyoamua wakapewa. Ndio hawa: Mkeka wa kazi 1. Dora Ninga na Cpcilia Wavito. 2. Abigail Alizao, Bertha Feruzi na Agnes Sambutu. Msala, Clementina Laiti. Kasha la ubao, 1. Fabiano

MSIMULIZI. 177

Bwambwara. Chombo ao ngalawa &c. 1. Filipo Taruka, 2. Reginald Songolo. Kipakacha, ao kikapo, ao jamanda &c. 1. Isaac Kambazo, 2. Sheldon Mabruki. Namna nyingi za vijamanda &c. vikifanyizwa na mtu mmoja, 1. Giles Kushelwa, 2. Elvani Kachawa na Charles H. Simba. Kitanda, viii na Meza ndogo, 1. Yusuf Kijumbe. Kichezo chenye sauti, 1. Mbwana. Sanamu ya Merikebu ao Ohombo imeandikwa karatasini, 1. John Makunjila. Kazi ya Almaria ya Kanisani, 1. Rose Muriezai, 2. Emma Nyawela. Kitani chenye Almara ya kwa Kanisani, 1. Annie H. Songolo, 2. Keziah Shikalako. Kazi ya kushona 'Crewel work', 1. Rebeka Wajionaje na Rose Dunia, 2. Rose Dunia. Mbegu ao ushanga zilizotungwa kwa shingoni, 1. Hugh Mhina, 2. Orpa Sulia, 3. Yakobo Chorola, 4. Emily Mrashi. Nyuzi zilizosukwa kufanya 'Knitted rug,' 1. Charles Humfrey Simba. Flaneli iliyosukwa, 1. Sheldou Mabruki, 2. William Asilimali. Visibau vya kwapa, 1. Barnabas Farajallah, 2. Cyril Mabruki. Kisibau cheupe, 1. Cyprian Chitenje. Kofia nyeupe, 1. Jiles Kushelwa. Kifuniko cha kitandani ikishindaniwa na waanawake wazima, 1. Mary Hasina, 2. Lydia Sikujua. Vazi la kike ikishindaniwa, na waanawake wazima, 1. Bridget Matitu. Kazi ya kuinikia, kushona, kupiga darizi, kutia matata, 1. Lulu Masuke, 2. Eva Hasina. Vazi la kike likishindaniwa na watoto, 1. Charlotte Kabutu, 2. Elizabeth Ndilatu na Kandake Kabutu. Kofia na Mavazi ya Kiunguja, 1. Rebeka Wajionaje, 2. Emma Nyawela, Rose Muriezai na Eva Hasina. Kifuniko cha kitandani kikishindaniwa na watoto, 1. Hilary Kihinda, 2. 3rd. Class Mbweni. Mto wa kitanda, 1. Arthur Kasembe, 2. Day School Mkunazini na 5th. Class Mkunazini Choir School. Mfuko, 1. Liwago, 2. Mary Mkwea. ' Sanamu za rangi zilizoandikwa kwa kufikiri tu, 1. Hugh S. Mtoka, 2. John Matthew Mgonea. Tjpinde na mishale, Marko Mradi. Kambd, L Victor Magonga, 2.

MSIMULIZI 178

Kornelio Chonge.- Viatu vya Kizungu, Marko Njala. Kazi ya Bati, 1. Charles Masegwe, 2. Stefano Yehiwa. Kazi za kupiga chapa, 1. Gray Feruzi, 2. Daudi Kahambwa. Kutia vitabu jeldi, 1. Samuel W. Saadi, 2. Martin Zanga. Madema ya samaki. Yohana Chanamila na Hugh Mhina. Ufagio, Yohana Useni. Makondavi, 1. Monica wa Mkunazini, 2. Alice Faraji. Pepeo, 1. Paul Tuagonge, Theodore Mromo. Mijeledi ya chukuti, 1. Julius Mkwaya, 2. Charles J. Mkumbukwa. Kazi ya kutarizi, 1. Andrea Andani. Kata, Samuel Matthew. Kukutua shaba &c. Yohana Mnubi na James Juma. Kazi ya dobi, 1. Monica Hurumanani, 2. Alfaan Spkehola. Kazi za kushona "Cross Stitch," 1. Monica Hurumanani, 2. Kandake Kabutu. Kuimba kwa mtu peke yake, 1. John B. Mdoe, 2. Godfrey Mitimingi na Petro Kilekwa. Kuimba "Round", Watoto, edashara sawa sawa, na kuimba huku alikuamua bibi Balyozi. Mtg.

HABARI ZA KIUNGANI.

Feb. 7 Archdeacon Jones-Bateman alisafiri katika marikebu ya Admeli kwenda tembea na kubadili hewa, na Feb. 11 akarudi hapa.

Habari kidogo za Padre wetu Cecil Majaliwa, alitoka Unguja kwenda mji wake Chitangali Feb. 8, naye amewasili salama salimini huko aendako. Feb. 7, Sisi wote waana chuoni wa Kiungani tulifanyiwa Examination, naye aliyetazamia ni Archdeacon Jones-Bateman, Mr. Madan, Mr. Matthews, Mr. Bone na Mr. Viney, nayo ilichukuwa muda wa siku tatu, na mwalimu John B. Mdoe alitazamia darasa ya sita, na mwalimu Hugh S. Mtoka alitazamia darasa ya saba. Waalimu hawa Austini Mabruki, Daudi Machina, na Samwil Chiponde hawakuwamo katika Examination. Walioshinda ni hawa katika darasa ya kwanza, 1. Samuel Sehoza, 2. Hugh Mhina na Philip E. Yahom. Walioshinda katika darasa ya pili, 1. Wilfred Madudu, 2. Benedict Madalito. Darasa ya

MSIMULIZI. 179

tatu ni hawa, 1. Yustino Mkandu, 2. Grodfrey Mitimingi. Darasa ya nne, 1. Petro Mlanzi, 2. Amini Mvuma, darasa ya tano. 1. Daudi Wakati, 2. Mfalme. darasa ya sita 1. Danieli Abdallah, 2, Yohana W. Akupata; darasa ya saba, 1. Lukata, 2. Morisi Asani.

March 10, ndugu yetu mmoja amefarikia ugonjwa wa kitwa, ndiye Yohana Kimbilieni. Tena March 2, mwalimu John B. Mdoe na Hugh S. Mtoka walienda mjini kuwatazamia Examination watoto wa Miss Mills, muda wa siku mbili, nao walioshinda ni hawa; Katika darasa ya kwanza 1. Sheldon Mabruki, 2. Elvani Kachawa, darasa ya pili, 1. Yakobo 2. Alfred, darasa ya tatu, 1. Yustino, 2. Robert, darasa ya nne Kornelio, 2. Filipo, darasa ya tano, 1. Tomaso na Victor.

April 5, tukapamba nyumba yetu, na jioni tukaenda Mkunazini kwa sala ya jioni, wakabatizwa watoto watano wa hapa, Paolo Akilimali, Mikael Mwichande, Yohana W. Akupata, Marko Fikilahi, na Morisi Asani, kiisha tukarudi hapa. Siku kuu ya Pasaka April 6, assubui mapema tukaenda Mkunazini kwa sala kuu, na sala ya assubui, kiisha saa sita tukarudi. Juma a tatu tulikaa papa hapa sababu mvua. Siku ya Pasaka Henry Nasibu ameingia katika Chama cha Paolo Mtakatifu, nasi tumefurahiwa sana kwa ajili yake. April 15, Waalimu wote tulienda Mbweni majira ya usiku tukawasikiliza watoto wa Mbweni wanavyoimba, na tulipendezewa sana kwa kuimba kwao, na saa tatu tulirudi tukawasili hapa saa nne. Juma a nne pia tumekaa petu, balli saa nane tukaenda Mbweni, hatta saa edashara tukarudi. April 9, Juma a tano vilevile hatukwenda mahali, lakini saa saba unussu tulienda chuoni killa mtoto kupewa zawadi. April 12, Mr. Wilde na mwalimu Hugh Peter Kayamba, George Songolo, na Herbert Selenge, wamewasili Unguja wakitoka Bonde. Hugh Peter Kayamba, na George Songolo wapo hapa. April 21

MSIMULIZI. 180

tumewasafirisha ndugu zetu kwenda Nyassa, nao ni hawa Richard Kanyema, So Songolo, Clement Kathibeni, Philip E. Yahom, Anne Hathaway Songolo, na Clara Kanyema, jana wamelala ndani ya meli ya Seyid, leo April 22, wameng'oa nanga kwenda Nyassa.

April 24, Tumewasafirisha ndugu zetu wangine kwenda pande za Bonde, nao ni hawa: Martini Furahani R., Manfred Manyula, John Mdoe, na Mildred Furahani; wameingia ndani ya jahazi ya Kiunguja.

April 25, Siku kuu ya Marko Mwanjilisti tumeanza kutweka bandera yetu ya Koleji ya Andrea Mtakatifu.

April 28, Watu watano wameingia katika Waalimu ndio: Wilfred Madudu, Luke Chivoko, Arthur Kasembe, Leonard Mkwasomba na Sipriani Chitenji. Mtg.

HABARI ZA PWANI.

Vita ya Wadoicha yaendelea. Walipigana na Bwana Heri pande za Saadani, wakawa na mizinga sita, wakalivunja boma lake lenyi nguvu sana na watu wengi, wakatwaa kituo chake, mwenyewe akakimbia, wasimpate. Akafanya uthia vile vile, akazuia misafara ya biashara isifike pwani, nayo itokayo pwani isiende juu. Hatta Wadoicha wamechoka, wakapatana naye, sasa yuko Saadani tena mwenyi enzi za kadiri, sijui itakuwaje baadaye. Na maana ya Wadoicha kufanya haraka ya kumpatanisha, wamkumbuka yule Mzungu Enim Pasha, aliyekaa sana pande za Sudan, akaja pwani pamoja na Mr. Stanley karibu na Uganda? Bassi huyo alipofika pwana, alianguka chini dirishani, akaumia sana karibu kufa. Baada ya siku akaamka, akaja Unguja, akaheshimiwa sana na Sayidi Ali na Wadoicha pia, akapata afya yake. Hatta akasema, Sitaki mimi kwenda Ulaya. Nirudi kule kule barra ya juu. Wadoicha wakafurahi, siku hizi wamsafirisha, wampa killa kitu, kwani amekuwa kama mtu wao, ataka kueneza mamlaka ya Wadoicha pande za Victoria Nyanza. Bassi

MSIMULIZI. 181

kwa sababu ya misafara, ndio maana walimpatanisha Bwana Heri upesi.

Tena Wadoicha wameongezewa asikari wengi wa Misri, kama sita mia walikuja jahazini siku hizi. Sasa wanakwenda kupiga Kilwa na Lindi pia, kwani wa Lindi wamesema wataka vita. Twatumaini, wakipigwa, ndio itakuwa mwisho.

HABARI YA UGANDA.

Bwana Madan ameletewa barua hii ya Henry Wright Duta. Ilitoka Busambio, ndio upande wa kusini wa Victoria Nyanza, Jan. 5, Busambiro, Jan. 5, 1890.

My dear Rafiki yangu Mr. Madan, Salaam sana, na baada ya salaam, nakuarifu habari za kwetu Buganda. Mwenyiezi Muungu ametusaidia sana, tumepigana na wale adui zetu Waislamu, na Warabu twaliwashinda kabisa katika Oct. 12, 1889. Wakakimbia mbali inchi ya Unyoro na Sultani wao Kalema, bassi sisi Wamasihya twalimtwa Mfalme wetu yule wa kwanza Mwanga, tuliyemfukuza kwa ajili ya ubaya wake, amekwisha kuhitimu elimu na kuingia Umasihya; alisema, ametubu katika uovu wake. Bassi twalimrudisha katika ufalme wake.

Bassi Mwanga alisema, kwamba Muungu amekwisha kumwathibu, Hafanyi tena ubaya, anataka kuwa Mmasihya anataka Wazungu waje wengi kwake wafanye biashara, na Waalimu wengi waje wakae kwake wakawahubirie watu wake popote katika Buganda. Tena nakupasha habari ya kwamba, wakubwa wa Buganda wote Wamasihya watupu, tangu makathi, na waamuzi, na mawaziri wote wamepewa Wamasihya. Hatta mimi nimepewa ukubwa, Sultani wa kwetu akanichagua kumpeleka kwa Balozi Ingreza, kumletea barua zake zilizotoka kwa Mwanga Buganda nimekwisha

MSIMULIZI 182

kutoka Buganda, nakaa hapa Usambiro alipo Mackay, nangoja safari ya Mr. Stokes kuondoka, kwa sababu ameagizwa, amepewa ujira yeye Stokes kwa Mwanga, atulete mpaka kwa Balozi. Nitafurahi sana kuwakuta ninyi wazima, Wazungu wa Mission wote niwajua na watoto Wamasihya ndugu zangu wasalimie, nawasalimia sana sana, Inshallah nitawaona nikifika amani huko Zanzibar; na ndugu zangu ninaokuja nao wapata 40, na watafurahi kuona nyinyi rafiki zangu, na kuona Makanisa mapya yaliyojengwa siku hizi. Muungu akubarikie, akutunze dayima katika neema yake. Unisadiki mimi Rafiki yako akupendaye. Henry Wright Duta.

Lakini nimetumwa kwa Balozi, Wazungu watakaokubali kwenda Buganda.

Bassi tena tukasikia habari ya safari ya Mr. Stokes kama anakuja na karibu, na Henry W. Duta pamoja naye, tukathani marra tutaonana naye, tutasikia habari za ndugu zetu Wamasihya wa Uganda. Marra ikaja habari kusema, H. W. Duta amekwitwa kurudi upesi Uganda, kwani uthia uko wa Kamega, mfalme wa Wanyororo, sijui Waarabu wanamsayidia. Bassi ndugu yetu akarudi, tusipate kumwona.

Tena tumesikia, iliyo huzuni sana, kwani Bwana Mackay, mtu aliyekaa sana ajabu, yapata miaka arobatashara, Uganda na pande zake, akiwafundisha watu mambo ya Muungu, na kazi nyingi sana, kwani ni fundi wa kazi zote, hiyo Bwatia Mackay amefariki kwa homa kule kule Usambiro, kule alikofia Askofu wao Parker.

Lakini Askofu mngine amepatikana, jina lake Tucker, atakuja sasa hivi, ataka sana kwenda marra moja Uganda, kwani Wamasihya wa huko hawajapata kumwona Askofu hatta mmoja.

Askofu wetu hajambo, alikaa Rumi siku ya Pasaka. Sasa twathani amefika Ingereza. Twataka sana apumzike katika kazi zake nyingi, akapate nguvu ya kuturudia upesi.

MSIMULIZI. June, 1890. XI.

Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,

KATIKA "UNIVERSITIES' MISSION TO CENTRAL AFRICA."

HABARI YA PWANI.

Vita ya pwani kama imekwisha. Madachi walikwenda kupiga Kilwa na Lindi na Mikindani vile vile walivyosema, na manowari mbili tatu na jeshi kubwa kidogo. Manowari moja Ingereza ikafuatana nao kuwaokota Wahindi na Mabaniani walio chini ya hamaya ya Waingereza.

Madachi wakafika Kilwa kwanza, wakasema, "Labuda vita kubwa leo, kwani watu wa pwani watapigania mji huu." kumbe sivyo. Madachi walipiga mizinga ya merikebu kwanza usiku. Assubuhi wakashuka pwani wakauendea mji. Kumbe wote wamekimbia. Madachi wakaziteketeza nyumba za makuti tu, wakafanya boma wakakaa. Mabaniani wengi wanaurudia mji, kwani wamekimbizwa vilimani na wenyeji, wakaacha maduka yao; halafu wakapata kurudi wasitake kukaa mjini, wakapanda merikebuni mwa Ingereza, kama watu miteen na mizigo mengi, wakaja zao Unguja.

Hatta Lindi hakuna vita illa kidogo tu. Bassi Madachi wamekaa mijini mwote pwani, hakuna uthia. Wakubwa wa Lindi wamekubali maneno yao, nao majumbe ya pande zile, ndio tumesikia, kama Bondei. Watu, mizigo, barua, zote hupata njia sasa. Na Major Wissmann amerudi kwao kumpelekea mfalme wa Madachi habari ya vita yake.

Na sisi hapa Unguja tumeletewa habari kubwa kwa simu, kwani Waingereza na Madachi wamefanya maneno makubwa siku hizi kwao juu ya mambo ya Afrika, na zayidi upande huu wetu. Hatta wamepatana wakafanyiana maagano ya shuruti. Hivi. Waingereza walisema, "Pwani yenu, barra ya juu yenu. Unguja na Pemba kwetu, je?"

MSIMULIZI. 184

"Madachi wakakubali, Waingereza watengeneze mambo ya Unguja (na Pemba pia), kama kwanza, wasije kuja Madachi bado. Waingereza wakasema, "Twataka njia ya kupitia tangu Nyanza hatta Tanganyika, kwani hatta sasa twapita, twaitengeneza." Madachi wakakubali, "Hatuzuii. Tupite na sisi tu." Na vile vile njia toka Tanganyika hatta Victoria Nyanza.

Tena Waingereza wakasema "Mpaka wenu wa kaskazini toka Wanga pwani hatta Victoria Nyanza. Wataka inchi tena upande wa kaskazini? Madachi wakasema, "Hatutaki, wala Witu pwani, wala Uganda juu." Waingereza wakasema, "Vema." Ndio tumesikia, lakini hakika ya maneno tutapata zaidi halafu.

Tena maneno mengi yako Ulaya juu ya biashara ya watumwa na ya mvinyo mbaya, zipate kuzuiliwa. Lakini bado hayajaisha.

WARAKA WA ASKOFU MKUU.

Waraka wa Askofu Mkuu wa Kanterburi, kwa watu wanaosoma katika Kiungani Theological College, na kwa Chama cha Paolo Mt. katika kisiwa eha Unguja. Sisi tumestuka na kuajabu kwa kuletewa barua hii; tena twashukuru mno kuupata, kwani sisi hatukustahili tuandikiwe naye barua kwa mkono wake yeye.

Bassi sisi tunaona tumeheshimiwa sana. Tena maneno aliyotundikia naona hatutayasahau, kwa ginsi yapate kututia moyo tuzidi kuendelea mbele. Kwa hiyo barua hii tumeitundika Class Room kuwa ukumbusho wake, nayo imeandikwa kwa Kiingereza, lakini tafsiri yake kwa Kiswahili ni hii:

Jumba La Kiaskofu, Lambeth, (London) S.E. Juma a pili ya Mitende, 1890.

Kwa watu wanaosoma katika Kiungani Theological

MSIMULIZI. 185

College, na kwa Chama Cha Paolo Mt. katika kisiwa eha Unguja.
Waanangu wapenzi,

Nafurahi sana kusikia katika Archdeacon Jones-Bateman kama Chama chenu kina watu zayidi ya asharini, wazima na vijana, wanaotumaini kuonwa wastahilio, wakiisha kuwekwa tayari iwapasavyo, kuamriwa halafu kwa Ungoje mtakatifu wa Kanisa la Muungu.

Nastaajabu kusikia, hatta namshukuria sana hilo, kama mmoja wa waalimu Waafrika ameisha kufanywa Kasisi na mmoja Shemasi ya Isa Masiya, Mchungu mkuu na Mkohani mkuu wa kuungama kwetu. Naomba kwa moyo wangu wote kama Roho Mtakatifu aidirikishe kazi amini ya Askofu wenu na ya Kasisi awachungaye na ya Wangoje wangine na watii wakaaao nanyi, hatta halafu aufanyize akautunze akausitawishe Ungoje wa watu weusi, akawabariki wazae matunda mengi hatta mwisho wa ulimwengu.

Katika Afrika neno lile lililotabiriwa limeisha kutimizwa kama Kushi itahimiza mikono yake Muugu. Twamwomba awatimilizie mataifa yote neno la Nabii kama killa mahali itakuwapo sadaka safi ya rohoni, na kama atatwaa watu katika mataifa yote kuwa wakohani na walawi ndio Wangoje wa kweli wa Anjili.

Jambo hili lipate kutimizwa kwa kweli yatakiwa imani hayi na nia imara kwenu. Ndio hii Muungu anayowaitia ninyi kwa ufathili wake mmtolee, apate kutimiza nayo shauri lake yee. Nayo awatakiayo yu tayari sana kuwapa mkiutazama Msalaba wake Masiya.

Majaribu ni mengi nje, na moyo wa mtu ni thaifu, na shina la thambi laingia sana ndani. Lakini yee aweza kuwalinda katika majaribu, yee ni nguvu ya moyo

MSIMULIZI. 186

wenu, yee aweza kuingia sana mwenu kuliko thambi aing'oe kabisa. Msiache kabisa kukesha, msiache kabisa kuwa watu wa kuomba. Naye atawatia nguvu ya kuishinda saa ya kujaribiwa, atawafanya imara kung'oa killa lililo baya kati mwenu. Mbaraka wa Muungu, Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, uwajaze kwa moyo mkuu na furaha.

Mimi hapa Baba wenu wa kweli katika Masiya niwapendaye,
EDW. CANTUAR

HABARI ZA MSUMBA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu, nataka nikueleze habari ya kazi yetu hapa Msumba na Matope, sababu mwezi wa December nalikwenda Matope kuwatazama Waanafunzi waliopewa misalaba. Mr. Johnson alinipeleka niwafundishe Imani na mafundisho mengine. Bassi nalikwenda na watu wa hapa Msumba wakuvuta makasia ya mashua yetu kubwa sana hatta watu 20 huingia, na watu wanne wa pa Chisanga pia walifuatana nami, jumla tulikuwa watu kumi na mbili. Siku kuu ya Kuzaliwa Bwana wetu twalikuwa kwa mahali paitwapo Mlambuzi.

March 23, tangu kurudi Matope sina nguvu hatta kidogo na mke wangu hajambo, na mtoto wangu Emma Mary Ambali hana afya vema.

Hapa Msumba pazuri sana kwa kazi yetu, lakini miji mingine ina uthia sana kupita tangu kwa Makanjila hatta Lusefa miji hiyo hakupendi, sharti kuwa na bidii sana kuwaleta hapa.

Mashamba mengi hayana watu wakulima, walimaji ni wachache huku Nyassa. Hatta makasisi hatuna mengi sana na sasa Archdeacon Maples anakwenda Ulaya

MSIMULIZI. 187

mwaka huu, kwani mama yake hawezi, tena aenda apumuzike. Bassi tuna Kasisi mmoja tu, naye ana kazi nyingi sana, anatuangalia katika miji yetu sisi Waalimu tunamokaa.

Sijui kama mmesikia habari ya Kasisi wetu Mt. Johnson alikamatwa na Amdoka, ndio yaliyompata.

Katika miji yetu ya huku bara hii mji mkubwa ndio Msumba, na sasa Wangoni wanataka kuuharibu Msumba. Safari ya kwanza walikamatwa watu 50 wa Msumba na mwezi wa March 22, Juma a mosi wamekamatwa watu wanane, na mmoja kauawa. Bassi inchi hii haikai burre, siku zote vita, Amasanji na mke Wake amekamatwa na Wangoni. Daudi Benyamini ametoka Bandawe na mkewe wanakaa kwa Mkalawile.

Alipofika huko na "Steamer," wenyeji wakaja na mitumbwi yao kwenda kuwachokoza watu waliomo ndani ya "Steamer". Bassi Mr. Mills akatwaa kibunzi cha mhindi akatupa ndani ya mtumbwi, marra wenyi mitumbwi wakarudi pwani, wakawaarifu wenzao kama Mzungu ametupiga burre tu. Mashua ya "Steamer" yetu ikaenda pwani, marra hiyo washenzi wakaikamata na watu waliemo pia wakakamatwa, mtu mmoja akapiga kelele, Bwana tunakufa! marra akaja Mr. Johnson pamoja na Aruffo, kwani ndio desturi yake kushuka na mwalimu, na yule mwenyi kupiga kelele akajitupa majini akaogelea kwenda kwa "Steamer." Bassi Mr. Johnson na Aruffo wakakamatwa wakavuliwa nguo, walipata mashaka sana siku hiyo. Stefano Rehani amekufa ao amekamatwa hatujuwi, kwani tangu siku hiyo hajaonekana.

Waanafunzi walio watu wazima ni Akombe na Mawawa na hawa ni Waanafunzi wadogo, Mzinda, Mpila, Kalybzi, Chapuchapu, Paonanga, Wantuamwewa

MSIMULIZI. 188

ma Kangoma. Tena Mzinda anafundisha pamoja na Murphy Makamla, na Kangoma yumo katika "Steamer".

Wanaojifundisha kusoma sasa ni hawa; Achizui, Achikonda, Amakani, Amtepa, Hasani, Anyenje, Alijenjeru, Monyenje, Likwambe, Mpokonyoka na Katoma.

Tena watoto wawili wametoka chuoni lakini wanakuja kusoma, ndio, Nyefu na Mtambalika.

Hapa tuna Wamasihya wanne tu katika Mji huu wa Msumba, ndio, Ibrahimu Kulambilanja, Yakobo Talekatawene, Sulimani Matengeni na Petro Mtakula. A. A.

HABARI ZA KIUNGANI.

May 1, Tumepata watoto wawili wageni, lakini mmoja wao alikuwa mdogo sana amepelekwa Mkunazini, aliyesalia hapa jina lake Ngumbi. May 15, siku ya Kupaa hatukwenda popote. May 22, Mr. Wilde akaja pamoja na Bwana John Swedi kwani Mr. Wilde alikuwa hawezi, May 14, Bwana John Swedi alienda zake Mkuzi pamoja na mkewe na watoto wake wawili George J. Swedi, Willy J. Swedi.

May 26, Juma a tatu baada ya Pentekote tukaenda kushinda Mwera, mahali unapoingia mto chini ya inchi ukitokea Chukwani, pamoja na Archdeacon Jones-Bateman, Mr. Madan na Mr. Mallender, na kiongozi wetu ndiye Nicholas Faraji. Sisi watu wa Chama cha Paolo Mt. tumefurahi kwa Sipriani H. Chitenje ameingia Chama June 4.

Alituwasilia hapa Bwana Askofu wa Mombasa akawatia mikono watu 14, wa hapa Samuel Matthew, Petro Mlanzi, Frederick Makwela, Paolo Akilimali, Mikael Mwichande, Yohana W. Akupata, Marko Fikilahi, Morisi Asani; na watoto watatu wa Miss Mills, Elvani Kachawa, William Asilimali na Theodore Mromo, na wawili tena wa Mkunazini Yohana Mnubi na Danieli Abdallah, na watoto

MSIMULIZI 189

wanne wa Mbweni, Godfrey Hamisi, Yakobo Chaneema, Clementina Laiti na Adelaide Akulaiti.

Tena amekuja hapa Mzungu mgeni anaitwa Mr. Kick, naye anafanya kazi ya kupiga chapa.

SAFARI TANGU NEWALA HATTA KIUNGANI.

Bwana Porter na watoto wengi wa Newala tulitoka Newala kwenda Unguja, tukatoka kama saa tatu tukaenda hatta Mlolela, tulifika jioni wangine usiku. Asubui hatukutoka illa hutembea tu mjini. Alhamisi ukafanywa Usharika Mtakatifu, kama saa pili tukaenda hatta Mpatila tukalala, ha Mpatila ni jangwa kubwa hapana majani.

Jumaa tukalala Chidou, maji yake machafu, tulipotoka Juma a mosi hatta kwa Martin Liwengwa, Juma a pili ukafanywa Usharika Mtakatifu tena sala ya asubui, alasiri tukatoka hatta Lilonga tukalala. Juma a tatu tukaenda hatta kwa Selimu tukalala, Juma a nne tukaingia mashuani tukafika Lindi, askari wa Madachi wakatuuthi na mizigo yetu marra huchukua marra hutua marra kwenda marra hurudi, tukapewa kulala nyumbani kwa Mdachi, tukalala siku tano. Mdachi akatukaribisha vizuri sana kwa heshima sana. Askari siku zote wanachukua mawe na chokaa wajenga ukuta.

Juma a tatu tukapakiwa merikebuni tukalala siku moja baharini, ya pili yake tumefika kwetu Kiungani. C. M.

Tumefurahi sana kuona ginsi watoto wengi wa miji yetu ya Upelekwa wanavyokuja hapa Kiungani kuzidi kupata mafundisho, na kutazamia kuwa Waalimu baadaye. Mtg.

HABARI ZA MLOLELA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu sina habari nyingi zayidi, illa habari zetu zayidi

MSIMULIZI 190

ni kushukuru Wamasihiya na Waanafunzi wamenipa maneno haya. Kwa rehema za Muungu twathubutu kusema, sisi Muungu ametupenda tumepata mji wetu tunda la kwanza la Kasisi mweusi. Siku aliyowasili hapa akitoka Unguja tulifurahi sana, sisi twamshukuru Muungu ametuacha tukae gizani kwanza, hatta sasa ametupa Mchungu tupate kuona na kumtumikia Muungu wetu, hii ndio bahati yetu tuliyowekewa. Twamshukuru sana Muungu kwa yote.

Alipofika Bwana Gecil kwa furaha tulipiga bunduki. Habari za Siku kuu ya Pasaka Juma a mosi mbele ya Pasaka tulitengeneza Kanisa letu kupamba maua, jioni walibatizwa watoto wawili Wamasihiya baba na mama, majina yao Yona Sikumbili na Debora. Bassi watoto majina yao Daniel, Yona na Neema Akanilaga. Alfajiri tuliondoka tukaimba kwa furaha saa ya kwanza kengele lilipigwa sana, ilionekana vizuri killa njia inatokea Mmasihiya na Mwanafunzi, tukaingia kanisani. Tukaanza kuimba nyimbo za kumsifu Muungu, ikaanza Taratibu ya Usharika Mtakatifu tukajibu kwa kuimba vizuri sana, watu walioshariki 28, wangine hawakuwa tayari kwa kushariki.

Saa tatu u nussu ikapigwa kengele ya Wamasihiya, Mwalimu Harry akawahubiria kwa Kiyao, saa nne ikapigwa kengele yetu ya sala ya Assubui, Wamasihiya na Waanafunzi tukaja kanisani tukamsifu Muungu; halafu Bwana Cecil mwenyewe akatuhubiria habari za kufufuka kwa Bwana wetu.

Tulipotoka Wamasihiya na Waanafunzi wakapewa nyama na mchele wote, watoto wanaokuja kwa kusoma wakapewa nguo wote waume na waanawake. Juma a tatu watoto wote wa hapa walikwenda Newala, na watoto wetu wanaosoma Newala walikuja hapa kuwatazama wazee wao.

MSIMULIZI 191

Juma a nne Harry na mkewe akaenda zake Masasi, Alhamisi watu wa hapa na Barnaba Nakam na mimi tulikwenda kuwinda. April 13, watu wakaleta malimbuko ya mavuno yao Kanisani kumshukuru Muungu aliyetupa mvua.

Uthia wa Lindi unazidi, tena watu hawawezi kwenda Lindi kuchukua mizigo. Tena njia hapana, kwani raiya wa mfalme Machemba amenyang'anya mizigo ya Newala sababu yake hatujui, amenyang'anya akisema, Sitwai mizigo hii kwa sababu nataka vita la! lakini watu wangu amenitwalia Chiwaula hataki kunipa, bassi nimeona nikitwaa mizigo hii ya Mzungu watu wangu watanipa sababu watamwogopa Mzungu. Bassi watu wakarudi hapa pasipo mizigo.

Ndugu zetu, tutasema tena marra moja, twasema kama Chitangali mwalimu mmoja ao wawili hawatoshi kabisa, watoto wanaokuja kusoma waume 42, waanawake 32, mwalimu nani kwa hawa wote? M. H.

Siku hizi ametufikia hapa Kiungani Bwana Porter pamoja na watoto thenashara, bassi ametupa habari za Mlolela akaapo Padre wetu Cecil, na tumesikia hivi:

Siku moja alifika Mlolela akashinda huko siku nzima, aliona kama mji unaendelea vema sana, na watu wote humheshimu Bwana Cecil, na ginsi anavyofanikiwa. Tena majengo ya hapo mazuri sana ya nyumba na kanisa pia, hatta hili kanisa limejengwa kwa fetha za watu wa Mlolela, hatta watu hutenda kazi yoyote na wapatapo mali huitendea kwa kazi ya kanisa lao kununulia mafuta ya taa za kanisani.

Tena jambo la kuangaliwa zayidi ndio utaona watu ginsi wanavyokuja kanisani kuabudu killa siku wala siyo katika Juma a pili tu, bassi kwa jambo hili naona watawawekea

MSIMULIZI 192

wangineo namna njema wawafuate kutenda vile. '

Kama ukienda Mlolela utaona mji ni safi umetengenezwa vizuri kwa amri ya Barnaba Nakam wala si kama pengine pengine. Jambo lingine tena utaona Wafalme wa pale na watu wao ginsi wanavyovaa nguo safi na nzuri, hatta na bunduki na selaha zao pia ni safi. Waume wengi wanajua Kiswahili sababu hufika Lindi kwa kuchukua mizigo, lakini waanake wanajua kidogo sana. Kwa sababu hiyo ni vigumu kuwafundisha wajue habari za Muungu mbele ya kuwafanya Waanafunzi. Pengine waume na wake huja kusema kama ni tayari kwa kubatizwa na wameacha yote mengineo, lakini wasijue nini amri za Kanisa la Muungu zimipasazo killa Mmasihiya kwa ginsi wanavyoiga matendo ya pale Mlolela. Mtg.

HABARI ZA MKUNAZINI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuletea habari kidogo, kama hatuna daktari hapa, kwani Miss Shaw alikuwa hawezi naye amesafiri Ulaya pamoja na Miss Townshend, na daktari Charlesworth pia amesafiri, John Edward Makunjila ndiye daktari wetu sasa, Meli hii ya Ulaya amekuja Mzungu mmoja anakaa hapa jina lake Mr. Faulkner, anamsayidia Mr. Beetham. Alban Sekehola siku hizi karibu anakuwa fundi na kutoka katika uwanafunzi, sasa anachuma. Mnara wa Christ Church kanisa letu uliyovunjika kilele chake sasa unatengenezwa, wanafunga majukwaa kwanza. Tena nyumba ya Seyid ya darajani imeanguka imewaumiza watu kathawakatha. Juhe 25, nyumba ya fortha ya Mdachi ilianguka upande mmoja ikauwa watu watatu, mmoja tena amejeruhi tu lakini mzima.

Watu jeuri na wabaya walimwingilia Baniani mmoja wakamua burre. S.U.

HABARI ZA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi, salamu. Mnamo mwezi wa May 6 ilikuwa harusi ya Mwalimu Sugh P. Kayamba na Faith Kayamba.

Siku kuu ya Barnaba Mt. saa 9 tulienda Njia kuu kujifurahisha. Na tena jioni ya Juma a pili 15 June ilikuwa Ubatizo wa Watoto, nao ndio hawa, Saura Masilamu, Stella Chatangu, Winifreda Kamwana, Irene Akwangwara, watoto wa Mission. June 17, Bwana mmoja akaja afanye kazi yake Kibandani, Sermala, ndiye Mr. Brough. R.M.

HABARI ZA NEWALA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu, nataka kukueleza habari kidogo. Bwana Hainsworth na Mr. Watson wakaenda Rovuma pamoja nao watoto wawili, wakalala siku tatu wakarudi hawakupata kitu. Mwalimu Yohana alikuja hapa na Watoto wa Chitangali, mmoja anakaa hapa kujifunza kusoma jina lake Francis Sapuli. Bwana Sinith alikuja hapa na mtoto mmoja wa Masasi jina lake Austini Namwejeka, bassi Waliposikia nduguze wakaja wakamtorosha ukawa uthia sana. Bwana Smith akataka kumchukua mtoto wakamkataza wakatwaa bunduki zao, wakawa tayari mmoja na kisu chake wakaweka tayari, tena akaja mtoto akamwita Bwana Porter, kwani twalikuwa kanisani. Bassi Bwana Hainsworth tu akasalisha, kwani tumepata makasisi wawili. Tulipotoka kanisani tukaenda mezani. Wakatwaa chakula chao wakawapelekea huko huko walikokaa, na chakula cha mtoto pia, wakamtafuta mfalme mzee Matola hakumwona alikwenda kwa Mpepe naye mfalme mdogo lakini, akarudi usiku. Bwana Porter na Mr. Smith wakarudi, wale asubui wakaenda zao na mtoto. Waalimu wawili Daudi na Samwil wamekwenda Kiungani na watoto kumi nao. Juma a nne hatukusoma twaliwasindikiza.

MSIMULIZI 194

HABARI ZA MASASI.

Salamu, baada ya salamu nawaarifu habari zangu. Tuna huzuni sana kwani Wamasihya waliotengwa katika kanisa sababu ya kuoja wake wawili, tena wangine karibu watabatizwa. Watoto wa serkali yetu ya Masasi wengi sana wanatoka sijui sababu yenyewe naona kudanganywa na mama zao waende kuoja. Tena wagonjwa wengi walikuwa hawawezi siku nyingi sana, mmoja naona mtamjua, alikuja zamani huko Unguja, jina lake Isaya Nauganje na watoto wangine pia siwezi kuwataja majina yao maana hamuwajui.

Lakini tena nitawaambia watoto waliojiweka tayari kwa Ubatizo majina yao, Mtumbela, Mtukananje, Salehe, Arruli, Simana, wa serkalini hawa, wa nje siwezi kuwaambieni maana wangine hawajulikani majina yao. Tena Kanisa letu wanaanza kujenga kuta za miti. Twafurahiwa sana mfalme mmoja ajaribu sana kuja Juma a pili siku kwa siku pamoja na watu wake, jina lake Chiwalo, kwani kusema hivyo maana shidda sana wafalme wa huku kwetu kuja kujifunza maneno ya Muungu, illa huyu tu. Ndiyo maana watoto wengi hawaendi Unguja kusoma hawapewi ruksa, kwani hawana nguvu kusema iliyo ya haki, mtoto asipopewa ruksa na mamaye, wala mfalme hawezi kuamuru mtoto aende mahali, tena tamaa imewashika, hiyo hawawezi kuendelea katika mambo mengine.

Mwalimu Paul Kasese alikwenda awinde baada ya siku kuu ya Pasaka, hakupata kitu. Bassi. Gl. M.

HABARI ZA SHAMBA LA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu habari hizi kidogo tu. Wakumbuka kama April 24 alipokwisha, safiri mwalimu Martini Furahani kwenda Bonde, hapakuwa na mwalimu

MSIMULIZI 195

wa kumsayidia Mr. Key kwa kuhubiri killa Juma a pili, kwani Mr. Key jioni huenda mjini kwa sala ya Kiingereza na kuhubiri pia. Bassi Hugh P. Kayamba alikuwa akija Mbweni kusalisha, halafu hurudi Kiungani.

Mwezi wa May 6 ikawa harusi yake Hugh P. Kayamba. Siku hizi Prancis Mabruki ametoka Mbweni amesafiri Mvita, anafanya kazi katika British Company.

May 12, alitokea mtu mgonjwa sana ana pingu zake, naye mzee sana, alitaka msaada. Wazungu wakamhurumia wakamfungua pingu zake, wakampa dawa. Akaenda zake kwa shuruti, kwani hakukubali kwenda zake akaogopa kama atafungwa tena.

Wamkumbuka kama mtoto yule aliyeokotwa na Nicholas Nailua, bassi siku moja alienda mjini Juma a mosi kuchukua mizigo. Marra akatokea bwana wake akasema, Mtoto huyu amenipotea tangu alipokufa Seyid Khalifa, bassi akaambiwa amchukue.

Siku ya Filipo na Yakobo Mitume, watoto wa school ya shamba walitaka kwenda kushinda Buyu, lakini hawakuenda sababu ya mvua nyingi. Juma a nne baada ya Pentekote watoto wa shamba walienda Buyu pamoja na Bwana Mr. Key na mwalimu wao Nicholas Faraji.

June 7, Juma a mosi ilikuwa siku njema sana sababu waliorudi wenzetu waliosafiri Masai ndio hawa, Selemani Mtwana, Timoteo Komba, Palmer Majaliwa, Pilipo Mpande, Hugh Kambena, Edward Juma, Liponje, Musa, Mabruki, Diva Dimwende.

June 20, twasikitika sana, kwani mwenzetu amefariki jina lake Kamua, naye bado kubatizwa. N. F.

HABARI ZA NYASSA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu ginsi tulivyokuja zetu Unguja baada ya

MSIMULIZI. 196

kukaa miaka minne huko Nyassa. Naliingia jahazini "Charles Janson" May 2, pamoja na watoto 13 wa pande za Nyassa; bassi watoto wenyewe walikuwa wa Likoma 3, wa Monkey Bay 1, wa Pachiya 3; wa Msumba 6. Twalitumainia kuja sisi sote hatta hapa Kiungani, lakini tulipofika Blantyre tukasikia kama hapana meli siku hizi ya kwenda Unguja: habari hizo zikatusikitisha sana, lakini shauri jingine hapana isipokuwa hilo la kurudisha watoto wote 13 Likoma walipokwisha kufuatana nami hatta kwa Katunga na kutazama jahazi ile kubwa "James Stevenson."

Bassi katika safari yetu katika "Charles Janson" twaliingia katika miji yote ya Wanyanja wanapokaa waalimu wetu, tena tukafurahi sana kuona ginsi kazi yao ilivyoneemeshwa naye Muungu. Tena tukashinda usiku moja Juma a pili pa Msumba, na siku ile ile watu wote wa mji ule walikuwa wakiona khofu sana kwa sababu ya Magwangwara wa Mhaluli waliokuwa wakiwaletea vita watu wa Msumba; bassi Magwangwara hawakuweza kuvunja mji wala kuua watu; wakaenda zao: alasiri watu wakaiacha hofu yao, wakatulia.

Bassi kule kule Msumba twalipata habari za kweli za mwenzetu Stefano Rehani, kama ameuawa kwa amri ya Mkaliwili mwenyi mji ule ule alipokamatwa yeye na alipouthika Bwana Johnson. Bassi tulipopata habari hizo tukania tusiende mjini mwake wala kumwamkia wala kuonana naye siku hizi wala kupeleka jahazi bandarini mwake hatta tutakaposikia kama habari zake ni njema na za watu wake.

Bassi uthia ule ule wa mji ule na wa miji yote ya Wayao kando la Nyassa kwa mashirikiki ni kwa sababu ya Wareno walioua watu kwa Mataka mwaka jana: habari zile hatunazo zote, lakini tunajua kama Wareno wawili na watu wao wengi sana wakaenda kwa Mataka wakapigana nao wakaua watu

MSIMULIZI. 197

wengi, na wenyewe wote wawili wakauawa, na Wayao wa mji ule na wa miji mingine wanakasirika sana, wala hawataki tena kupambanua Wazungu na Wazungu; wanasema "bassi tupate kisasi tu juu ya Wazungu wote, ajapo Waingreza ajapo Wareno, ajapo Wadachi." Bassi hatta roho zao zitakapotulia jahazi yetu Charles Janson haiwezi kwenda kutia nanga kwa salama karibu na miji ile ile ya Wayao.

Bassi tulipoagana na Augustine na Murphy na Wamasihya wangine wa Msumba, tukatweka tukavuka Nyanja tukatia nanga kwa Kazembe Sultani mkubwa aliyekwisha kukubali bandera ya Serikali ya Kiingereza pamoja na Jumbe wa Kotakota: yeye Kazembe aliniambia maneno mengi ginsi Makanjila alivyojaribu kumshawishi kuacha maagano yake nao Waingreza na kufuata Wareno; naye akamwandikia Balozi H. H. Johnston nyaraka za kuomba taraza ya bandera ya "Queen" taraza yenyewe, maana yake, baruti na bunduki, apate kuiangalia sana bandera hiyo na kushinda adui zake zote. Kule kule kwa Kazembe nalikutana nao vijana watatu waliofundishwa naswi Masasi zamani sana walipokuwa watoto wadogo sana, na hawa vijana bado hawajasahau maneno yote waliyofundishwa, lakini hawakubatzwa, wakasoma kidogo kidogo tu bass.

Hatta tukatweka tena, tukaenda zetu Monkey Bay tukaona nyumba inayojengwa huko nao "African Lakes Company" na watu wa mfalme wa mji ule wakaja kwangu kuhubiriwa ha kufundishwa. Tukashinda siku moja kule kule, tukaingia mtoni, tukaja zetu kwa Mponda ndipo tulipoonana nao Padre wale waliokwitwa "Peres Blancs." Padre wenyewe walikuwa Wafransa wala hawakuweza kusema neno moja lisilokuwa la Kifransa: wamejenga nyumba yao mjini mwake Mponda aliyewakaribisha vema.

MSIMULIZI. 198

tukawapa kitabu kimoja: vitu vyao vyote vimeibiwa njiani, makasha, barua, chakula - vitu vyote pia; hatta kitu kimoja hakikupona. Bassi Padre hawa wakaniuliza mambo mengi sana ya Mission yetu na ya Missions zote zilizoko kando la Nyassa, nasi twaliwapashia habari ginsi tulivyoweza. Bassi tukaagana nao, tukatweka tena, twaliingia katika miji mingine mingine ya Wayao na ya Wanyanja hatta tulipofika kwa Msapa ilipokwama jahazi mwaka juzi: hapo tukakutana nao waanafunzi walioshika sana kukumbuka maneno yote waliyofundishwa mwaka ule ule; na kwa maulizo yetu ya katika mambo ya dini wakatoa majibu yaliyo bora, nasi tukastaajabu sana kuona na kusikia ginsi walivyokuwa wakinia kushika sana mafundisho yale waliyoyapokea kwa makanwa ya Bwana Johnson na waalimu mwaka jana.

Bassi tulipotweka tena tukaamkia Wayao wangine na miji mingine, tukatafuta waanafunzi na wasikiao (hearers) hatta tukafika kwa Matope, ndipo mwisho wa safari yetu sisi katika Charles Janson. Bassi katika May 18 nikaagana nao Denys na watoto wale kwa Katunga, nikaja zangu hatta kufika tena papa hapa Kiungani. C.M.

HABARI ZA MAGILA.

Kitendawili! Tega. Sungura wetu anapata usingizi mtamu.

HABARI ZA MISOZWE. Kitendawili! Tega. Nazi zetu makoroma tu.

HABARI ZA MSAAKA NA UMBA, Kitendawili! Tega. Maji yetu yamemwagika njiani.

HABARI ZA MKUZI. Kitendawili! Tega. Bibi wetu amevaa shela.

MSIMULIZI. August, 1890. XII.

Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,

KATIKA "UNIVERSITIES' MISSION TO CENTRAL AFRICA."

VITENDAWILI.

Mwezi wa June tulitegea wenzetu wa Bonde vitendawili, kwani habari zao hazikuja upesi kutiwa katika Msimulizi hatta ajabu ginsi walivyoamshwa navyo, hatta habari zimekuja chungu chungu hatta hatuna nafasi za kuzipiga chapa zote!

Bassi vitendawili hutumilisha watu akili zao, hatta sasa twatega viwili, viende killa aendako Msimulizi, na tunaahidi kama mtu mweusi wa kwanza aletaye majibu ya kweli kwa Mtengenezi mbele ya Jan. 1, 1891, atapata Msimulizi wake burre pasipo kulipa kwa mwaka wote 1891. Lakini sharti asisayidiwe na Mzungu, kwani wao wenyi funguo nyingi hatta kitendawili huweza pangine kukifungua upesi!

1. Kitendawili cha kwanza: "Mimi mwalimu mweusi, kipofu tena bubwi nafundisha wenzangu.

2. Kitendawili cha pili: "Wazee wangu Tembo na Chuma, nyumba yangu ngozi." Mtg.

KUFUNGULIA WALIOFUNGWA.

Twakumbuka marhemu Seyidi Khalifa alivyotangaza habari ya uhuru kwa watu wengi, watakaofikia ufalme wake. Bassi na huyu Seyidi Ali, yeye pia siku hizi amezidi kupiga mbiu kubwa sana kwa jambo lilo hilo. Hati yake ikapigwa chapa huku Kiungani, ikatiwa mlangoni pa jumba la Seyidi na forthani na pangine. Na amri yake ndiyo hii, biashara yote ya utumwa ikome pia katika ufalme wake tangu panapo Aug. 1 iliyopita; nyumba za mjini ifanyikapo biashara hii zifungwe zote;

MSIMULIZI. 200

waliopo utumwani wakae utumwani, hao tu; mtu wo wote aliye rayia ya Ingereza ama amewekwa huru kwa Barozi asiwe na mtumwa wo wote; hatta mtumwa akitaka kujikomboa kwa fetha, aruhusiwe; ao akitendewa makali na ukorofi, bwana wake aathibishwe; mwenyi watumwa akifariki, asiye na mwana halali halisi wa kuwarithi, watumwa wote wawekwe huru: bwana na mtumwa aamuliwe na kathi sawa sawa; na vingine. Pana watu walikasirika, wakathubutu kuiondosha hati, na kuipasua. Wakakamatwa, Seyidi akataka kuwakata mikono, Barozi akasema, Wamestahili lakini afathali wapigwe wakafungwe. Wakapigwa sana.

Bassi tufurahi tukashukuru, kwani watu sio vitu, na waana Adamu wote mbegu moja, wote wenyi heshima yao, nao walio wajinga na wanyonge pia. Siku hizi ulimwengu haukubali mtu amwonee mtu mwenzake burre. Killa mtu haki yake, mali yake, mke wake, heshima yake, wala asitwaliwe burre. Hatta Afrika pia itapata siku zake.

HABARI ZA NYASSA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Katika Msimulizi wa mwisho naona mna habari kidogo za mtoto, jina lake Yakobo Zebedayo, ndio Masengu.

Na sasa nataka kukupasha habari za shemegi yake, jina lake Musa Kalulu. Baada ya kufa yee Yakobo huyu Musa akawa hawezi sana tumbo (typhoid fever) akapata maumivu mengi katika ugonjwa wake. Kwani siku moja usiku alijijeruhi mwenyewe kwa kisu, karibu na kitovu. Bassi kwa hivyo na kwa ugonjwa ule ginsi unavyozidi, akafariki panapo Feb. 8, 1890, kama 11.45.; a. m. Juma a mosi. (Na wakati huu S. S. "Charles Janson" iko pande za chini huko).

Panapo feb. 9. waanafunzi wakapewa misalaba, kama

MSIMULIZI 201

sitashara. Panapo Feb. 19, mwivi akaja (jina lake Kanjeyule aliyepasi kwa kuiba) akaiba sahani, kasha la baba Rev. W. P. Johnson, na vitu vingine vingi, akaenda navyo. Hatta leo hivi havionekani tena. (naswi twamvizia huyu Kanje; siku ya kumwona tu usiku ndio mauti yake).

Bassi hivyo siku zikipita S. S. "Charles Janson" ikaja, ndipo panapo March 1. 1890. Vitu si vingi, haba tu, habari zingine za huzuni, ndio ndugu yetu Stefano Rehani amekamatwa, amefungwa, (yule yule aliyekuwa mpishi kwanza, ndipo kutoka upishini akaingia katika stima). Habari ni hizi stima kutoka hapa kwenda kwa miji ya waalimu na kutembea kama siku zote, panapo Pachia akamtwaa mwalimu mmoja Aruffo aende na stima pande za Matope. Yeye mwalimu, kazi yake kuwafundisha wale wafanyao kazi mle na kuwasalisha, assubui na jioni; kwani wamo waanafunzi. Bassi stima ikatoka hapo pa Msumba, ndipo kushuka pande za chini. Hatta wakafika hapo Panaapanje pa Mdoka (ao Mkarawile, ni mmoja), naye baba Rev. W. P. Johnson amezoea tangu zamani kushuka humu. Bassi leo hivi pasipo shaka akashuka vile vile kwenda kunena na ni falme Mdoka na kunena maneno ya Anjili pia. Na wakati huu waliposhuka hawa, stima ilikuwa haijatia nanga, ilikuwa ikitafuta mahali. Bassi wakaja watu wa pale wenyi biashara yao katika mitumbwi. Walipofika jahazini, nahotha akawaambia, "Ee masheki, tokani! Jahazi bado kutia nanga." Illakini wale wakafanya ukaidi tu, akawaambia tena, "Tokani" Hawasikii, bassi, akatwaa kibunjo cha mhindi na kuwatupia, kikampiga mtoto wa mfumu. Bassi marra wakarudi pwani, wakafanya mashauri yao mabaya, marra wakaenda kwenyi mashua, wakanyang'anya chumvi, waliyokuwa mabaharia wakinunulia kuni. Marra pakawa chafuko kubwa sana, "Haya! waueni!. wachinjeni!" Wangine wakaitwaa

MSIMULIZI. 202

mashua, wanaipandisha mjini, baharia wengine wakazama majini, na wengine wakakamatwa, uthia tu. Hatta watu wengine wakamwangusha Yohana, Mmasihiya, wa Pachia, (labda) kutaka kumchinja, marra akaona Bwana Johnson, akaenda kwa kassi akawapiga mateke, wakakimbia wakamwacha, akaenda zake jahazini. Na wakati huu wote bwana na Aruffo wamekwisha kunyang'anywa nguo zao zote. Bwana wamemwachia nguo moja na viatu tu, bassi Aruffo hana kitu, uchi tu. Bassi, bwana, uthia tu. Watu wengine wa huruma wanaanza kuwaonea akina Aruffo huruma, hatta wakataka kumpa chiondo (nguo ya mti) avae, marra akaja mtu na mtumbwi wake akampakia Aruffo akampeleka jahazini. Bassi sasa kule pwani amesalia bwana na huyo Stefano, naye hajulikani huko alikochukuliwa, kwani bwana hakuwa karibu. Bassi wale wabaya wakamsumbua, bwana weee, wamvute huku, wamsukume huku, yee kujaribu kunyamazisha, asipate, lakini wapi, bwana? pa burre tu. Nguo zikaletwa kwa kumlipa huyo mtoto aliyeguswa na chibunjo, lakini wapi? yote burre. Aulize, lakini wapi? wengine "Mueni," wengine "mfungeni," wengine hivi, uthia tu huko pwani.

Bassi tangu (kama) saa kumi (4.0. p.m.) hatta saa tatu za usiku (9.0. p.m.), ndipo kuonekana baba Rev. W. P. Johnson anakuja peke yake katika mtumbwi mbovu peke yake anavuta, hana msayidia, akafika jahazini, ule mtumbwi akauacha uende pwani, kwani ilikuwa usiku, giza, baridi inavuma kidogo. Alipofika jahazini akauliza, "Nani yuko pwani." Wakajibu "Stefano bado kufika." Akawauliza watu wa pwani wabaya wale, wakasema, "Hakuna." Akasema, "Mleteni hapa." Wakakataa, wakasema, "Hayuko."

Bassi wakatoka usiku ule ule wakaja zao Livingstonia,

MSIMULIZI. 203

assubui wakatoka, (Na yote yale ya pa Mdoka hayangalifanyika mambo hayo, isipokuwa fitina ya kwa Makanjila wa huko karibu na pande za Newala na Mponda wa pande hizo, ndio waliopeleka wajumbe kwa Wayao wenzao, kusema, killa mwonapo Mzungu tu mchinjeni, msimwache. Hatta twalisikia kama Wazungu wawili, Wareno nao, wameuawa kwa Mponda wa huko polini). Wakafika bahari Malombe, wakasakama, sababu maji haba, kwani bahari hii ina matope mengi kuliko maji. Wakalala, assubui wakatoka, wakaendelea hatta mlangoni mwa mto Shire, wakasakama tena. Wakalala, assubui wakatoka wakaendelea mpaka pale pa Nstapa, tulipokaa sisi kale. Wakangoja mashua kuja, ikaja wakapakia jahazini, wakashika njia ya kurudi huku juu.

Walipofika mlangoni mwa bahari hii wakaenda kwa Abdallah na kumwagiza ya kuwa pa Mdoka tumefanyiwa uthia sana, na ya kuwa mashua yetu na mtu wetu wametwaa. Bassi yee akasema atasayidia sana kujaribu kuvirudisha, bwana akasema, ahsante, akampa zawadi. Bassi wakashika njia ya kuja zao; wakaja hapa petu, tuliposikia habari hizi tukawa na huzuni sana sana, na tukashukuru kwa kumpata baba yetu Rev. W. P. Johnson.

HABARI ZA LIKOMA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Baada ya kupata habari hizi bassi tukakaa. Habari zile za kale za Wareno, kama mjuavyo, hapana vita tena, jemadari amerudi kwao: na sasa tunataka sana kupata habari ya kuwa ilipo meli ya kwenda pande za Unguja; tutafurahi sana, kwani akina bwana wengine. wataka kuja pande za huko kwetu. March 5 stima yetu yatoka kwenda chini. Huku nyuma habari ni hizi. Huko Kumanda ndio mahali pande za ng'ambo, kama saa mbili tatu kutoka pa Kobwe pa

MSIMULIZI. 204

Chiteji, kumetokea hatari ya simba. Bassi akaua watu kumi ao edashara, mmoja akamrarua tu na madonda akamwachia. Siku hizi twasikia kidogo tu lakini yupo papo hapo, kwani watu hawawezi kulima mashamba hatta jioni, kwani huyo simba yupo. Panapo saa kenda ao kumi watu wamekwisha funga milango kabisa; ndio habari.

Stima leo March 22 yafika yenyi mizigo tele, na barua za Unguja zipo tele: baba Rev. W. P. Johnson asalia pande za chini. Pande zile aliko Stefano, haikupita safari hii, kwani yule Abdallah aliwaambia wakakae kama siku arobatashara, ndipo waende kwake, labda atamkuta, pamoja na mashua. Ndio maana wakupita upande.

Stima yatoka leo March 27, kwenda pande za chini. Huku nyuma Delta-metal Stima "Charlotte" panapo March 27 nayo ikaenda Bandawe pamoja na Denys. Yee akaenda kutazama kwa Chinteji mfumu wao Chigoo, inchi ya Watonga ao Wankamanga; kwani hawakuenenda Bandawe halisi illa huko Kuchinteji. Panapo ya 30 wakarudi wote pamoja na mtoto wa chuoni humu, jina lake George Mahumela, aliyepata ruhusa ya kwenda kumtazama mamake. Wakarudi tena na mwanamke wa chuoni, jina Mary Anchoni anayoposwa na Charles Nasibu mtu wa Mbweni; labda panapo Apr. 22 atamwoa. Ndio habari zetu.

Panapo Apr. 3, stima yarudi kutoka pande za chini, pamoja na waalimu wote kabisa kwa Ijumaa kuu na siku kuu ya Pasaka. Illa Paul W. Mambo tu, kwani jahazi haikupita pake, lakini atakwenda kutwaliwa.

Stima "Charles Janson" ilikuja na vitu vingi safari hii: lakini ilikuja tena na habari za huzuni, ndio hii. Yule ndugu yetu Stefano ameuawa amekufa. Habari ni hizi, kwani haijulikani vema. Bwana alikwenda kwa yule Abdallah akamuliza "Jee habari?" Akasema, alikwenda;

MSIMULIZI. 205

alipofika akaambiwa amekufa kwa maji, alitaka kuogelea hatta kwa Stima, lakini hakuweza, panapo siku ile ile. Lakini watu wangine wa Pachia, hapa akaapo Eustace, walikwenda kwa mambo yao, bassi wakasikia kama ameuawa kusudi, alipigwa risasi la bunduki, bassi kukimbilia majini na kufa humo. Bassi watu wa pale wakatwaa nguo zake na kutupa majini, kusudi waseme amezama majini. Na mwili wake twasikia wameuweka kilimani. Bassi hapo ndipo mwisho wa ndugu yetu Stefano Rehani, hatujasikia habari tena hatta leo hivi. Na baba Rev. W. P. Johnson alikuja pia, kwa Jumaa kuu, kwani nalisema kama alisalia pande za chini.

SIKU YA PASAKA.

Hurrah! Hurrah! Wote tupo hapa mkutano. Furaha kabisa; kuonana, kwani kwa miezi mingi bado kuonana pamoja. Ee ndugu, Mtengenezaji Msimulizi! Hebu! kae kitako, nikuarifu vema, upate kutuletea vema habari. Sikia!

Panapo siku ile ya Pasaka yenyewe kama ujuavyo ni Juma a pili, ao sisi watu wa huku twaita "siku la Mulungu" la, "kupuma pa nchito," ndio kustarehe katika kazi. Tukala karamu sisi kwa sisi, ikawa furaha kabisa. Tukalala. Panapo juma a tatu wakaenda watu wa nje walio Wamasihya na walio waanafunzi wa kupewa msalaba. Wakaja kwa karamu, ndama ya ng'ombe akachinjwa, chakula kikapikwa wakala, mke kwa mume, kijana kwa mzee. Wakapewa na ndoana tena, panapo mshuko wa alasiri wakaenda zao. Ndio siku ya Juma a tatu. Na panapo Juma a 'nne yakawapo mashindano ya namna namna, yule afikaye wa kwanza ao wa pili hupata "prize" (thawabu). Panapo alasiri, Ah! tukakaa tu papa hapa. Na panapo Juma a tano, waalimu, yule atakaye, kwenda Mchizumulu. Bassi tukaenda Augustine, Mapundi, Aruffo, T., Daudi, Benjamin, huyu ni mwalimu wa huku, na W. K. K. na watoto wangine wa

MSIMULIZI. 206

chuoni wapata nane pamoja hivyo. (Na siku hii ya Apr. 9, ndipo akaja Paul Mambo na mkewe na watoto wao pia, bassi ikazidi jamaa yetu). Tukashinda huko hatta panapo Ijumaa, tukarudi alasiri wangine waliosalia hapa wakacheza mpila tu. Na panapo juma a mosi katalika kama siku zote tukaosha nguo zetu, na panapo alasiri, walio waalimu, tangu mwenyi mke hatta asiye naye, tukatwaliwa sura ("Photograph") wote pamoja; baadaye akina bwana wote wakatwaliwa sura zao. Bassi waona ni furaha tu, kwani tangu zamani bado kukusanyika pamoja kama hivi.

Siku ya Juma a pili vile vile tupo wote, na panapo alasiri mtoto mmoja akabatizwa wa ndugu yetu Paul W. Mambo. Ndio siku ya Apr. 10 jina lake alilopewa ni "Cecil Paul" Mambo, kwani ni mwanaume. Panapo Juma a tatu hii ingine Apr. 14 tukakaa papa hapa tu na furaha yetu, na kufunga mizigo ya hawa wa chini. Siku ya Juma a nne panapo saa nne tukawapakia wale wa chini kwa bunduki katika jahazi "Charles Janson" wakaenda zao. Ndipo ikawa mwisho wa siku kuu yetu na furaha yetu, na karamu yetu. Kwani sisi wa hapa panapo alasiri tukafungua chuoni kusoma,

Nimesema kama "Charles Janson" yaenda chini kupeleka waalimu. Bassi panapo Juma a tano ikarudi jioni. Hatta panapo Alhamisi, ikashika njia ya kwenda Bandawe ndio kwenyi Mission ya Waskachi Dr. Laws mkuu wao. Ilikwenenda kusudi kumpeleka Mr. C. Alley, mgonjwa, akaangaliwe na mganga huyo. Wakafika, lakini Dr. Laws mwenyewe hawakumkuta, kwani naye ni mgonjwa sana. Bassi akaenda kwenyi baridi, ni milimani kwa Waangoni, ao Makwangwara, kupata afya. Bassi wakamkuta mganga mwingine mdogo aliye chini yake. Huyo ndio akampa mashauri: bassi panapo Ijumaa jioni wakarejea hapa.

MSIMULIZI 207

Sikia habari zingine. Leo Apr. 22nd furaha tena, ndio ipo harusi ya watu wawili kati ya Charles Nasibu wa huko kwetu Mbweni, na mke wa hapa chuoni petu jina lake Mary Mchono, na kati ya Wm. Yona Kao, mtoto wa chuoni humu wa huku huku, naye na mke: jina lake Elizabeti Kumtiwa wa huku huku. Ndio harusi, ilikuwa njema kwa upande wake, kwani killa ghasia ya bunduki ilikuwapo, si namna ya ngoma. Wallakini, bwana, kama ujuavyo, ya kuwa huku ni barra, bassi haiwi sawa wala kupita ya huko Mbweni. Kwani huku hakuna watu wengi wajuao maana ya harusi hizi za Kimasihiya. Ndio habari.

Na Msimulizi huyu hangalikuja upesi, isipokuwa "Charles Janson" anangoja mashua yake inatengenezwa, kwani ni mbovu, nayo anayo hiyo moja tu, kwani ya pili ile iliyonyang'anywa na Wayao wa Mdoka huko chini, kama nilivyokuambia huku nyuma. W.E.K.

Panapo mwezi May tutamsafirisha Bwana Archn. Maples kwenda Ulaya pamoja na watoto wa huku waendao Unguja. May 2.

(Lakini hao watoto hawakujaliwa kuja petu, kwani uthia wa Wareno njiani. Bassi wakarudi kwao. Labuda mwaka wa pili watakuja. Mtg.

HABARI ZA MAGILA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu kama katika May 21 tukaenda Mkuzi watoto wote tukatoka kama saa ya kwanza assubui. Mr. Dale ndiye aliyetuwekea nafasi, kuwa wageni watoto wake wa Magila. Assubui yake Juma a nne, watoto wakacheza mpila, hatta kama saa kumi nathani, tukashika njia kurudi kwetu Magila; watoto wadogo walichoka sana wakati huu wa kurudi, kwani tulipatwa na mvua njiani.

MSIMULIZI. 208

Katika May 28, tulipata habari ya huzuni mno itokayo Uмба, ya kuwa mamake mwalimu Peter Limo amekufa; alikuwa hawezi sana kwanza karibu na Msaraka. (Mkumbi), tena akahamishwa Uмба, ndipo akafariki.

Tena katika May 29 Mr. Dale akawatazamia watoto kusoma, mimi nikatazamia darasa mbili, ya nne na ya tano. Ingekuwa kwa siku mbili tu nathani, lakini kwa sababu Mr. Dale akashikwa na homa marra kwa marra; bassi ikawa kwa juma moja u nuss, kwani akiwa hajambo atafanya awezavyo, lakini marra hushikwa na homa. Nazo darasa tano zilizotazamiwa, nao walioshinda ni hawa katika darasa ya kwanza, 1. Basil Mhada, 2. Earlo Mwaimu; Darasa ya pili 1. Michael Mfuko, 2. Edward Kirigodi. Darasa ya tatu, 1. Mngindo, 2., John Longton Mwaimu. Darasa ya nne, t. Chavuchavu, 2. Kingodi. Darasa ya tano, 1. Bebe, 2. Mfuko.

Katika June 15 Bwana mkubwa wa Tanga Herr Krenzler alifika hapa athuuri, pamoja na yule mkubwa wa forotha yao ya Unguja na asikari haba tu, kama kumi; kwani haogopi sasa, hapana adui atakayepigana naye. Hatta asubui akaenda zake Misozwe, tena mpaka Tanga, lakini alipokuwa hapa akasema kama "Pangani wapo "Sisters" wa Kidachi, kazi yao kutunza wagonjwa Bassi Mzungu akiwa hawezi hapa, apelekwe Pangani auguzwe; ikija mashua ya moshi ndio apelekwe Unguja; na Tanga pia kipo chumba kizuri kwa Wagonjwa; mkitaka leteni wagonjwa, watatunza.

Katika June 18 ikaja habari kusema kama Wamasai wanakuja, wapo pa Ntunuritu, ndio karibu na Misozwe. Lakini tukangoja wee, nao hawaji. Lakini tukasikia tena kama wapo kwa Kibanga, wanajenga mji na boma, wakiisha ndio walete vita; wakifukuzwa waende bomani pao, lakini kutoka bomani ndio hawatakubali hatta kidogo.

MSIMULIZI. 209

Bassi haijulikani kama ni kweli; lakini habari imekuja kama wanajenga boma lao na mji, wakiisha waanze vita. Ah! safari hii hatuogopi, tutawafukuzia mbali pamoja na bwana mkubwa wetu wa Tanga Herr Krenzler, kwani yeye anatamani sana Wamasai waje apigane nao.

June 28 akafika hapa mwalimu Reginald Songolo, assubui, amekuja kutembea kwa mwezi.

Katika July 2 tulipewa watoto wote ruhusa tangu assubui hatta jioni kwenda killa mtu kwao na kurudi jioni. Illa watoto wanaokaa Msaraka waliondoka hapa alasiri siku iliyopita, pamoja na Mr. Roberts na Sister Agnes, wakaenda Msaraka, na Reginald Songolo pia wakarudi siku ileile ingine tunayorudia, watoto wote jioni. Na July 10 tukaingiwa na furaha nyingi sana, kuwaona, Sister Ann Margaret na Wazungu waume wawili wakiingia hapa assubui. Hatuna buddi tufurahi sana sisi tukijiwa na watu wajao kutufanyia kazi.

Sister Dorothea na Sister Clara, marra kwa marra wanashikwa na homa siku hizi, kwani hawajazoelea bado hewa ya Bonde, lakini sasa wote wazima. Tena tuna hatari sana ya kanisa letu "Msalaba Mtakatifu". Boriti zake zote mbovu kabisa, bassi mvua ikija linavuja sana: hatta huwezi kupata hamsini zilizo nzima tunavyothonia.

Siku hizi twataka Magila tuwe na watoto kama mia tukiweza, lakini kwa siku hizi wana kazi mashambani mwao, labda mavuno yakiisha, lakini hatujui kama tutapata, twatumaini tu. Siku hizi tena Mdachi anaanza kutoa amri katika inchi za huku anazotawala, twajua mbili tu sasa: ya kwanza, Saa ya tatu ya usiku ikiisha, hapana kutembea njiani wala vijijini: ya pili, ngoma zote na michezo yote ya kuimbaimba usiku hapana, illa kwa ruhusa ya Mdaichi

MSIMULIZI. 210

kwanza, ndio watu wafanye michezo na ngoma katika miji. Tena Kibanga na Makange wameondolewa enzi yao, illa atakuwa liwali tu katika inchi, lake jina Abdallah Gugu. Martin Furahani anakwenda kukaa. Misozwe sasa, kwani Henry amefiwa marra ya pili sasa na mtoto wake kulekule Misozwe; bassi itamfaa abadili hewa.

Tena katika July 12 amekuja mfalme Mdami kuamkia, yule aliyewakaribisha ndugu zetu Mr. Wilde na Dr. Castle na Samuel Sehoza na wangine walipokwenda Zigua. Ni mtu tajiri sana, ukimwona huthani kama ni mtu wa Zigua. Na kabila lake ni Mpale: malidadi sana mtu huyu, upanga wake umejaa fetha tu, illa mahali padogo tu pakashikia penyi ala yake, na joho lake, ah! la. Peke yake; kwa uzuri; na kanzu yake, naam, ni mfalme kwelikweli yeye. Asubui yake Juma pili, akaja kanisani na watu wake: yule mtoto wake aliyekuja ufundishwe, marra kwa marra akawa hawezi, bassi amerudishwa kwao, lakini labda atakuja tena pamoja na wangine wafundishwe we waalimu.

Katika July 14 tulifurahi sana kumwona Archdeacon Maples akifika hapa asubui. Hatta sisi wengi hatumjui, lakini tulifurahiwa naye akitoka barra ya Nyassa na kuja kutuamkia. Hatta jioni akatukusanya Chuoni, akatuambia habari nyingi za kazi yake na mambo yote ya Nyassa, tukafurahiwa sana kusikia yote ya wenzetu wanavyofanya kazi yao.

Lakini tukahuzunika ya kuwa siku ya pili yake alitoka hapa alasiri yeye na Mr. Woodward, na bibi Smith alitoka asubui, wote waja huko Unguja; bassi tukamhurumia kwani hakupumzika, tangu Pangani mpaka hapa alienda kwa miguu pasipo punda.

Katika July 16 Mr. Viney alifika hapa jioni akitoka

MSIMULIZI. 211

Mkuzi. Alikuwa na Archdeacon Maples, lakini yeye alipumzika Mkuzi siku mbili kwani alichoka kwa mwendo.

Katika July 21 Mr. Vinfey na Mr. Ross, wakatoka hapa assubui kwenda Misozwe, na Mr. Dale alitoka alasiri kwenda kumwalia Martin na wangine. Bassi assubui yake Mr. Ross akapata homa kulekule Misozwe, na Mr. Viney akamleta hapa: siku ya tatu ugonjwa ukamzidi sana sana.

Katika July 25 Tulienda mlimani kushinda watoto wote na 'day-boys' wangine. Tulienda mbali sana, juu kabisa kupita Seluka safari hii, pamoja na Mr. Viney. Wengi walichukua bunduki wapige ndege, mimi nikaingia maguguni pamoja na Mr. Viney tusipate kitu, lakini wangine walipata.

July 27 Mr. Ross alizidi kuugua, bassi akapelekwa Tanga aje Unguja. Kufika Tanga akakaa kama zayidi ya juma nzima isije Stima, bassi akapata hajambo, na sasa amerudi.

Na Mr, Dale naye alishikika sana na homa Mkuzi, bassi Mr. Roberts akaenda kumtwa kuja naye Magila, na sasa hajambo sana.

Tumesikia tena habari ya ajabu. Kama mfalme wa Wakilindi Kimweri, ameshua na watu wapata elfu kwenda Pangani, lakini hakupitia kati ya inchi ya Bonde, illa upande wa kusini. Ni ajabu sana yeye ashuke, kwani yeye ni Mkilindi, hutharau sana watu wakaao pwani, na ginsi alivyo mfalme kweli-kweli, hataki aje inchi ya Bonde wala pwani, bassi ndio marra ya kwanza akanyage inchi yetu na kufika Pangani. Twatamani sana tumwone, lakini Wabondei hawampendi; kwani marra nyingi yeye huleta Wamasai kuja kutupiga, lakini twapenda aje apitie na Magila akirudi kwake tupate kumwona.

MSIMULIZI. 212

Katika August 11 akafika hapa nahotha wa Boadicea pamoja na mtumishi wake (Mzungu,) na daktari, Wazungu watatu, na askari wa Kinubi watatu na bendera ya Kidachi. Tulitengeneza vyumba tayari na killa kitu, kwa heshima ya nahotha. Hatta athuuri wakatafutiwa wapagazi wapate kwenda zao Misozwe, kwani tangu Pangani mpaka hapa mizigo yao ilichukuliwa na watu wa Kimweri, bassi wakarudi tena Pangani. Bassi athuuri wakaenda zao Misozwe, pamoja na mwenyeji wao Martin Furahani, nao wameenda nyikani karibu na Digo kuwinda nyama. Na wakatupa habari kama Admeli anakuja bado siku tatu.

Hatta August 14 jioni, ndipo akaja Admeli na mtumishi wake Mzungu, na Mr. Woodward, na mwalimu Hugh Mtoka na Arthur Mveuya: killa kitu kimeisha wekwa tayari.

Hatta asubui Jumaa, watoto wote tukabadili vizurivizuri kwa heshima yake. Tukaenda chuoni kusoma saa moja tu asubui, bassi akaja kuangalia, watoto wengine walisoma Kiingereza mbele yake, tena akaangalia Copy books za watoto, akapendezewa sana na kuona ajabu ginsi walivyosoma Kiingereza na kuona maandiko yao, killa kitu hapa aliangalia na kuonyeshwa kwa adabu. Nasi watoto tulipewa siku nzima ya kucheza kwa heshima yake, tangu asubui hatta jioni.

Bassi alasiri Admeli na Mr. Woodward, mimi, Hugh Mboka, na Arthur na askari mmoja, tukaenda juu mlimani, mangaribi ya mji wetu huu Magila. Tukapanda mpaka juu kabisa, na yeye mwenyewe Admeli alipendezwa sana, bahari na visiwa pia tukaona, kama ingalikuwa shwari tungaliweza kuona Unguja. Bassi wakati wa giza kidogo tukarudi zetu nyumbani.

Na asubui yake Juma a mosi, saa kumi na mbili, akatoka akaenda zake Misozwe pamoja na askari wa Mdoicha aliopewa Pangani; huko Misozwe ameenda nyikani kwa

MSIMULIZI. 213

nahotha wake wakutane huko huko, wazidi kuwinda nyama, kwani walichukua bunduki nyingi na za nguvu. Wakiisha watarudi Unguja wakipitia njia ya Tanga, pamoja na ndugu zetu hawa waja nao wakae Kiungani wasome, Basil na Karlo na Leonard Pesa.

Bassi ndugu zetu wa killa Upelekwa, mtastaajabu sana, ginsi siku hizi tunavyoheshimiwa, hatta Admeli mtu mkubwa kweli kweli, lakini amependa kuja Magila; tulistaajabu kusikia kama Admeli atakuja Magila. J.B.M.

HABARI ZA MSARAKA.

July 13, 1890.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu ninathani utapenda kusikia habari ya huku kwetu, kwani ninaona safari zako nyingi umenijia. Lakini hukupata hatta kidogo habari za miezi ile iliyopita.

Siku hizi kazi yetu ya Chuoni imerudi sana nyuma, kwa maana watoto ni shidda sana kupatikana, baba zao na mama zao wanawahitaji kwa kuwasayidia kulinda ndege. Bassi nimepata ruhusa kufunga chuoni kwa mwezi huu wa July, tunatumaini mwezi wa August haina buddi tutawapata, kwa maana mavuno yao yatakwishia, bassi tutawapata. Na mwaka huu Wabondei ninatumaini hawakudanganyika kuacha nafaka zao kuliwa na wanyama, lakini palitokea uwongo mmoja wa kusema, Mlinga hataki watu wakalinde mahindi, kwani mwaka huu watu wa huku kwetu waliuthika sana kwa nguruwe. Bassi Wabondei wangine wakasema, Kwa maana gani Mlinga hataki tukalinde nguruwe? Walijibiwa na wenzao, Nguruwe ni waanawe Mlinga. Walinena, Tufanye jambo gani? Wakasema, Yafaa killa mtu atwae vipande vya mbaazi viwili aende shambani akizunguka akipigapiga akiisha arudi killa mtu nyumbani kwake.

MSIMULIZI. 214

Marra nilipata habari hiyo. Nami hawaambia, Tafathalini msidanganyike kuacha mahindi shambani, haina buddi yataliwa na nguruwe. Hawakukubali, lakini assubui walipoamka killa mtu alikwenda kuangalia shamba lake akaona upande mahindi yametafunwa. Bassi killa mtu hakukubali kulala mijini, mume hatta wake waliamia shambani.

Ninathani mtapenda kusikia habari iliyotokea panapo July 18. 1890, siku ya Ijumaa. Mwajua tangu kutawala kwa Madachi, inchi ya Bonde imetulia sana. Ninathani hatta pande nyinginezo haina buddi nazo zitatulia. Lakini July 18, siku ya Ijumaa pana saa sita va athuuri twalistaajabu sana, kwani palitokea mwanamke mmoja anakaa mji mmoja unaitwa Mavumbi. Alichukua kikapu chake, hari zikimtoka, nguo alivaa mpaka magoteni aliwasili mji mmoja unaitwa Mkumbi. Bassi waanaume walimwuliza, Kwa nini ukawa hali hii? Naye aliwaambia, Ni kwa maana mji wetu ndio Mavumbi kwa Mfonga pia umechomwa na Wamasai. Wamekuja na Hungura, bassi ndipo nawaambia aibu ilipoonekana kwa waume, hatta wake, halisi kwa waanawake. Marra ngoma za kuonyesha dalili ya vita zilianzwa kupigwa. Tangu kutawala Wadachi madawa ya vita yalisahauliwa, lakini siku hiyo yalikumbukwa. Bassi mashujaa ya vita. waliondoka, hatta walipofika mahali panaitwa Mahalawe (soko) walikutana na waanaume wenzao wakipiga makelele ya kondo. Kwani nao walikwenda kwa kasidi ya hiyo vita. Bassi waliwauliza, Za nini ngoma zinazopigwa? Wale waliwaambia, Zinapigwa burre, hakuna vita, ni Semakunda anatoka Giriyaama, inchi ya Waduruma. Bassi marra walirudi mijini mwao.

Bassi kama tujuavyo mtu akisafiri inchi iliyo mbali, atakaporudi salama wa salimini hana buddi kupiga bunduki na kurandaranda kwa furaha ya kurudi salama katika

MSIMULIZI. 215

safari yake, lakini wao waliposikia bunduki walithania kuwa Wamasai, kumbe sio. Bali July 17, twalipata habari ya kuwa Wamasai karibu watakuja. Bassi ilipopata alasiri twalisikia ya kwamba sio Wamasai, ni Walaita wanawavizia Wabondei. Bassi na mshindo huo uliotokea July 18, ilisadikiwa mno kuwa Wamasai. G.K.

HABARI ZA MISOZWE.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salam. Wa baada ya salaam, na kuarifu habari za huku kwetu Misozwe.

July 15 alasiri nikaona watu wawili wanatoka kwa Makange, wakaniambia, Jumbe Makange salaam; wabaada ya salaam, andika barua sasa hivi kwenda kwa Liwali Magila. Mwambie Hungura huyu yupo Gonja ana vita; bassi upesi toka na asikari usiku huu umlaki kabla hajavuka mto Zige. Labda usiku huu ataingia vita, ipo mlangoni, ao saa 10 za usiku ataingia, kama safari ile alipokuja na Wamasai.

Nikatwaa karatasi nikaandika barua kwa harufi za Kiarabu, maana Liwali hajui harufi zetu, saa tatu u nuss barua ikatoka na mtu kwenda. Hatta usiku ukiwa nikaona hofu kwa watoto na kwa bibi yangu na ya Arthur, nikasema, Jumbe hasemi wongo, na Hungura ana hasira, kwa sababu aliona Wazungu wetu vita ile ya Wamasai; Bassi alithani ndio sababu ya kushindwa Wamasai, kwani wakali hao Wazungu, Wallakini Wazungu hao hawakwenda kwa kupigana illa waone adui ni nani hao. Bassi nikaona shidda sana nikawatwaa wote tukawaondoa tukapanda milima kwa mji mmoja wa Washambara tuliojua sana, tukawa pale; hatta saa 10 nikatoka na Arthur kurudi kwetu tuone yatakuwaje, kwani saa 10 ya usiku ndipo vita iingiapo. Tukaingia Misozwe saa 10.15, tukaona salama

MSIMULIZI. 216

vyote, kwani tulifunga nyumba zote, hatta saa 3 ya mchana nikapeleka kuletwa watoto na wake.

Mchana wa Juma a tano uthia tu, Abdallah asije siku ile. Nikiuliza watokao njia ya Magila watasema, Abdallah anakuja, na nikiwauliza watokao njia ajiayo Hungura, wote husema, Hungura huyu njiani; nisipate iliyo kweli hatta saa 8.

Nikaonana na mtu atokaye kwa Liwali Abdallah, akasema, Salaamu Allahu Abdallah, wabaada ya salaamu, peleka hatta kwa Makanje, kaseme, Abdallah asema, Peleka hatta kwa Hungura, mulize vema ana vita ama sivyo. Nikaona vema karibu yangu, nikatoka mimi na Arthur saa 10 kwenda Kumbamtoni, ndio mji wa Makanje. Nikafika nikaonana nikatoa habari zote, naye pia akanitolea pia, akasema, Sikujua habari hizi kama Hungura yuko, illa nina mtoto wangu mwana wa ndugu yangu, ndiye aliyeniletea habari hizi. Nikamwuliza, Je! Jumbe, habari sasa, nifanyeje. Akasema, Hatta mimi nimepeleka kwa Hungura, kuuliza kama ana vita ama sivyo; Bassi wewe mwalimu, nenda zako kwako. Watu wakirudi niliowapeleka, watakavyosema ana vita ana amani pia nitakuletea habari kadri wafikapo tu. La, Hungura katharau watu wangu hakuwatolea neno lolote, akija kwa nguvu, simpi njia; nitampiga, ao ajapo kwa ghafula hatta siwezi kukuletea mtu, bassi utasikia baragumu ndio dalili ya vita, ao akinipita nimelala nikisikia bunduki upande wa Bonde la Masange (ndio bonde Wamasai walipoua watu wengi sana) nitamfuata Hungura hatta kumpiga kabisa, simwachii Hungura mtu hatta mtu. Bassi mwalimu, nenda zako, ngoja kwangu kwa habari utakazosikia, kuona watu ao kusikia baragumu. Nikaagana naye nikatoka nikakesha kwa zamu mimi na Arthur nisisikie kitu mimi. Hatta asubui nikaona watu wawili kusema, kama Hungura hana vita illa kaitwa

MSIMULIZI. 217

na Mdachi wa Pangani; bassi ataka kupita njia ya Bonde hatta Pangani; bassi nawe andika barua kwa Liwali Abdallah, kusema kama Abdallah ajua habari hizo, kama Hungura anaitwa kweli. Bassi pita kamtwae, wallakini asipite njia ya Bonde hatta kidogo.

Nikaharaka nikaandika barua. Nikapeleka ndio siku ya 18 ya July. Abdallah akatokea akaenda aonane na Makanje, sijui tena walivyokwisha, Hungura karejea kwake, asema Wadoicha wakinitaka wapeleka mtu kunitwaa.

Siku ya July 21 akaja fisi usiku mjini Misozwe (ndio wenye jino haswa) akavunja nyumba ya mtu moja aitwa Kazogolo akatwaa kondoo, wamfuata watu wasimpate. Siku ile ile wakaja Mr. Viney na Mr. Ross kutembea na Bev. G. Dale

July 23 usiku akaja nyama aitwaye kiribe, akakamata kuku wetu, akaenda zake na kuku huyu alichelewa kuingia ndani.

July 24 usiku akaja fisi akaona tena kuku amechelewa akamfukuza sana kuku akamkamata, lakini hakumkamata vema kuku akapokonyoka akarukia juu ya mti akawa kule hatta assubui.

July 31. akaja mkuu wa askari Mdachi alitokea Magila, na pamoja naye askari 12 na watumishi 2 na mkalimani mmoja na ndiye kiongozi wa njia. Jina la Mdachi huyu ni Hograth, na mkuu wa askari weusi, jina lake Swisz Mturuki.

Ndio siku ya gulio Kisinga. Watu walipowaona wanakuja asikari wote watu wakakimbia illa kwa shidda sana tukawatuliza watu. Nikaenda nionape na askari nikawauliza kama wanaendea mji yetu. Nikapata bania nikawatangulia hatta petu, wakafika kama saa 5. Jemadari kapanda

MSIMULIZI. 218

Hatta kwa majira ya saa 9 akapita Mbondei mmoja ana bunduki. Marra wakamwona wakamwulizia asimame. Kwani siku hizi si ya Bonde hapana mtu kutembea na bunduki illa askari labda wa Liwali Abdallah, ao wa Kibanga ao Kinyasi ao Kimweli ao Makanje. Bassi marra wakimwona wakamwita "Ewe mwenyi bunduki, njoo," asije ile kusikia, ya pili ya tatu pia. Marra wakafanya shauri akamatwe Ya 'nne, ataka akimbie, ama yumo mkononi mwa askari ghafula, hana bunduki wala pembe wala shime yake. Wakamchukua hobelahobela hatta kwa banda alipokuwa mkuu wao. Yee akasema Na apelekwe kwa Commander. Akaambiwa, Inuka twende. Akasema, "Ah mimi siendi, sababu mimi si jumbe." Wakakaa hivyo kubishana. Hatimaye wakamwinua kwa nguvu, Ah! akapiga kelele kuu sana hatta kumwamsha yule Jemadari mkuu.

Akiamka akauliza asipate iliyo yakini. Nikaitwa kufasiri, kwani alinifanya mkalimani, kwani ajua sana Kingreza kuliko Kiswahili, bassi yee huniambia yote, nami hutoa kwao askari. Na yule mtu pia naye tena huniuliza habari zao killa neno, mtu gani, katoka wapi, shughuli yako nini, kwani anatembea na selaha hii tena kwani haina chapa ao alama ya Kidachi. Kwani haswa alilokamatiwa ni kwa sababu bunduki yake haina alama ya Kidoicha. Hatima akasema na akae hatta ajapo Abdallah Liwali, akawaita wakuu wa miji hii Misozwe, Hemkole, Hesosolwe, Kwemikwamba, Langaia.

Walipokuja, akasema, "Nataka chakula kwa askari zangu, na kondoo ao mbuzi kwa kitoweo chao." Hatta saa 10 wakaja wa kule wale na ugali na kuku ndio kitoweo chao. "Ah!" akawafukuza vikali sana. Hatta saa 11 akatokea Abdallah, yule mtu akaletwa nikaitwa, kufasiri

MSIMULIZI. 219

maneno kati ya jemadari na liwali, liwali aseme, mimi nimwambie jemadari, jemadari aseme mimi nitoe kwa liwali, hivi hatta tuyamalizapo maneno yote. Na yule mtu, akapewa Abdallah bunduki ikaamuliwa kwenda kwa Tanga kutia alama shime yake, ikatwaliwa na jemadari Mdachi na pembe ya baruti pia. Marra majumbe wakaja kwa Liwali kusema habari za kitoweo cha askari hawa na mbuzi wala kondoo. Bassi nikaitwa na Liwali nifasiri, ataka kusoma na jemadari Mdachi, kama hawana kitu chochote illa kuku tu. Akasema, Vema. Wakaenda kutafuta. Abdallah akawasayidia kutoa fetha wakapata kondoo wakaleta saa 3 ya usiku, askari wanapika nyama, ugali ni tayari. Nikauthika sana nao, wallakini ah! nitendeje? Tukajinyosha wote. Hatta saa 9.30 usiku nasikia naitwa, nikatoka nikaona yule jemadari aniuliza punda wake, hamjibu, Sikumwona. Kumbe punda katoroka usiku maana hakufungwa, yakawa haya na haya, akaamuru asikari kutafuta pote katika mlima wote. Hatta saa 10 akapiga baragumu, askari wote wakarudi, akatoka kusafiri kwenda Bwembwara. Akaniachia askari 4 na kijana mmoja aliyeangalia punda, akaniagiza sana nitafute pote, mpaka saa 5 ya mchana niwape askari habari kaonekana ama sivyo pia. Nikijua kama punda hapotei njia saa 11.

Nikatoka nikatwaa selaha, nikafuata njia ya Magila kwa maana ndiko walikotokea. Nikiendelea kama robo ya njia nikaona nyayo zake. Hatta kama mayili mbili nikaona kabisa nikafuata, hatta kwa mayili 4 na zayidi, jua likatokea kuchomoza. Nikifika njia ya panda, marra nyayo zikanipotea, haona hapa alikutana na nyama mkali, wa mwitu, nikashika kufuata hatta Magila, nikafika saa ya kwanza n nuss, nikatoa habari. Nikaambiwa, Hakufika hapa. Saa tatu nikatoka kurudi Misozwe, nikafika saa ya tano u robo. Nikaandika barua nikawapa wafuate njia ya jemadari

MSIMULIZI. 220

alioenda.

Aug. 2, Nikatoka usiku saa 10 kwenda gulio la Mambosasa, kutafuta vifao vya watoto wetu. Njiani nikirudi nikapate kutazama watoto kujieleka Misozwe. Nikampata mtoto aliyekuwa akikaa Magila, sasa yu kwao, nikasema naye, lakini labda hataki. Nikarudi Misozwe nikaambiwa, Punda huyu akaleta, ni Mbondei. Nikasema, Vema. Hatia juma a tatu ndio Aug. 3 nikampeleka Tanga na barua kwa Liwali Mdachi. Ndio habari kidogo na thaifu. M.F.

P.S. Aug. 11, Alifika kwetu jemadari wa Waingreza aliyetoka jahazi H.M.S. Boadicea, na Dr. Harris na baharia George, wanaenda kupiga nyama. Naliagizwa niwatafutie mwenyeji mwinda, afuatane nao. Nikawatafutia. Sasa wako kando ya mto Zigi, wanapiga nyama katika inchi iliokufa ya Wabondei. Bamba ana asikari Wanubi 4 aliopewa Pangani na Wadachi kuonyesha inchi ina mtawala Mdachi.

Aug. 13 akaja fisi usiku akakamata kuku saa 5 usiku katika nyumba isio watu. Nikifungua mlango nina bunduki ya kubandua niki mwona ikanitoka nikampiga nyuma ya nyumba, asianguke, akaingia maguguni. Nikatokwa na ya pili, nikamkosa. Watu wakaja kunisayidia kutoka miji ya chini. Nikawapa shauri tumzuie. Ah! Wabondei waoga wasikubali. Wakakubali kumfuata nyuma. Nikawapa ruhusa wakafuata, marra akawatisha wote wakarudi nyuma, wote pia mbio; wakipewa moyo, wakaendelea illa kwa woga tu. Fisi akatupa kuku akapata njia akaenda zake. Nikatafuta nisimpate, nikarudi.

16 Aug. Admeli akafika petu siku ile ile akaenda Zigi. M.F.

HABARI ZA MKUZI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu

MSIMULIZI. 221

nakuarifu habari kidogo tu. Siku ya Barnaba Mt. mimi na watoto wa Mkuzi na mwalimu George na William Swedi twalienda kushinda Mkwiazu wa ntano peke yetu kwenda kucheza kurudi jioni, watu kumi na moja tuliokwenda.

June 22, Juma a 'nne athuuri saa sita u nussu, tukasikia kishindo kikubwa sana cha kanisa letu la Mkuzi limeanguka upande uliokuwa ukijengwa nguzo, na majukwaa yake pia yote imeanguka, illa upande wa mathabahu na nussu tu zilizobaki, ndio upande uliokuwa ukimalizwa kujengwa, nalo limeanguka karibu na nyumba ya Mwalimu mkubwa, naswi tunasikitika sana mno. G.L.

MATAIFA YA ULAYA.

Mataifa ya Ulaya wanakumbuka sana mambo ya Afrika siku hizi, na zayidi biashara za watumwa. Hatta wamefanya baraza kubwa katika Brussels, mji mkuu wa Belgium, killa taifa likatuma wajumbe kwenda kufanya shauri la kuzuia biashara hiyo. Wakaja wakakaa siku nyingi, wakifanya maneno yao. Na aliyetoa shauri la hekima sana ndio yule Sir John Kirk, aliyekuwa barozi wa hapa zamani, akapewa jina la heshima kwa ajili ya shauri lake.

Tena Mr. Stanley ameandika habari za safari yake ya kupita tangu Kongo hatta Unguja katika kitabu kikubwa chenye sanamu nyingi. Kitabu kile kimeenea sana katika ulimwengu wote, kinazidi kuwakumbusha watu wote habari za Afrika na mambo yake. Bassi siku yake Afrika zinakuja, zinaleta mambo mengi, mengine mema mengine mabaya, ndivyo hivyo siku zote. Haya! tufanye tuwezavyo.

Kwa vita ya pwani hatuna habari nyingi. Twasikia tu kama kumekuwa uthia kidogo pande za chini penyi Kilwa na Lindi, hatta Madachi wameifunga inchi wasipishe watu wetu, lakini labuda kwa muda kitambo.

MSIMULIZI. 222

HABARI ZA MKUNAZINI.

Kwa Mtengenezaji wa Msumulizi salaamu. Baada ya salaamu nakuarifu habari kidogo za huku kama Aug. 16 tuliitiwa karamu kubwa sana, kwa sababu ya Mr. Madan tangu kuja kwake hapa Unguja kwa ajili yetu sisi watu weusi yapata sasa miaka kumi.

Tena nakuarifu kama Petro Abdallah amefariki.

Na siku hizi mjini kumekuwa na kishindo sana sababu ndio hii. Iliandikwa khati ya kutiwa watu wote huru katiwa forothani killa apitaye asome. Bassi Waarabu na Wangazidya hawakukubali wakaenda kutatua ile khati, ukawa uthia sana, umetulia kidogo. Lakini khati ngine iko ya kusema, kama watoto wa watumwa watakozaliwa sasa watakuwa huru, walakini mwisho wake itakuwaje sijui. Na tena siku ya mwaka wa Kiswahili kishindo cha nguvu hatta bunduki zinapigwa, watu wawili wamekufa. Na tena nakuambia ni habari ya furaha, wote mtafurahiwa, ni hii ule mnara wetu uliovunjika ncha kwa radi sasa umekwisha jengwa vile vile. Na huku uwani kwetu tumefanyiwa pembea tuchezee. Na tena Mr Weigall anakaa hapa kwetu. Na Daud Tovi amekwenda kwao Newala. Na tena habari hii kidogo, Michael Mradi anataka kuchuma kidogo, ametoka katika uwanafunzi kawa fundi anafanya kazi kwa mshahara wake.

Na leo Aug. 24 siku kuu ya Bartolomayo akabatizwa mtoto mmoja wa Miss Mills, jina lake Bartolomayo.

HABARI ZA SHAMBA LA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu kama ndugu yetu William Mabruki aliyekwenda fanya kazi Tanga kwa Wadoichi amerudi hapa June 13, na June 25 ndugu zetu wangine wa hapa

MSIMULIZI. 223

Ibrahimu na wangine wamesafiri kwenda Uganda na Askofu wa Mvita.

July 3 Deva Dimwende ameo. Mr. Key amefanya shauri jema sana ya watoto wote waume walale nyumba moja, wanalala nyumba ya Mabruki. N.F.

HABARI ZA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu, nataka nikueleze habari kidogo. Siku kuu ya Petro Mt. ilikuwa Juma a pili lakini tukaiadhimisha June 29. Naswi wote watoto wa Mbweni tulikwenda shinda Chukwani tukashinda barazani pa nyumba ya Sayidi, kwani tulipata rukhsa, na msimamizi Amani akawapatia madafu Wazungu wetu, tena tukazunguka bustani yote na tukala chakula chetu upenuni pa nyumba ndogo. Saa 10 ya alasiri tukarudi kwetu.

July 23 watoto 49 tulikwenda Mnazi mmoja, tulikwenda alasiri saa 3 u nussu kuangalia askari wa Kiingreza mchezo wa vita.

Hatta July 25, assubui mapema saa 10 tukaamka tukashika njia hatta Shangani nyumba ya Barozi mkubwa. Kule tukaangalia ginsi merikebu zote zilizo forothani zilivyopambwa kwa bandera, na mizinga ilivyopigwa mingi mingi, mizinga na kathalika bunduki. Sultani Seyidi Ali alikaribishwa na Admeli katika merikebu yake Boadicea.

Barozi mdogo na Bibi yake wana huzuni nyingi kwa mpendwa mtoto wao mdogo amefariki Aug 15 usiku, nao rafiki wasikitika kwa huzuni iliyowapata. R.M.

HABARI ZA KIUNGANI.

July 14, Archdeacon Maples alitelemkia Bonde kutazama Magila pamoja na Mr. Viney. July 16, Archdeacon Jones-Bateman

MSIMULIZI. 224

alienda kutembea ndani ya H.M.S. "Boadicea", akarudi July 18 hii.

July 22, Archdeacon Maples ameingia ndani ya meli kwenda Ulaya.

July 23, Mnazi Mmoja palikuwa na mchezo, Wazungu wa merikebuni walishuka kucheza mchezo wa vita. Watu wengi mno waliokusanyika kutazama, na njia kuu yote imejaa askari, na sisi watoto wa Kiungani tulikuwapo, na watoto wa Mbweni na watoto wa Miss Mills pia. Bassi mabaharia na askari wa merikebuni kama 700 walishuka kwa shangwi, tena ilisimamishwa milingoti miwili kwa bandera, mmoja wa Mwingereza na wapili wa Seyid Ali. Balyozi alikuja na Seyid Ali pia, mizinga ya salamu ikapigwa. Halafu mchezo ukaisha.

July 25, Bwana Seyid Ali aliingia saa tatu asubui katika H.M.S. "Boadicea" kuitazama, merikebu zilitweka bandera nyingi, na mabaharia killa merikebu walipanda juu ya milingoti wakasimama sawa sawa juu ya formali. Seyid alipokuwa akienda merikebuni, merikebu zote zilipiga mizinga mingi, na alipopanda ndani ya H.M.S. "Boadicea" ikapigwa mizinga. Tena ndipo akaonyeshwa mambo yaliyomo, ya mizinga, na "Torpedo" ya kuvunja merikebu ao kuung'oa kwamba, bwana, maji yaliruka juu sana. Na sisi wa Kiungani, Mkunazini na Mbweni, tulikaa penyi baraza ya barozi mkubwa tukiangalia mambo yatendekayo.

Hatta saa tano Seyid Ali alishuka na mizinga ikapigwa tena. Wakati wa kurudi Bibi wa barozi mkubwa alitupa machungwa na ndizi, kiisha tukarejea killa mtu mahali pake.

July 31, Mr. Viney na Mr. Allen wamewasili Unguja wakitoka Magila.

MSIMULIZI. 225

Barnabas Farajalla ameingia ndani ya H.M.S. "Conquest" kufanya kazi. Tena August 11, Alban Njengune ameingia ndani ya H.M.S. "Cossack" kufanya kazi. August 6 ilianza Examination hatta August 11 Juma a tatu, muda wa siku tatu urobo. Na walioshinda katika Darasa ya Waalimu ndio 1. Hugh S. Mtoka, 2. Hugh Mhina, 3. Samuel Sehoza. Katika Darasa ya pili, 1. Benedict Madolito, 2. Yustino Mkaodu. Katika Darasa ya tatu, 1. Tito Kungulukutu, 2. Kolumba Msigala. Katika Darasa ya nne 1. L. Mattiya Kangati, 2. Frederick Makwela.

Tena mwisho wa mwezi wa September tunatazamia Wazungu wanne kufika Unguja; Mr. Coupland, Mr. Lupton Taylor, Mr. King, na Mr. Dalebrook (wa Oxford) na pamoja nao Mr. Salfey aliye Kasisi sasa. Mtg.

NJIA YA MAGARI YA MOSHI KWA VICTORIA NYANZA.

Juzi, Aug. 26, mambo makubwa yalianzishwa kule Mombasa. Kwani hao Wazungu, waliofanya Kampeni ile, ndio kama chama cha kufanyizia biashara kule, wamefanya shauri ya kujenga njia ya magari ya moshi tangu bandari mpya wa Mombasa kupita Kiliminjaro kufika Kavirono katika pwani wa Nyanza.

Bassi kazi hii kubwa sana ikazinduliwa kwa fahari juzi. Watu wengi Wazungu hatta Waarabu na Wahindi na wengine wakatoka Unguja, na Manowari nne za Wazungu na moja ya Wadachi na stima tatu ngine wakaja wakatia nanga pale katika bandari mpya ya Mombasa, siyo ile ya zamani penyi ngome lakini iliyo kubwa sana na nzuri zayidi kwenyi upande wa pili wa kisiwa cha Mombasa.

Bassi marikebu zote zikapambwa bandera nyingi, wakashuka watu wote penyi rasi iliyo karibu kabisa na

MSIMULIZI. 226

pwani lakini imeinuka juu, wakakusanyika wote, ndipo mkubwa wa Kampeni Sir Francis De Winton akamtakia Padre Mr. Binns wa C.M.S. kumwomba Muungu kwa wazi aibariki kazi hii inayoanzwa, kisha alimtaka Bibi Balyozi, kwani ndiye mwenyi heshima, kuanza kazi yenyewe.

Na kuianza ni kama hivi, kwa desturi ya Kizungu. Yule Bibi anapewa jembe jipya na kigari kidogo (wheelbarrow) akachimba marra moja kwa jembe akautia udongo garini akaendesha gari kidogo akalipindua. Bassi ndio kazi imeanzwa kwani kazi ya kuchimba na kusawazisha njia itaendelea tangu palepale hatta Nyanza!

Kisha Wazungu mia walikula karamu palepale katika hema, wakasema maneno mengi ya kuitakia mema kazi hii. Tukaambiwa na mkubwa wa kazi kama njia hii itawekwa tayari upesi sana, hatta kisha mtu ataweza kukaa katika gari la moshi na kufika Kavirondo toka Mombasa kwa siku mbili u nuss! Ajabu sana.

Bassi Wazungu wakiisha kula wanaona kama kazi imeendelea na kama wari hamsini ya vile vyumba zikalazwa na kuundwa tayari, na gari la kukalia ndani lipo, hatta akaingizwa Bibi Balyozi pamoja na wengine wakaendeshwa kupita juu yake. Watu wote wakapaliza sauti wakifurahi. Kisha killa mtu akarudi kwake. P.L.J.B.

MSIMULIZI. October, 1890. XIII.
Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,
katika "Universities' Mission to Central Africa."

HABARI ZA MAGILA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu kama katika Aug. 12 ilikuwa harusi ya mpishi wetu mmoja Yohana Kisasa, ilitawi kwa upande wake.

Katika August 17, Mwalimu Lawrence Kingodi alipata mtoto mume, bassi akabatizwa.

Aug. 19, Mr. Woodward akampeleka Sister Clara, Tanga, akapata kwenda Unguja, kwani hana afya; pamoja na Mwalimu Leonard Pesa, na Basil Mhada na Karlo Mwaimu, wamechukuliwa katika H.M.S. "Boadicea."

Katika siku kuu yetu ya Bartolomayo watu walifurahiwa sana, nayo ilitawi sana. Tulipamba kanisa letu kwa uzuri sana juma a mosi na siku hii jioni akaja mwalimu Martin Furahani na watoto wake wa Misozwe. Assubui yake sala ya Usharika Mtakatifu na sala ya pili, tulifurahiwa sana sana, kwani kanisa letu lilijaa watu kuliko siku zingine. Bassi juma a tatu yake ilikuwa karamu na michezo kwa watoto waume. Hema na vitu vya kushindania vikapelekwa boondeni tunapochezea mpila. Killa namna ya kushindana watu walifanyiza; bassi watu walianza assubui. Hawa washindana kupiga mishale, kukimbia, kuvutana kamba, na manginge mengi watu walishindana wapate zawadi: bassi ilipotimia athuuri tukarudi nyumbani. Watu wakala karamu yao, wakala wali na ng'ombe hatta kuchoka. Alasiri tarumbeta ikalia, ndio ya watu waende kushindana mpila, watoto wa chuoni, na watu wa kazi. Watu wengi sana walikuwapo, bassi walioshinda ni watoto wa chuoni, tukawapigia makofi. Tena ikawa mashindano manginge manginge kama ya assubui. Siku ya pili juma a nne watoto wote wa chuoni wakapewa

MSIMULIZI. 228

ruhusa kwenda kwao, wacheze kwa juma mbili. Bassi usiku wake hawakulala kwa furaha iliyowapata, huogea tu, hatta ukiwazuia utaona wakichekacheka wasiweze kuvumilia. Na siku hii ilikuwa karamu na michezo kwa watoto waanake wajao kusoma, walifanyiziwa na 'Sisters'. Wengi sana walikuja, zayidi ya 50. Wao walishindaniana hapa hapa nyumbani: Walishindania zawadi tangu asubui mpaka athuuri, tena baadaye wakala karamu yao.

Katika Aug 26. Mr. Dale akaenda Mkuzi kuwafanyizia siku kuu watu wa Mkuzi.

Aug. 27 Mr. Woodward akaenda kuwafanyizia siku kuu watu wa Misozwe.

Bassi siku kuu hii ilikuwa mtawanyiko tu, Magila ikawa kama si Magila ginsi watu walivyotaka. Mr. Roberts akaenda kumwambia Mdachi wa Minyuani upande wa Zigua kidogo pamoja na waalimu akiwa Manfred na Herbert Feruzi. Tena wakaenda Msalaka kwa siku kuu, kule walifanyiziwa na Mr. Woodward. Tena wakaenda Pangani kutembea, bassi juma mbili watu hutembea tu huku na huku.

Katika Sept. 6, Watoto wakarudi, ilikuwa siku ya furaha sana kuonana tena, wengine wakarudi alasiri, wengine jioni.

Sept. 8, Mwalimu Hugh B. Mteka na Arthur Mvenya walitoka hapa alasiri wakaenda Unguja, kwani walikuja kutembea kwa mwezi. Sept. 9, Mwalimu Lewis Bondo akaja hapa na watoto wake, waume na wake wengi sana, walikuja kupewa waume visibau na nguo, na waanake mateitei. "School" ya mwalimu huyu Lewis inastawi sana kule Mlembule, waume na wake, nathani zayidi ya Watu 50 anaopata, naye peke yake, na sasa tumewapata watoto wawili wakukaa hapa Magila, kwani wamepita wenzao. Katika Sept. 14, Ilikuwa siku kuu yetu ya Kanisa la Magila, liitwalo "Holy Cross" Msalaba Mtakatifu,

MSIMULIZI. 229

lilipambwa vizuri sana, na watu wengi walioingia wakafurahia kanisa. Assubui yake juma a tatu watoto wote tulienda kushinda, mlimani Seluka, tukifurahia hii siku kuu ya kanisa letu; tulichukua kondoo na mchele huko huko, tukala jioni tukarudi.

Tena bwana wa Msimulizi nataka kukuambia kama sisi huku tuna huzuni sana, kwani Wamasihiya wengi sana wanakaa Tanga na Pangani na Minyulani (upande wa Zigua), wakifanya kazi Hatta ndio maana hatupati watoto wengi wakae katika miji yetu. Upelekwa watu waenda wengi wengi kufanya kazi; bassi kazi yetu kama inazuilika kidogo lakini hatujui baadaye nathani tutastawi sana. J.B.M.

HABARI ZA MSARAKA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salaam. Baada ya salaam Ninakuarifu habari za siku kuu yetu ya Bartolomayo, siku ya August 23 kwa jioni yake nilikwenda zangu Magila Juma a tatu August 28 twalishindana kule, palikuwa namna nyingi za michezo, ninathani Mletaji habari wa Magila atakuhadithia vema. Juma a nne ndio August 26 nilistarehe huko Magila, Jumaatano August 27 nilikwenda Misozwe kumwamkia mwalimu Martin na mkewe, Alhamisi nilirejea Magila Ijumaa niliamkia Gulio (sokoni); kutafuta mbuzi kwa karamu ya watoto wa Chuoni. Bassi nilinunua mbuzi wawili.

Bassi August 30 ndipo alipokuja Bwana M. Woodward, Mr. Roberts pamoja na watoto, walishinda hapa Msalaka Juma a tatu ndiyo siku ya karamu, Sept. 12 Lakini twalifanya hivi, wanaume siku yao ilikuwa Juma a tatu, wanawake Juma a nne. Bassi wanaume walitumia wali na nyama hatta walishindwa, na mashindano yalikuwapo, mshindano wa kwanza kukimbia kwa kanzu, kwa ao kisibao.

MSIMULIZI. 300

Shindano la pili kutia fimbo karibu na pua na kufumba macho uzunguke marra sita, ukiisha ufunue macho na kukimbia upesi kupiga mti uliosimamishwa katikati, akiupiga atapewa zawadi. Lakini watoto wengi walioshindwa kwani walipokuwa wakifunua macho hawawezi kwenda sawa sawa walikuwa wakionekana kama walevi kwa kizunguzungu, mchezo wa tatu upande mmoja kuwekwa mawe thenashara na upande mwingine kathalika mawe thenashara, bassi watu wawili wataanza pamoja na atakaye kwisha upesi mawe ya upande wake ndiye aliyeshinda.

Juma a nne Sept. 2, ndiyo karamu ya wanawake na machezo yalikuwapo kushindana ushanga na kofia. Waliokuja kuwafanyia karamu Sisters wawili.

Sept. 5 hatta Sept. 6 tumepata uthia mkuu kwa Simba, zayidi hapa mahali pangu alikuja hatta kukaribia nyumba yangu. Bassi marra moyo walinihukumu kumpigia bunduki, lakini kwa sababu ya giza sikumwona vema nilipiga tu. Bassi ilikuwa kama nitemzidisha ukali. Assubui Wabondei walikuja kuniuliza kama nitempiga nikawaambia nitemkosa. Bassi siku hizi ni shidda sana huku kutembea usiku usiku kwani mchana hao simba hawaendi mbali, na jua likiisha kuchwa, panapo saa ya kwanza tu ndipo wanapoanza kunguruma, bassi hatujui mwisho wao. Juma a tatu ndiyo Sept. 1 kwa sala ya jioni Bwana Mr. Woodward alifanya waanafunzi watatu hapa Msaraka mwanaume mmoja, waanawake wawili; majina yao ni haya Wantia, Mamkuzu, Patani. Nao ndiyo watu wanaongojea nyumba zetu za Umba. G.K.

SAFARI TOKA YERUSALEMI HATTA DAMESKI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu ya kwamba barua yako imeniwasilia

MSIMULIZI. 301

huko Ulaya, asante. Wanitaka niandike habari za safari yetu toka Yerusalemi hatta Dameski, bassi nitajaribu. Twalitoka Yerusalemi Apr. 21, 1890 pamoja nami bibi yangu na mabibi wangine saba. Killa mtu na frasi wake illa Mrs Hodgson naye akachukuliwa na palankini, tena hema tano, nyumbu tele na watumishi wengi wenyi mkubwa mmoja, kiongozi ndiye aliyekwitwa Dragoman, msafara mkubwa bass. Huwatunza sana wasafiri katika inchi hii huwafanyizia chakula chema malalo mema killa kitu kizuri, illa kitu kimoja tu, ndio njia nazo mbaya sana, kwani inchi yote milima na mawe matupu. Bassi kwenda pole pole tu dayima hatta wasioweza kupanda frasi waweza huko marithawa. Labda kwenda kwake siku ya kwanza na siku ya pili kubaya kupita zote wala bado kuzoea. Marra kwa marra njia kama mto usio na maji, mawe mengi sana frasi hutiririka tu. Killa siku hufanya safari, assubui na mapema tukiisha kula tu, huenda mpaka athuuri ao saa tano, wenyi hema na chakula wametangulia, bassi huona tayari, hulala, hula, hupumzika saa mbili halafu huenda tena mpaka saa kumi. Saa edashara ndipo hukuta matuo yamekwisha kutengenezwa, chai tayari, na chakula kimepikwa.

Siku ile ya kwanza twalika athuuri Beeroth, ndipo husema wazee wake wameona Mtoto Mtakatifu amepotea (Luka II. 44). Nikapanda kilima karibu Gibe ya Saul, Twalienda wee milimani milima tu mpaka kutwa. Tukachoka sana, jua kali miti hapana, mawe na mawe tu. Mahali pa kwanza tulipotua kijiji cha siku hizi tu, jina lake Sinjil pazuri lakini. Tukaalala vyema sana. Assubuhi wangine wakazunguka kwa Shilo maanguko tu sisi wangine tukakaa tukatoka inchi ya Benyamini, tukaingia inchi ya Efraim saa nyingi kuzunguka mlima

MSIMULIZI 332

mle mkubwa Gerizim hatta alasiri tukashuka, tukatazama kile kisima cha Suchar Bwana alipokutana na mwanamke wa Samaria. Hapana shaka kisima kile kile Bado kidogo kuingia boonde kati ya Gerizim wa Ebal kuzunguka Nablous, ndio Shechem wa zamani, ndipo tulipotua siku ya pili.

Tukiisha kushuka tukaingia mjini tukatembea. Mji mkubwa, watu tele, tena watoto wazuri mno kuna Sunagogi ya Wasamaria huko nami nikaenda dukani kununua viatu vya inchi. Maili mengi nimekwenda kwa miguu, kwani sipandi frasi mno, hatta viatu vyangu vimekwisha kwa ile milima na mawe. Nikapata viatu vyekundu (Turkish Slippers) vikanitoshia mpaka Dameski, maili kumi hamstashara killa siku. Hatta siku ya tatu tukapita vijito, maji tele, halafu kupanda milima tena ndipo bibi mmoja karibu kuumizwa sana. Kulikuwa na kipunda anatembea na mzigo wake kamba ikafunguka naye alipomkaribia frasi ya bibi frasi akapiga teke, mguu wake ukanaswa na ile kamba wote wakapiga teke sana, wakazidi kufungamana, mpaka walipoanguka wakifingirika pamoja bibi na frasi na punda wala hakuumizwa akatoka salama.

Halafu tukaingia mji wa Samaria sasa maanguko, nguzo na vibanda tu tena tukapita Yezreel sasa kijiji na taka taka tu. Mawe ya pande hizi mazuri sana. Alasiri tukapita boonde ya Dothan shayiri tele tukaona kijiji cha Dothan, hatta jioni tukatua Jenen (Aingamim.) Huu ni mji kwa upande wa inchi sawa ya Ezdraelon. Ndiyo tuliyoipita siku ya pili yake nayo imelimwa yote. Ngano na shayiri tele. Bassi hii tukafika mapema alasiri mahali mashuhuri sana. Nazareti kwanza kutoka ile inchi sawa kupanda milima kidogo mna mji kama shimoni kwa juu milima pande zote. Ndipo huona Karmel na

MSIMULIZI. 333

Bahari. Mji, haikosi, pale pale alipotembea zamani Kijana Isa lakini nyumba zake na majengo ya siku hizi tu. Nikaitembea sana milimani karibu.

Keshoye tukaenda unussa kupanda mlima Tabor, vema kupita njia sawa kwa Kana ya Galilaya ule mlima Tabor si mrefu sana, lakini unapanda peke yake katika ile inchi sawa ya Ezdraelon bassi huonekana sana. Tena juu yake miti, mieloni, wala mpaka hapa shidda kuona mti wo wote. Tukapanda kwa frasi, tukarudi kwa miguu halafu tukakutana na wenzetu kwenyi mlima laini wa majani. ndipo alipohubiri Bwana maneno yale yote ya Matt-v, vi. vii. Tukaendelea kidogo tukaona kitu kizuri kuliko tulivyoviona vyote inchini Ziwa la Genezereti ziwa zuri kweli maji yake rangi ya mbingu tu milima mizuri pande zote tukapendezwa mno. Hatta jioni tukapita mji wa Tiberia, tukatua karibu kama kutoka mjini hatta Kiinua Mguu pwani kabisa karibu na maji, tukakuta huko maua kama yale ya Unguja Oleanders. Jioni tena assubuhi huoga majini maji ya baridi,

Assubuhi, Juma a mosi Apr. 26 tukaenda mji ule wa Tiberia, wala sio mji mzuri sana pana siku tena wa hari mno. Tukaingia mashuani tukavuka kaskazini mpaka maanguko ya Kapernaum wala hapana jiwe juu ya jiwe lakini mawe ya Sunagogi hatta sasa yaonekana maguguni. Tukashuka tena kidogo hatta Ain-et-Tini labda Betsaida wa zamani - wala hapo hapana nyumba yo yote sasa. Mahali pazuri tu, na kijito ndipo tulipotua tukikaa kitako Juma a pili. Juma a tatu tukasafiri tena juu ya milima ya Naftali kupita maji ya Merom nayo haba kama maziwa nyuma ya Kiungani tu, hatta vijito vya juu vya Yardani, tukatua Ainbalata. Nyati tele pande hizo.

MSIMULIZI. 334

Juma a 'nne tukakaa aththuuri kijiji kile cha kaskazini kabisa, Dan; tukatoka Palestino, tukaingia Syria (Sham) jioni tukatua Barias (Nao Kaisaria Filippi) hapa labda Bwana alipong'aa mbele ya wale watatu mlimani, kuna gereza ya zamani juu sana nikapanda kulitazama. Juma a tano tukapita, mlima Hermon tukapanda juu sana, njia mbaya, tukaona theluji hatimaye tukashuka kidogo Hauron tukakaa Kefr. Harun. Assubuhi yake tukapita inchi ya nyika juu kali sana: tukawa pahali alipoanguka Paolo kwenyi njia pande. Tukaingia "Oasis" miti tele, mijozi na mingine ya matunda vijito pande zote, na kati kati mji ule wa zamani kupita yote Dameski ukubwa wake kupita Unguja nyumba za mawe kubwa. Tena nzuri moskiti na minara tele sana. Mito inapita kati yake, kama zamani.

Huko bibi mmoja akaugua homa, tukamchukua hatta baharini (Beyrut) Juma a mosi May 3 nayo njia ipitayo juu ya Lebanon nzuri kupita njia zote nijuazo, kama njia yetu ya Mbweni shambani. Tukafika vizuri kwa gari kubwa siku ile ile frasi sita - kupokezana marra kumi na tatu kwenda kwenda tu saa thelitashara. Wala hatukuchoka, tukathania sote tumeona mambo ya kutufikirisha maisha pia. Wote tukawa hatujambo illa yule mmoja, naye akaugua Iskandaria, akapona baharini. F. R. Hodgson.

**HABARI ZA KUTUFIKIA KIUNGANI SAMWIL NAGANAFU
JUMBE WA UGANDA.**

Tulisikia kama majumbe wawili wa Uganda wamekuja Unguja nao wote ni Wamasihya, wameleta barua itokayo kwa mfalme Mwanga. Bassi tukaarifiwa ya kwamba Jumbe mmoja atakuja hapa Kiungani siku ya Juma amosi; nasi tukawa na shauko mno ya kumwona.

MSIMULIZI. 335

September 20, Juma amosi jioni saa thenashara unussu, majira hayo tunaingia kanisani kusali, marra tukasikia kama yule Jumbe amefika pamoja na watu wake wawili; huyu jumbe jina lake Samwil Naganafa. Hurrah! Hurrah! tukawasalimia na kuwaamkia kwa furaha kubwa sana sana, kiisha tukaenda mezani, tulipokwisha tukawa watu wa kutamani sana kusikia habari zao na za Uganda za ndugu zetu Wamasihya waliouawa kwa ajili yake Isa Masiya. Ilipotimia saa kwanza unussu Archdeacon Jones-Bateman alimleta Samwil Naganafa Sebuleni (Library,) Mr. Matthews na Mr. Viney walikuwapo, tena na waalimu wote tulikuwapo bassi akatuarifu hahari. Zamani huyu Samwil alipokuwa mtoto, alikuwa mtumishi wa mfalme Mtesa na alikuwa akienda kusoma kwa Wazungu killa siku. Hatta alipokwisha kufa Mtesa, akamiliki mwanawe huyu wa sasa ndiye Mwanga. Bassi huyu Samwil akasema, afathali nitoroke katika jumba la mfalme, akatoroka, akawa akifundishwa na Wazungu. Bassi Mfalme Mwanga akasema, Nakumbuka zamani za babangu Mtesa, palikuwa na kijana akimtumikia babangu, marra akaenda letwa.

Alitumwa na mfalme Mwanga apeleke ng'ombe 50 kwa mfalme mgine, kumbe huku nyuma mfalme akawakamata watoto wasemao wengi sana akawachoma. Huyu Samwil alikuwa tayari naye kuuawa, lakini kwa rehemu za Bwana wetu amepona.

Marra kwa marra aliwasumbua Wamasihya kwa kuwatumikisha magumu, kuchimba ziwa katika inchi kavu, siku ya Juma a pili pia. Hatta Mwanga akafanya shauri la kuwaua kwa njaa kwa kuwashindisha pasipo chakula kisiwani; lakini shauri lake baya likajulika nao, asilitimize hatta kidogo. Tena Waislamu wengi sana waliokuwa Uganda, bassi

MSIMULIZI 336

wakatoa shauri wapatane wamfukuze Mwanga bassi walimfukuza Mwanga akammilikisha Mwanawo Kiwewa. Bassi Waislamu wakafanya fitina mbaya, wakamwambia mfalme Kiwewa, Angalia, wale Wazungu wanawaambia wafuasi wao kama afathali wakupige wewe, kiisha wampe ufalme Mwanamke bibi yake Mtesa, kwani Ulaya mfalme wao Wazungu ni Mwanamke, wanatawaliwa na malkiya (Queen Victoria). Mfalme akawasadiki Waislamu, bassi akaleta vita juu ya Wamasihya, bassi Wamasihya wakakimbilia Unyoro wakakaa watu zayidi 2000 na zayidi.

Kumbe Waislamu halafu wakamgeukia mfalme Kiwewa wakapigana naye wakamishika Kalewa, ndipo mfalme alijuta, akasema, Naona Wamasihya wamesingiziwa tu.

Marra Wamashiya wakapata habari kama Mr. Stanley anapita Uganda. Naye Mr. Stanley aliwaona Wamasihya wako nyikani ndani ya vibanda, wanasoma Anjili, bassi akaingiwa na shangao. Bassi wakamwendea wakampasha habari ya taabu yao, na juu yote wakaomba msaada awasayidie. Bassi akawasayidia akawapa bunduki na watu wake pia wakaingia vitani, bassi Mwanga alipoona ule msaada naye akafanya nguvu. Akaamuru Waarabu wakamatwe wote, wakakamatwa, bassi akaamuru wakauawa.

Bassi tena mfalme Mwanga na Waganda Wamasihya wakafurahiwa, bassi ndipo Mwanga akajiapia kama hawataki tena Waislamu katika ufalme wake, illa anataka Wazungu tu. Mfalme akawa Mmasihya akabatizwa na mapadre wa Kifaransa, na watu wote wakuu na wadogo walipomwona Mfalme amekawa Mmasihya, wote pia nao wamekuwa Wamasihya.

Huyu Samwil Naganafa ni Mmasihya amebatizwa tu, lakini bado kutiwa mikono, kwani pande za Uganda hajafika bado Askofu, Lakini mtu huyu ametenda kazi nyingi ya kuwafundisha watu wake habari njema ya Bwana

MSIMULIZI. 337

wetu Isa Masiya. Marra kwa marra wakitiwa ufukuzo Wamasihiya yee ni tayari kumwungama Mwokozi wetu na tayari kwa kumshika Yee tu. Hata pengine mfalme anapotoa amri kali kwa Wamasihiya wakamatwe wachomwe moto, huyu Samwil huenda na kuwafariji Wamasihiya wawe na imani imara wala wasiwe na hofu. Bassi mwezi huu September 20 ametufikia hapa Kiungani akakaa kidogo tu hata Sep. 22 tukamwaga, akaenda mjini akaingia ndani ya Henry Wright pamoja na watu wake. Lakini baharini wakapatikana na tufano karibu kuzama, wakarejea hapa Unguja tena. Bassi September 28 ameingia ndani ya meli amesafiri Mvita. Mtg.

HABARI ZA NEWALA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu kama hapa Newala wapo watoto wanaokuja kusoma, hata na wengine wamekwenda kusoma katika Koleji ya Andrea Mtakatifu. Tena Luka Lichinga amesafiri Yao kwa Mtarika babuye kwenda kutembea. Tena mtu mmoja wa hapa naye Mwakua, jina lake Mripa, amefariki. Katika habari zile nilizokwenda Rovuma, niliandika jina moja la mahali paitwapo Mkitama. Bassi nitakuarifu habari zilizotukia mahali hapo. Siku moja Petro Mbika, Tembe na Msonde, na watu wengine walienenda kuwinda nyama, Bassi wakamkuta nyati, Petro akampiga bunduki lakini alimwumiza tu, bassi nyati kwa uchungu wa risasi akaenda kassi akakimbia, lakini watu wakamfuata. Bassi huyu Tembe na Msonde wakamfuata hata wakamkaribia, na Tembe ndiye aliyemtangulia mwenyewe. Bassi nyati akamwandama Tembe, hata Tembe akakuta gogo kubwa; kumbe na nyati naye aja zake kassi upande wa pili wa gogo, Tembe akaanguka na nyati pia akaanguka penyi gogo. Bassi Tembe alipoamka aliacha bunduki yake, nguo,

MSIMULIZI 338

kisu chake, akakimbia akaufikia mti akaupanda, na Msonde pia akapanda juu ya mti, Marra akatokea Petro Mbika akamua yule nyati, na wale walio juu ya mti wakashuka. Walipoendelea mbele wakamkuta mzee tembo, Petro akampiga risasi mbili akaanguka amekufa. Wakaja watu wakamchukua hatta mjini, ikawa furaha sana. E.M.

HABARI ZA MLOLELA AO CHITANGALI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu maneno haya,

Tumepata furaha sana kwa kuendelea habari ya dini ya Kimasihiya. July 27, Juma a pili ya kenda baada ya Pentekote, wamefanywa Waanafunzi asharini na mbili, waume edashara na waanawake edashara. Siku kuu ya Bartolomayo tulifurahiwa sana sana, tulicheza kwa furaha mno, watoto wa chuoni walitazamiwa kusoma (Examination). Katika darasa ya kwanza aliyeshinda 1. Augustino Malemla, 2. Alfred A. Mpetula, 3. Edward Sudi. Darasa ya pili aliyeshinda 1. Kalemwaga, 2. Oseni, 3. Kawanga. Tena watoto waanawake walitazamiwa kusoma. Darasa ya kwanza aliyeshinda 1. Amkolo, 2. Amtoto, 3. Chembole. Darasa ya pili aliyeshinda 1. Fayida, 2. Apasonje. Bassi watoto waume walioshinda walipewa zawadi, wangine rupia, pesa, kofia, na visibao. Tena nao watoto waanawake walioshinda katika kusoma walipewa zawadi, kama thiraa mbili ya lesa ao ushanga. Sisi hapa Mlolela tumepata furaha sana sana, kwa sababu Padre wetu wa hapa amepata barua itokayo Lulu kusini ya Afrika, ndiyo hii:

S. Marks, Kaffraria.

Kwa Reverend Cecil Majaliwa.

Mpenzi wangu Ndugu yangu katika Masiya, baada

MSIMULIZI. 339

ya kusoma habari za kuamuriwa kwako ya kwamba ndiwe Mwenyeji wa Afrika wa kwanza upande huo wa Mashariki aliyeingizwa katika Ukasisi wa Kanisa Katoliko.

Hatta tungawa hatujaonana, labda hatutaonana hapa ulimwenguni lakini katika Ufalme wake Muungu ndipo tutakapokutana mbele ya kiti cha Muungu cha upesi. Kwa hiyo ninasukumwa, ndugu yangu, kukupa mkono kwa furaha na upendo katika Uwito wako mkuu; upate kuwa kama "Nyota ya Assubui" maisha na hali yako kwa jamaa zako. Uwalete wengi kwa Masiya, wala hahitaji kusema siku ya kuinuliwa kwako kwa Mapokezano ya Mitume, itakumbukwa nasi walioiona. Maneno ya siku ile yaliyofaa sana kwa jambo lile Kufurahia kweli na kupendezwa nayo.

Salamu yangu na mahitaji yangu kwako Uzidi kufanikiwa. Mimi mwenyeji wako, Kasisi aliye mtu wa Afrika mwenyeji P. R. Masizu.

Habari kidogo za wenzetu wasafirio kwenda Nyassa.

Naona mtapenda kuzijua, kwani tumezipata katika barua aliyoandikiwa Mr. Madan. Ndiyo hii:

Kando la mto Zambezi, July 2, 1890.

Dear Mr. Madan,

Tulipotoka Msumbiji tulifika Kilimeni June 24, Bwana Frere na Captain Sherriff wakaja mwenyi meli kutukuta sisi. Tukashushwa pwani marra moja pamoja na Wazungu wawindaji nyama waliotoka Msumbiji pamoja naswi; tukashinda siku moja, Alhamisi tukaenda kupakia mizigo yetu, assubui tukafanyiwa Siri takatifu.

MSIMULIZI. 440

Tukaingia mashuani, tukapatiwa killa mashua wawili wawili. Richard Kanyema na mkewe wakaingia katika mashua ya Mr. Frere na Captain Sherriff. Mimi na Anne Hathaway tukiingia mashua yetu ya chuma, na Philip E. Yahom na Clement Kathibeni wakaingia yao, tukaendelea hatta tukafika hapa salama. Mashua niliyoingia mimi na Anne Hathaway imechukuliwa sasa na watu 30 ipo hapa tayari kwa kwenda kesho Kilimeni.

Tulienda kuulizwa sisi wote kwa Governor na wazungu wetu pia. Twashukuru sana kwa sala zenu kwani hutumaini kama mwatuombea. Watu wanatuambia kama Wareno wamechukua mizinga minne kwenda Puo na stima mbili, lakini bado kuvuka Puo, ipo bendera yao. Labuda Bwana Archdeacon Maples atasumulia habari alizoandika Bwana Frere. Leo July 2, twalalia safari kesho July 3, tutapanda mto Zambezi; mto huu una mbu wengi nao wanatuuthi sana sana.

Wareno wanajitahidi kutuzuia tusipande, mashua ya Bwana Frere ilishikwa nao, lakini aliwaonyesha Cheti wakaiacha ikapita. Mimi mtoto wako, So Songolo.

HABARI ZA KIUNGANI.

August 13, Mr. Woodward alisafiri kwenda Bonde, pamoja naye walifuatana Hugh S. Mtoka, Arthur R. Mvenya na Nyange, aliingia ndani ya H.M.S. "Boadicea." Mr. Woodward alifuatana na Admeli mpaka Magila. August 21, Mwalimu Leonard Pesa, na Basil Mhada na Carlo Mwaimu wamefika Unguja wakitoka Magila, nao waliingia katika H.M.S. "Boadicea." Tumefurahi mno kuwaona.

MSIMULIZI 441

August 26 August 28, Archdeacon Jones-Bateman alirudi hapa. Siku hiyo ilikuwa siku ya Augustino wa Hippo, Askofu wa Afrika, bassi tulicheza siku nzima. Tena tulitia chokaa nyumba yetu. August 29, Ijumaa, tulipamba nyumba yetu sana tayari kwa Juma a mosi, kwani ndio siku ilipofanyika karamu ya Bartolomayo.

Habari za August 30, ndio siku ya karamu, na Seyidl Ali alikuja, habari.

Zimeandikwa chini kidogo. Sep J4, Mwalimu Hugh S. Mtoka na Arthur Mvenya, na mtoto mmoja Nyange wamerudi hapa Kiungani wakitoka Magila.

September 19, Ilikuwa siku ya faragha ya rohani (Retreat) kwa Chama cha Paolo Mtume, ilikuwa ya siku moja unussu. September 20, Mr. Bome amesafiri kwenda Magila pamoja na Mr. Brough. Tena Sep. 24, tumemsafirisha Mwalimu Hugh Mhina kwenda Magila. Sept. 30, meli ya Ulaya imekuja pamoja na wageni watatu, Mr. Salfey Padre wetu mweusi, na Mr. King na Mr. Dalebrook. Mr. King na Mr. Dalebrook wanakaa hapa Kiungani, na. Bwana Salfey anaenda Magila. Mtg.

HABARI ZA KUTUJIA SEYID ALI.

Mr. Matthews na watoto wake walikuwa wakitengeneza nyumba, kufagia, na Mr. Madan pia alifanyiza merikebu nayo nzuri, kupita zote tulizofanyiza miaka iliyopita. Ikatiwa mizinga minne. Ikatiwa bandera nyekundu mbavuni mwake na chini yake ikatiwa bati nyingi ndio bahari, na juu ya milingoti zikatiwa bandera. Zingine zikatiwa tangu mwanzo wa mpaka, na makuti pia tukapamba. Tena baharia wengi wa manowarini, wakaleta hema, na bandera wakaja nazo. Wakajenga hema barazani kubwa sana na mlangoni, bandera kubwa zikapambwa mitini, zingine zikapambwa tangu dari ya kengele hatta dari ya Kanisa

MSIMULIZI. 442

letu. Tena mstarini tukapamba kwa makuti, na bandera nyingi, na kutengeneza killa mahali, siku zile. Juma a mosi Aug. 30 ndiyo siku kuu yenyewe, watu wengi sana walikusanyika, watoto wa Mbweni pamoja na mabibi yao, hatta kondeni pia walikuja siku hiyo, ndio waliokwisha kuoa. Wazungu wengi walikuwapo, Balyozi Mwingreza na Balyozi Mdoicha, kwani wote waliitwa kwa sababu ya Mfalme atakayekuja. Akaleta Nahotha wa "Boadicea" mdundo wake, kusudi wampigie Seyidi Ali. Bassi alikuja hapa saa 11, marra akatokea aliyetangulia mpanda frasi, kuangalia kidogo marra mwenyewe akatokea tukampigia Hurrah! marra tatu. Tukamkaribisha ndani pamoja na na Waarabu wake. Watoto wangine wakaenda uani kwenyi merikebu yetu. Waalimu walisimama mlangoni, mwandishi mtumishi wa Balyozi. Kwanza kahawa, akampelekea hakunywa sana kidogo tu, kiti alichokalia ni cha Balyozi wa Kiingreza. Tena akapelekewa sharbati, marra alipokwisha kunywa wote wakatoka, kumwonyesha Bwana killa pahali. Tukamwonyesha Kanisa letu. Tena akaenda chumba cha kupiga chapa. Tena kule iliandikwa maneno ya kumsifu. Tena akampa kujaribia mwenyewe kwa mkono wake akapiga. Tena wale watoto wanne wenyi kupiga mizinga wakaenda. Alipokwisha kutoka akasimama akiitazama merikebu ile tulioijenga, kapigiwa mizinga 21 heshima yake. Akatoka, ndio moja kwa moja akaingia katika gari lake tukampigia vile vile Hurrah! kama kwanza. Wakaupiga mdundo, wakapiga weee. Tena killa mtu akashika njia yake. A.T.M.

MSIMULIZI. December, 1890. XIV.

Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,

KATIKA "UNIVERSITIES' MISSION TO CENTRAL AFRICA."

HADITHI.

Kuna sehemu kubwa ya dunia hii yenyi watu na miji na mathehebu za kustaajabisha watu wengine waliozaliwa katika ustaarabu, hatta kuwachekesha watu wakitazama sanamu za miji yao na mashujaa wao, na safari zao za namna mbali mbali, za mitoni na barani. Na mavazi yao pia huchekeka sana, kwani pengine huvaa ngozi kidogo, pengine nguo ta mti na majani, pengine mtu mzima mzee mkongwe mwenyi mvi hutenda kama angalikuwa nyama asiyejua kuona haya; kwani tangu siku ya kuzaliwa kwake hatta siku ya kufa kwake, hajapata hatta siku moja kujifunika nguo maungoni; hatta hapana tafauti na nyama illa labuda kwa kuwa ana roho tu.

Sasa sikilizeni hadithi inakwitwa,

USHUJAA WA MZEE TUMBO TUMBO Na Mr. Money-Liker.

Palikuwa na Mfalme jina lake Tumbo Tumbo, katika inchi ya Wamasai. Mwenyi mji wake si mkubwa sana kadri ya nyumba 200, lakini majumba yake makubwa sana, tena yamekaa mbali mbali, hivyo mji wake waonekana kuwa mkubwa sana. Wallakini angalia mji huu wa mfalme kweli naye mshujaa sana kwa vita, lakini, Ah! ushenzi si kitu chema kabisa, sikia nitakuhadithia mathehebu yao watu hawa na mji wao Nafaka.

Kwanza mji wao hauna ngome, umejengwa pahali peupe, napo juu ya kilima, kwani inchi yake haina misitu mikubwa, kama ya inchi zingine za barra. Majengo yao?

Ah! ajabu hiyo ginsi watu hao wanavyoweza kulala katika nyumba hizo na kupata usingizi mtamu kama katika nyumba za mawe zenye madirisha na mikeka na mito, na magodoro na chandarua. Kwani nyumba za watu hawa za miti, ukuta wake si mrefu sana kadri kimo cha mtu aliye wastani; nazo zimeviringana tangu ukuta wa chini hatta

MSIMULIZI, 1890
Imepigwa chapa Kiungani, Zanzibar,
katika "Universities' Mission to Central Africa."

paa lake la juu. Hazina dirisha illa mlango mdogo, hatta mtu akiingia sharti ainame kabisa-a-a chini.

MSIMULIZI. 344

Nao hukandika nyumba zao hatta hapana tundu hatta kidogo iwezayo kuvusha hewa nzuri katika nyumba hizi.

Hatta pengine wanatwaa mbolea ya ng'ombe wanazidi kukandika hatta ukuta unakuwa kama ubao kwa ginsi wanavyokandika kwa ustadi. Malalo yao je?

Ah! bwana ajabu hiyo kweli kweli; nathani mtu aliyestaarabu akilala usiku mmoja utamtosha asitake tena kulala usiku mwingine wala hatausahau usiku huu uliompitia kwa taabu na majuto makuu. Kwani watu hawa hulalia kitanda cha mito iliopangwa uzuri kama wafanyavyo wakianika nyama kwa moto, wala mkeka hapana. Na karibu na miguu yake pana jiko la moto kwani hawa hawatumii taa kama sisi waungwana. Na karibu na kitwa chake ndiyo mahali pa kufunga mbuzi zake. Bassi angalia nyumba hii haina dirisha wala kitundu kidogo, nayo ina moshi na jasho na manuka ya uchafu wa mbuzi. Ah! usingizi wa ajabu huu, nathani ukilala usiku pua huziba hatta pumzi huna. (Angalia sana sanamu ya kwanza) ndio namna za nyumba.

MSIMULIZI. 345

Hatta siku moja mfalme Tumbo Tumbo akaletewa habari kama mkewe na watoto wake wamekamatwa huko shamba. Marra mzee Tumbo Tumbo alipopata habari hii akaamuru goma la vita lipigwe, watu wakusanyike kuwakatizia njia adui wale waliomtwalia mkewe na wanawe. Wallakini kwa kuwa mzee Tumbo akisikia vita moyo wake unawaka kama lami iliyotiwa moto! Akaondoka akatwaa shime yake akajikaza kiunoni, akatwaa na nguo nyembamba ndefu akazungusha kiunoni (sio kuvaa, la! kuivingirisha tu, kwani watu hawa hawavai nguo kabisa), akatwaa na dude lililofanywa kwa ngozi na manyoya ya mbuni yaliyo marefu meusi akalivaa usoni. Akatwaa lingine limefanywa kwa manyoya mengi sana akalivaa shingoni.

Akatwaa nguo ndefu sana nyeupe iliyoshonewa nyekundu katikati akaiweka shingoni ikawa inapepea nyuma.

Akatwaa na ngozi za mbega mzuri, ndefu nyeupe, akazifunga miguuni, ngozi nyingine nyeusi akazifunga chini ya zile nyeupe, akatwaa mkuke wake mkubwa mweupe kama barafu, urefu wa chuma chake tu theraa 3,5 na mti wake theraa 2 na chuma kilichotiwa mwisho wa mkuke theraa 1,5. Akatwaa ngao yake kubwa uzito wake ratli kumi na tano. Akatwaa na tumbaku yake ya kunusa akafutika karibu na shime lake.

Akatoka mshujaa huyu thabiti. Naye alikuwa mtu mrefu kadri ya theraa nane unussu, pua yake kubwa hatta katika tundu za pua yake mtu anaweza kupenysha konde zima. Naye kwa kuwa na ghashu nyingi, hakungojea askari zake. Alitoka kassi akaenda mbio kassi kupita Bedui apandapo frasi. (Tazama sanamu ya pili).

Hatta alipowafikia adui zake alipigana kwa kiume na tisho kama simba aliyetwaliwa wanawe. Hatta watu wake walipokuja wakamsayidia wakawafukuza adui zao akatwaa mkewe na wanawe, akarudi kwake na shangwi kuu alichukuliwa

MSIMULIZI. 347

juu juu na mashujaa wake, na jina la mji wake ndio Nafaka. Akarejea akakaa raha kitambo.

Bassi Mzungu mmoja jina lake Mr. Money Liker naye ni mtu wa taifa la Waingreza. Alifunga safari yake kupita katika inchi ya mzee Tumbo Tumbo afike hatta ziwa Baringo; akatwaa wapagazi 220 Wanyamwezi pamoja na Waswahili, na kiongozi wake jina lake Wadi Nipe. Bassi walipokaribia katika miji ya rayia zake mzee Tumbo Tumbo, akapata baina kama kuna mfalme mweupe-e-e anakuja na askari zake wengi, na mfalme huyo macho yake yanang'aa kama paka, si meusi kama yako mzee Tumbo Tumbo.

Bassi mzee alipopata habari, akamwita mganga wake anayemtumainia kama anaweza kumtabiria mambo yo yote yajayo. Bassi yule mganga akaenda nyumbani kwake akavalia manyoya ya mbega shingoni mikononi na miguuni, na kiunoni akatwaa kibuyu chake cha dawa kimevikwa ushanga wa rangi zote, akatwaa na mkia wa simba akaufunga kitwani.

Akaingia nyumbani mwa mfalme saa saba ya usiku kama ilivyo kawaida yake siku zote. Akajilaza chini ya mvungu wa kitanda cha mzee. Hatta kama saa 11 ya alfajiri, akamwambia mzee Tumbo Tumbo,

"Ondoka upesi amuru goma la vita lipigwe upesi upesi, peleka watu hodari mashujaa, wallakini mwenyewe usiende kwani adui huyo Shetani (kwani ndivyo wanavyowaita watu weupe) anakaribia mto Rojeho."

Bassi Mzungu yule Mr. Money Liker alipopata baina ya mambo haya akafathaika sana kwani watu wale Waswahili waoga sana sana, wanaanza kuogopa ha kutetemeka mno kama si waume.

Bassi Mr. Money Liker akawaamuru watu wake wavuke mto Rujeho upesi upesi kabla watu wa mzee Tumbo Tumbo

MSIMULIZI 348

hawajawasili pale. Bassi watu wa Unguja kwa woga, hatta wengine wanaanguka ovyo katika ulalo (tazama sanamu ya tatu).

Bassi walipokwisha kuvuka mwendo wa saa mbili; watu wa mzee Tumbo Tumbo hawa wanatokea na wote wamevaa kengele ndogo ndogo miguuni zinalia sana wanapokimbia. Bassi Mr. Money Liker na watu wake walipoona haya walifathaika wakaanza kuchafuka, hatta Mzungu huyu asiweze kuwatuliza wala kuwazuia.

Kiongozi yule Wadi Nipe, akawalilia akasema "Kiume! Kiume! Simameni washenzi hao ndio wamekuja." Wallakini katika watu 220 wakasalia watu 186. Wakapigana kweli kweli, lakini, wapi bwana!

Ee washenzi wakali kama simba, Mzungu akatawanywa na watu wake pia. Mizigo yote ikatwaliwa hatta kwa mzee Tumbo Tumbo.

Mzungu yule kwa shidda sana pamoja na watu 16 wakafika ziwa Baringo, asitake kukaa ng'ambo ile kwani moyo wake umefathaika mno; kwa bahati na shidda akapata mtumbwi mbaya mbaya mrefu mwembamba sana. Akaingia pamoja na watu wake na washenzi wanne wakavuta mashua.

Hatta walipokuwa kati kati ya ziwa Baringo, washenzi wale wakavuta mashua na kuimba nyimbo zao za kishenzi, Lo-o-o! Mauti! kufa! watu wa Unguja wanalia mama wee tumekufa! Kwani Kiboko mkubwa alitokea akairusha mashua, na mtu wa Unguja mmoja kwa woga akataka ajitupe majihi. (Tazama sanamu ya nne) wallakini mshenzi mmoja mjasiri sana akatwaa kasia akalichoma kiboko lile jichoni, kwa uchungu yule kiboko akazama majini, watu wale wakazidi kuvuta wakafika pwani.

MSIMULIZI 350

Mzungu yule kwa shidda na majuto mengi, aliporudi kwao, akabadili jina lake akaitwa Mr. Money-Hater, hatta leo hivi.

Mwaona bassi ushujaa huo! na tamaa zisivyofaa? (kwani angalia jina la Mzungu huyu maana yake "Mpenda fetha"). S.S.

HABARI ZA MISOZWE.

Sept. 4, tukafanya karamu ya siku ya Mavuno, tukanunua mbuzi mkubwa sana hatta husemi ni ndama ya ng'ombe. Walikuja wake na vijana 42, waume na vijana 24. Alasiri yakawa mashindano kwa waume wazima na vijana, siku ya pili yake ndio 5 ya Sept. ilikuwa siku ya gulio Kisinga (gulio, ndipo soko watu wakusanyikapo) wakaja watu na michezo yao mle gulioni wakacheza ndio wa Kidanto na wa Willa wa mbugi tu.

Sept. 10 akaja Mdachi mmoja jina lake Mr. Flemming na wapagazi 12, mtu huyu wa upole na huruma sana kuliko Wadachi wote niliowaona, kwani alitaka kutoka wapagazi wengine wakatoroka! naye asiwafanye hatta neno lolote, hatta jioni walirudi wenyewe kwa kutaharika tu, tena akarudi zake Tanga.

Sept. 14, hatukuweza kulala usiku, siku hizo ilikuwa mvua mchana nayo kidogo tu, bassi usiku saa 3, nikiwa bado kufumba macho, loo! Nikasikia ghafula hiyo lio kubwa sana, la nyama, Simba mmoja ananguruma, Chui 2 wanalia pia na mafisi pia wanalia ndio hovyo tu usiku wote.

MSIMULIZI. 352

Sept. 12, akaja fisi usiku akavunja nyumba moja ya Mmasihiya jina lake Yohana Mganya, akatwaa kondoo, watu wakamfukuza wala wasimpate. Tena habari ya Imani na Matendo yake. Kuna kijana mwanamume mji wa Misozwe ndio mji wa zamani. Jina la kijana Benyamini Kiyama Mmasihiya, na ameo tangu siku nyingi zamani kidogo jina la mkewe Maryamu Mamhando. Marra ya kwanza wakapata mtoto, bassi wazazi wao wakasema, mtoto auawe, sababu mama yake hakuingia Kiwanga na mama na baba zao pia, (kiwanga ni mchezo mbaya sana) walakini wakakataa; walakini si na sibu yao mtoto kaitwa na Mwenyewe, akafariki, wakapata mtoto wa pili pia akafariki, sasa wamepata wa tatu, amebatizwa Juma a pili ya thenashara baada ya Pentekote. Mthamini wake Robert Makange (mwashi) jina la mtoto George.

Siku hizi Robert Makange na Andrew Yakuti waashi wapo hapa kwa jengo letu, vibarua wetu wanatoka wengi Magila, kwani wa hapa watu wavivu na wapendao thamani nyingi pasipo kutenda makuu, wapo wa Magila hawa, Simba, Msokelo, Sengaruwe, Sekakuli. Siku hizi twatumaini ya kwamba Wadachi watatu watutengenezea amani tupite vema, kumbe sivyo. Ilikuwa siku ya Gulio la Kisinga Sept. 29, nalikuwa humo mwenyewe nikaona ghafula watu wakienda kassi waume na wake na watoto. Killa mmoja niponye maisha yangu. Nikawatokea hima kwani nalikuwa kando ya kaskazini ya soko na shindo ilitokea kwa kusini, nikauliza, kuna nini? Nikaambiwa watu wa Wadachi Wanubi wanakuja.

Nikauliza wapi? nikajibiwa, njiani huko, ndio njia itokayo Magila, nikaendelea njia ile nisiwaone hatta mmoja, pamoja nami waume wengi, kumbe walisikia habari tu mtu aliyetoka chini kwa Pangani anasumulia wenziwe

MSIMULIZI 353

sokoni kwa nguvu sana, tukawazuia waume wengi na wake pia.

Kwani Wadachi wanaenda vitani juu kwa Wamasai wapita wakikamata watu wa kwenda nao vitani. Ah habari imeenea inchi nzima. October 8 nalienda nionane na watu mjini Mngaza pamoja na mtoto wa serkali petu jina la mtoto Mwangoto. Nami nimevaa kibandera na bwanda la kaniki, na mtoto kavaa nyeupe tu. Njiani nikakuta kijana mmoja mwenyi kuni kitwani akiniona tu akaenda vizuri kidogo kwani hapo tulikuwa peupe tu, hatta akafika majani nisipoweza kumwona loo, akaenda mbio sana akaacha njia akafuata mlimolimwa. Marra nikamwona nikafanya haraka yote nimitulize, nikamwambia, tulia utaumia visikini wee, Ah! nisimweze, nikaona anaelekea mjini, bassi nikamwambia wanikimbia burre tu, afathali ukifika mjini kwanza niwikie ugali akatoweka nisimwone tena ndani. Marra nikiingia mji nikakuta mwingine tena, naye mdogo wake kamweka chini, bassi akiniona tu akajaribu kumtwaa chini hataki, akalia, bassi akamwacha akakimbia kwa nyumba yao. Akichungulia aona sijafika vema akairudi tena amwokote akalia, akamwacha tena na wakati huo nikafika nikatazama katoto marra akaniona vile akaingia nyumbani, nikamwita asije. Nikaingia nyumba ya baraza la waume nikaongea sana nao, kiisha nikatoka nje ya baraza nikaanza kusema na wake, kwa kutafuta Girls kwa School.

Kwa nasibu yangu nikamwona yule aliyenikimbia njiani anichungulia yu nyumbani mwao. Bassi nikaenda nimwone nikaona na mama wake nikaongea sana naye akiniambia habari za binti yake alivyokimbia, baadaye akamwita kuja kunitazama, anijue. Ah, akawa na haya sana, nikauliza je! wapi ugali? akasema nasonga sasa ngoja tu. Nikasema haithuru siku ya pili nijaliwapo kuja tena, nikaagana nao nikatoka tena kwenda. Ah! inchi yote mioyo yao juu

MSIMULIZI 354

juu kwani wale wangine wa Wadachi hawaangalii ya inchi hatta inchi yote ina hofu tu. Kwani labda mtasikia ya habari ya Msaraka ginsi walivyofanya, mmoja wao aitwa Dr. Banman namjua sana, mahali pakutengeneza ndio kuharibu. George Kanakwahu akafika hapa October 8 anawakimbia Wadachi waendao vitani.

Oct. 5 usiku wake hatukulala vema, wakaja simba wawili jike na dume na mdogo wao mwana simba wakafika mjini Hemkole, ndio mji chini ya kilima chetu kwa mashariki, zikazunguka sana nje ya mji na kunguruma pia, zalifika kama, saa 8 za usiku saa 10.30 zikatoka hatta zilinguruma saa 11.30 asubui, zikienda zao zikafika juu ya kilima kikanguruma sana, hatta watoto wangu walithani zipo ndani ya mwitu karibu yetu.

Siku zilizo tangu September 15 hatta leo October 5 jua likichwa ni malio ya simba tu M.F.

HABARI ZA MKUZI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi Salamu.

Aug. 24 Siku kuu Bartolomayo imetufikia siku ya mavuno Juma a pili. Kasisi wetu Mr. Dale naye amekuja kukaa hapa.

Aug. 27 Juma a tano tukafanya karamu kubwa kwa watu wote siku ile ya furaha sana kwetu; Assubui ulikuwa Usharika Mtakatifu kwa Wamasihya karibu wote waliokuja kwa Usharika assubuhi. Saa tatu unusu sala ya pili ya watu wote, Kanisa likajaa sana waume na waanake pia. Wakaleta mihindi na mtama kwa kumshukuru Muungu kwa kuwa mavuno mengi mema.

Kwa karamu zikachinjwa mbuzi na kondoo jumla 2 ya wanaume, na siku ya pili karamu kwa wanawake. Bwana Mr. Dale akatoa zawadi nyingi kwa michezo mingine.

Mr. Allen amerudi, kutoka Unguja na punda wawili,

MSIMULIZI. 355

Aug. 28 yalikuwa karamu ya watoto waume na waanake, wakaja wengi sana siku hiyo; na bwana Mr. Dale akawahubiria kanisani, kuwauliza juu ya kuja kufundishwa mambo ya Muungu na kuja kusoma Chuoni killa siku.

Baada ya kanisani ikachinjwa mbuzi kwa karamu yao kikapikwa chakula wakala, baadaye ikawa michezo kwa zawadi.

Aug. 31 watoto wakapewa ruksa kwenda kwao kwa Juma moja, na mwalimu Henry alikwenda Pangani kutembea na mkewe Emma na Maryamu Swedi, alienda kupeleka bunduki zetu zote za hapa kupigwa chapa kwa Wadachi. Mimi nalikwenda kutembea Msaraka.

Kanisa letu linaanzwa kujengwa tena.

Sasa School ya watoto wanaume na ya waanawake waja siku hii kusoma, waanawake wanafundishwa na mkewe Mwalimu Henry Nasibu.

Tena sikitiko kuu sana sana kwa jambo la mtu aliyekuwa ndugu yetu, James Mwaimu, sasa amekubali nafsi yake mwenyewe kutengwa katika Kanisa na kushika Uislamu na kuwa na wanawake wawili.

Sept. 23, Mwalimu J. Swedi amefunga safari kwenda Zigua, sababu yake kumtafuta Arron Amwitamno aliyepotea utumwani wakati wa uthia wa Wadachi, twatumaini atakombolewa; akipatikana tena, kwani nyuma ana mkewe na mtoto wake.

Sept. 24, Mr. Bone na Mr. Brough wamekuja Bonde kukaa, Mr. Bonde kuwa bwana wa School ya Magila mahali pa Mr. Roberts anaenda zake kupumzika, na Mr. Brough kuwa bwana wa seremala mahali pa Mr. Ross aliyekwenda Unguja kwa ugonjwa.

Sept. 28, Mdachi Dr. Baumann na mwenziwe wamekuja

MSIMULIZI. 356

hapa wakafikia mji wa Mkuzi. Ilikuwa uthia sana watu waliokimbia msituni kujificha, na tena masikini wengi walikamatiwa kuku zao mjini bure na asikari. Ilikuwa siku ya Juma a pili, ilikuwa shida kupata watu wengi kuja kanisani kwa uthia huu.

Sept. 29, Ilikuwa siku kuu ya Mikael na Malaika zote, twalienda Kakindu kushinda huko watoto wote na kufanya karamu yetu pamoja na bwana Mr. Dale. Ilikuwa jua kali sana lakini twalifurahiwa sana huku tukarudi jioni, na bwana Mr. Dale akashikwa na homa ya siku tatu.

October 4, Mwalimu mkubwa John Swedi amerudi safari yake ya Zigua, illa hakuja naye Aaron Amwitamno sababu hawakumkuta hapo akaapo illa wameambiwa amekwenda Bagamoyo katumwa na bwana wake, akirudi wameahidiwa waende tena na fetha wachukue kwa ukombozi wake. C.L.

HABARI ZA MSARAKA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu.

Ninakuarifu habari kidogo iliyotokea upande wa huku kwetu, panapo Sept. 19, tulipata habari ya kuwa Bwana mkubwa wa Kidachi ndiye atawalaye Tanga yuko Mtanganta na Wanubi wake, pamoja na watu wamefungwa mnyororo anawakamata wapate kwenda kwa Wamasai.

Bassi kuamkia Juma a mosi ndio Sept. 20, panapo saa nane u nussu, niliona mwanamke mmoja akiniwasilia. Hamwuliza za Umba? Akaniambia Wadachi wamejaa.

Bassi wameniuliza yuko wapi Mwalimu anayekaa hapa, bassi tafathali twende zetu Umba. Bassi niliondoka nikaona ni kweli maneno yake mwanamke. Mji wetu umejaa wageni watupu, bassi niliwaamkia, nami nitazame marra hiyo Mdachi mmoja alikuwa na bastola yake, niliona anavizia kuku katika mji wetu pasipo kuuliza

MSIMULIZI. 357

na kupatana na mwenyi kuku, kuku alikoswa risasi marra mbili, kwa mwisho alimwacha. Bassi mji wa watu wa Umba usiku ulikuwa na kishindo kikubwa, kwani Wadachi wote watatu wakiingia ndani ya mji, tangu waanaume hatta waanawake walijitia msituni, mji wa Mmwachia jumbe Henry Semkali peke yake. Lakini waliponiona mimi ndani ya mji nimekaa pamoja na jumbe ndipo walianza kurudi. Nami niliwaambia, Ela nyinyi mtawakimbia Wadachi hatta lini nanyi mumo katika inchi yako. Jumbe aliniambia, Unajua hatta watu wanakimbia, ni kwa maana Wadachi hawa wa safari hii wamekuja kwa kishindo, kuku zetu zinapigwa marisasi, mayayi yanatwaliwa kwa nguvu, mitungi ya maji inatwaliwa; wenyewe wakikataa havifai hatta kidogo, minazi inapandwa ovyo, na safari nyingi zipitazo hapa halisi Bwana Herr Krenzler ndiyo njia yake anayopita anapotaka kwenda Magila kuwatazama Waingreza. Lakini sikupata kuyaona mambo kama haya.

Bassi hamwaambia Jumb, tafathali killa jambo wanalotaka uwapatie kwani hawa ni watu wa shari, halisi tena inchi ni yao, bassi hawana buddi watafanya vile wapendavyo wenyewe. Marra sijamaliza kusema na yule Jumbe, walitokea wale Wadachi wote watatu waliniuliza, Hapa ndiyo Umba halisi ao pana Umba ingine? hawajibu, Hii ndiyo Umba halisi; wakaniuliza, Wapi mtu mkubwa? hawaambia, Huyu hapa mliposimama. Wakamwambia, Haya mzee tunataka mbuzi zawadi, naye aliwajibu, Vema, ngojeni nifanye shauri na watoto wangu. Bassi alipowaambia maneno yale, walikasirika sana wale Wadachi walimwambia, Wewe mzee huna adabu, hatta sisi Wadachi tumekuja tangu asubui, hapa pako, njaa inatuuma na inchi ni yetu, sasa wasema tukungoje wewe na waanao mfanye shauri, siyo hatta kidogo! tunataka upesi upesi kungali mchana. Lakini ikitimia magaribi hatuna buddi

MSIMULIZI. 358

kukamata kwa nguvu chochote. Ndipo nilijaribu mimi kuwajibu, Afathali mpeni ruhusa kidogo. Bassi yule Jumbe akatazama akaona nisipowapatia mbuzi nitakuwa mashakani, bassi aliwapatia. Nami niliagana na yule Jumbe nikarejea kwangu Msaraka.

Juma a pili Sept. 21, saa ya kwanza nilipotaka kuruka kizingiti kusudi nitoke nje nikapige kengele ya kusali, nami niliona ugeni umekwisha kabisa kuniwasilia mlangoni na Jumbe wa Uмба wanaye. Marra tukaamkiana vizuri wakaniuliza, Mahali hapa panaitwaje? nikawaambia hapa ni Msalaka, wakaniambia, tunataka mtu wa kutupeleka Bwembwera, nikawajibu, ninaona itakuwa shidda sana kupatikana mtu.

Kaniambia kama watu wa hapa Msalaka hawatoki kutupatia mtu wa kutupeleka hatta Bwembwera, bassi huyu Jumbe Henry Semkali tutamchukua hatta tutakako. Bassi niliondoka na askari mmoja, nami nilifanya shauri nilimwambia yule askari, maneno haya, tukikaribia mlangoni wewe askari usiingie ndani ya mji kwani watu watakimbia, lakini shauri lile halikufaa hatta kidogo kwani walifanya nao akili moja waliweka mtu mlangoni, kusudi akiisha kuwaona tu askari akimbilie mjini kuwaambia wenziwe. Bassi ikawa nilipoingia ndani ya mji watu wamethania kuwa askari marra niliona watu waliomo ndani ya mji wawili watatu wote wamekwisha. Bassi nilimwendea jumbe nilimwambia, Wadachi wamemkamata jumbe Semkali bassi mkitaka arudi kwake Uмба sharti apatikane mmoja hapa, yule jumbe akajaribu kuwaambia watu wake lakini hakupatikana mtu. Bassi nikatoka hatta mlangoni pa mji nikamtwa yule askari tukaingia mji wa pili ndio Mkumbi nikawabembeleza wakataka kukataa, nami nikawaambia kama hamtaki kumpeleka huko atakako, haina buddi nitawaambia hapa ndani ya mji nanyi mpate mashaka kama

MSIMULIZI. 359

walivyopata watu wa Umba. Kwa maneno yale wakatazama ni kweli, jumbe wa mji ule akatoa watu wawili bassi kumbe mimi nikifanya vile wale Wadachi wanaona kukawiwa marra akaamrisha askari kuingia Msalaka kukamata watu wote wakajitia msituni lakini walimpata mtu mmoja naye mzee sana kwenda kwake kwa matata, Semkali na Jamaka, walisema, yatosha hawa wazee wawili watatupeleka safari yetu.

Nami kuwa ninarejea na wale watu wawili niliopata marra nilikutana nao wale Wadachi na askari zao na wale wazee wamo katika safari, yule mzee wa Msalaka ndiye Semkali amepewa kushika bandera.

Bassi niliwabembeleza wale Wadachi nikawaambia, nimekwisha kupata vijana wa kuwachukua hatta Bwembwera ni hodari kwa mwendo; nao wale Wadachi wakaniambia. Shauri nini sasa? Nikawaambia, tafathalini mnipe hawa wazee wawili warudi kwa sababu mwendo hawawezi, bassi wakanipa.

Bassi ndugu yangu ninathani labuda watu walio mikononi mwa Waswahili ao Waswahili wenyewe Wadachi wanawaombea mabaya sana. Lakini sisi Wamasihya tunawaombea wakae salama wa salimini, kwa maana Dini ya Kimasihya itapata kuendelea mbele kama mnavyosikia habari ya Mission ya Umba kama si watu.

Lakini juma a pili ya sabatashara baada ya Pentekote kanisa la Umba likapata watu 40 na zayidi kamwe, hatta watu waliokuwa zamani hawaingii waliingia.

Bassi ndugu furaha gani tuwezayo kuwa nayo kanisa likipata watu kama hawa zayidi ya 40, na yote haya ni kwa nguvu zake Mwenyezi Muungu wetu pamoja na mshindo ufe niliounena wa Wadachi. Lakini tunasikia ya kuwa nao Wadachi waliofanya mambo

MSIMULIZI. 360

hayo ya kuwaonea Wabondei, ati wamefukuzwa pa Bwana wa Tanga kwa maana matendo yamemchukiza. G.K.

HABARI ZA LIKOMA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu Ah! uwe rathi, naona sina mengi ya kukulisha safari hii, wallakini sikia kidogo hayo: - Naliandika katika barua yangu May 2, tumesafirisha bwana Archdn. Maples pamoja na watoto, bassi wakaenda na hiyo stima.

Sasa ya huku nyuma ni haya kidogo: - Pentekote. Tulifurahiwa papa hapa wala hapana kwenda mahali lakini panapo Juma a tatu sisi wengine tulikwenda Mchizumulu pamoja na Mr. Alley tukaenda kucheza humo. Hatta panapo Juma a nne tukarudi zetu hapa Likoma tukakuta imetukia huku nyuma, ndio mtoto mmoja alikuwa mgonjwa, kwanza baadaye akapata kuamka. Hatta siku hiyo ya Juma a tatu alasiri alijaribu kucheza mpila na wenziwe, yeye bassi akasimama mbali hajadiriki, kuupiga huo mpila. Bassi kwa kusukumana mtoto mmoja akamsukuma mwenziwe, na mwenziwe mtoto huyu, akamwangukia na huyu akaaguka chini. (Ee bwana ni ajabu tu) Alipokwisha kuanguka hivyo marra akaonekana ni mtu wa kumia sana, akachukuliwa chuoni, na waana wengine wakaenda kumwambia Bwana Johnson, akapelekewa yule mtoto, naye akampeleka kwa bibi Maclaughlin kwani huyu alikuwa nurse mkubwa kwa upande wake huko Ulaya. Bassi alipomwanguka akaonekana kweli ni mgonjwa sana, akili hana, kunena, haneni, akamlaza na kumpa dawa.

Nalikuambia kama sisi wengine tulienenda Mchizumulu, bassi tulirudi jioni siku ya Juma a nne, ndipo tulipoona mambo hayo. Bassi hivyo akaendelea tu katika ugonjwa

MSIMULIZI. 361

hajui kuamka kitandani, chakula hawezi kula. Hatta Bwana Johnson akaona afathali abatizwe, kwani alikuwa mwaanafunzi, na uwaanafunzi wake alitiwa siku ya Pentekote. Bassi akabatizwa, jina lake Tito Mkanga (kwani sura yake sawa na Tito huyu alioko huko Unguja). Hivyo ndivyo ilivyoendelea hatta panapo May 30 akafariki, siku ya Ijumaa. Tukazika siku hiyohiyo. Hizi ndizo habari za ndugu yetu Tito.

Habari zingine ni zile zile ya kuwa hatari huko ng'ambo ndio simba, naye kweli anafanya uharabu sana. Wenyewe kwa upuuzi na upumbafu wao husema, ni mtu mmoja jina lake Alumbe amefufuka, amejigeuza simba, bassi sasa anawala wenzake. Lakini haya wajua kama ni upuuzi wa huku.

Nalikuambia kama tangu May 2, stima ilituacha ikaenda pande za chini, leo hivi June 19, yafika, barua tele za Unguja za meli mbili; na watoto wale aliotaka kwenda nao bwana Archdn. wamerudi, sababu wajua uthia wa Mreno. Walienda wee hatta walifika mpaka Kugombe, lakini hawakupata vema habari za meli ya Unguja, bassi wakarudi zao Blantyre. Lakini Bwana Maples amepita kwani yee ni abiria wa Ulaya.

Bassi walipokaa hapa Blantyre walipata habari ya kuwa wapo Abiria njiani wanakuja wanatoka pande za Unguja bassi wangojeni kwani kwa leo hivi wamesakama katika mto Shire. Bassi, hawa akina Denys wakaja zao hapa Matope kuwangoja, wakakaa we-ee yapata Juma mbili tatu, bassi pale wasipoona ishara ya kuwa wapo pafupi sana wakashika njia ya kuja huku Likoma illa waje wapashe habari ya kuwa wageni wapo pafupi. Bassi hivi niandikapo Msimulizi huyu hawajafika bado huku juu, illa najua ya kuwa wapo pa Matope hivi panapo leo ao kesho kutwa stima yaenda huko kuwatwaa ndio akina bwana

MSIMULIZI. 362

Frere akina So. Hizi ndizo habari kama abiria wa Unguja wamerudi salama njiani. Tunatumaini kama uthia wa Mreno ukiisha watafika huko pande za Unguja.

Habari zingine zile zile za siku zote, ndio panapo June 21, jioni tuko kanisani wevi wakaingia nyumbani mwa Bwana Johnson wakaiba Koti lake yee bwana na mavazi ya Church ya chakula cha Bwana na mabushuti mawili ya bwana, Ah! ndugu zetu sisi tunathii sana kwa hawa wevi kwani haiwezi kupita Juma mbili tatu wasipokuja.

Habari za ndugu zetu walio kandoni mwa bahari hii naona hawajambo. Na tunafurahi kwani Murphy amepata mtoto mke, bado kubatizwa. Safari hii hapana habari kwa kadri yetu sisi wote hatujambo. Labuda ukitazama mwezi wa June huoni hatta Msimulizi. Ah! ndugu ni mambo ya kupitiwa tu, kuandika naliandika wallakini nalisahau kupeleka. Labda utaona ya kuwa nimeandika napita kwenda chini, wallakini nilipofika pa Msumba pa mzee Mapundi, tukaacha safari ya kurudi huku juu pamoja na baba Johnson na watoto sita wa kutoka hapa pa Msumba.

Naswi tulirudi katika mashua Ouse, na tulipofika Pachia tukakaa kidogo, tukataka watoto waliotaka kuja huko Unguja, waje naswi pamoja na wenzao hawa. Wallakini mmoja wao akawa hawezi na wangine wakawa katika kukataa tu, bassi pasipo kukawia marra tukaenda zetu, njia yetu ya juu. Panapo mwezi wa July tumesumbuka na uthia wetu wa killa siku ndio wevi, marra tatu, bwana, walikuja. Tena panapo mwezi huo huo, mashua Ouse yaenenda pande za chini pa Msumba kuwatazama wenzetu, ikarudi July 11. Nayo ilifika na watoto wale watatu waliokana kwanza, majina yao ndio Kamungo, Kalande na Chikokota, wote ni waanafunzi.

Tena pana habari za huzuni kidogo ndio mwezi huo wa

MSIMULIZI. 363

July mwivi mmoja amekufa, lakini hakufia hapa mjini petu, illa alipigwa mkuki tu akafia kwake.

Panapo siku ya July 24, mwajua ni siku kuu ya Yakobo, bassi sisi wangine, baba Johnson akatuambia twende Mchizumulu (ndio kisiwa cha pili cha upande wa Magrebi akaapo Williams) tumpelekee vitu vile avihitajiavyo. Tena kwenda kushindana mpila wa mateke na watoto wa huku naswi hapa tulitoka kama kumi. Ee bwana, kwa sababu palikuwa hapana upepo tulifika usiku, jioni kabisa.

Bassi panapo Juma amosi tulifanya mashindano yetu waana chuoni peke yao. Panapo jioni tukawa watu wa kurudi, lakini watoto wa Likoma waliingiza matano kwa watoto wa Mchizumulu, na wale wa Mchizumulu waliingiza mawili kwa watoto wa Mlikoma. Panapo siku ya July 25 Ijumaa alasiri kabisa stima ikafika pamoja na wageni wetu, tulifurahi kuwaona salama, watu wanane jumla. Naswi tupo hapa wote salama.

Siku hizi bwana Padre wetu ameona vema kupeleka juko na huko waalimu pande za ng'ambo kwa kufundisha na kazi zingine. Bassi panapo Aug. 6, Bwana Johnson aliniambia niende mahali panaitwa Kungofi pamoja na mwalimu So. Bassi tukaingia katika mashua Charlotte, tukafika, tukakuta mahali aliponunua Bwana Johnson tukawaambia watu wafyeke.

Wallakini wakafyeka kidogo tu marra wakaanza maneno ya kusema, hatuwezi kuongeza mbele, tukashindana nao kwa siku mbili mpaka ilipokuja stima siku ya Juma amosi kututwaa; wala hawakubali wale watu kututengenezea mahali.

Na habari za hapo pa Mapundi (ndio jina la mfumu aliyetukaribisha) njema kwa kadiri yake. Kwani aweza sana kuwatiisha watu wake, nimeingia katika miji mingine

MSIMULIZI. 364

nikatazama, nikaona, wallakini yee Mapundi killa aendapo watu humpigia magoti njiani, killa apitapo na akaapo yee watu ao watoto wasio wa cheo ao na adabu hawakaribii mbele yake, wala kutia ghasia yeyote.

Habari zingine za upuuzi tu. Tulipokwenenda huko Kungofi tulichukua saa yetu, bassi siku moja tumekaa wakaja watu wakubwa na akili zao. Bassi wakasikia saa ile inaenda tik, tik, tik, tak, ke, ke, ke, ke, - mmoja akasema, "Sikieni jamaa ajabu hii! mnaona kitu hiki kinaenda (Kwani saa hiyo ilikuwa na mkono ule wa kuonyesha kaabu) kinazunguka upesi," Wangine wakaanza kusikiliza, mwingine akasema, "Ah! nasikia watu wanafua vyuma humo." Ah, wangine wanagonga, wangine wanakimbia, na vitu vingine vingi huvitaja tu, naswi ni kucheka tu.

Mmoja jina lake Chitoe, akasema, Ah! Mwalimu So, mimi nitakupa kuku mmoja tu, unipe hii saa; Ah-a-a-a, bwana tukazidi kucheka, Looo! saa nzima hununuliwa kwa kuku tu? Ah! ajabu hii, hatta wakiisifuje na kustajabu kwote huko, hutaka kwa kuku tu. Bassi mwalimu So akafungua nyuma ya kule mitamboni ya ndani; mmoja alipoona inafunguliwa akatoka nje, kwa kuogopa, kwani alithani labda mna vitu ao mtu wa kuathibu hatta kufa. Na wangine wale waliosalia walikuwa na hofu kidogo moyoni mwao wallakini walijizuia. Bassi naswi tukawaambia, sasa karibu kufunguka, tafathali hamna buddi kukaa kimya na midomo yenu imefumbwa, bassi wakafumba vinywa vyao. Wallakini marra, walipoona vitu vya ndani vinavyoendaenda, na ule waya unavyomwaga na kurudirudi Ah! bwana hawakuweza kujizuia, marra wakaanza kunena, Na sisi tukazidi kuwaambia, Ah! ah! haifai kufumbua mdomo watu hawa waliomo humu wakipata hewa yenu ao vumbi, marra watakaa kimya wala hawaendi, bassi wakitaka kufumba kinywa, Ah! bwana, hawawezi moyo

MSIMULIZI. 365

hauwapi, kwa kustaajabu sana, naswi tulikufa kwa kucheka, bwana, kwa ginsi wanavyofikiria mambo ya mbali yasiokuwamo humo. Marra mmoja akasema, akauliza, Ah! bwana, hivyo usiku je watu hawa hufanya kazi vile vile wala hawalali nini? Tukamjibu, ndio huenda mchana na usiku haisimami. Akajibu, - ajabu hiyo, hapana tena watu wenyi maarifa kupita Wazungu!

Panapo Aug. 11 stima yalienda pande za Bandawe pamoja na mabibi kumwona Dr Laws, yalirudi siku ya pili yake. Na habari za huko ni njema illa moja, ndio S. S. Domira imesakama mchangani huko kaskazini, yaliingia kwa sababu ya thoruba ya usiku na nakhotha alikuwa amelala pwani.

Naona hizi ndizo habari nilizonazo. Kwa heri. W.E.K.

HABARI ZA MBWENI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu ya kuwa mwezi wa November 6, ilikuwa kusanyiko la Chama cha Mchungaji aliye mwema, tukakusanyika alasiri ikafanyika sala, tena za kumwaga Mwalimu Kathleen na kumwombea mumewe. Bwana akahubiri habari za kufundisha watu katika barra na za wenzetu waliokwisha kuingia katika kazi ile. Tena akambariki Kathleen apate safari njema. Siku hii wakaingizwa watu watatu Faith Kaytimba, Hildi Siyenu, Rebeka Wajionaje.

November 20, tukaenda kushinda wote Kidutani, tulifurahi huko sana kwa kutembea na michezo tulioitenda. R.W.

MSIMULIZI. 366

HABARI ZA KIUNGANI.

October 7, mwalimu Wilfred Madudu amesafiri Bonde kuwatazama jamaa zake. Tena tumefurahi mno kama kanisa letu limeisha kutiwa marmara upande wa mathbahu na kwenyi viti vya waimbaji.

October 21, wamesafiri ndugu zetu waendao pande za Newala kuwatazama jamaa zao, ndio hawa waalimu Sipriani H. Chitenje, na Arthur Kasembe na watoto wawili Yustino Mkandu na Barnaba Mtaula.

October 22, waalimu walitazamiwa akili muda wa siku tatu. Oct. 28, ndio siku kuu ya Simani na Yuda, Mitume na Mash., bassi sisi tulienda Mwera, pamoja na Wazungu sita, tulifurahiwa sana huko. Hatta majira ya alasiri tukarudi zetu hapa.

November 1, ndio siku kuu ya Watakatifu Wote, naswi tulicheza balli alasiri tukaenda kutembea wengine mjini na wengine Mbweni, na wengine wakaenda kucheza mpila.

Tena Nov. 4, tumewasafirisha ndugu zetu wawili kwenda Nyassa, mwalimu Austini T. Mabruki, na mpishi Gilbert Matengwe, nao wamefuatana na Wazungu wetu wanne, wawili akina bwana, na wawili mabibi.

November 7, waalimu Archibald Semanyi, Constantine Mgoma, na watoto wawili Herbert na Alfred, wamesafiri kwenda Bonde kutazama jamaa zao, na mwalimu Constantine Mgoma amekwenda kutembea kitambo tu kwa mwezi mmoja.

Wilfred Zulangeti ameingia katika H. M. S. "Conguest," anafanya kazi ya upishi. Tena Samuel Mathew amefuatana na Dachki kufanya kazi katika mji ulio juu ya Pangani ukifuata mto Ruvu, jina la mji ndio Lewa.

MSIMULIZI. 367

November, George Kambwende amepolekwa kukaa Mkunazini; naye anafundishwa kazi ya mabati.

November 7, Ijumaa, marikebu zote zilipambwa kwa bendera nyingi sana, na mizinga ikapigwa. Sababu yake nini? Kwa sababu Bwana Seyid Ali bin Sultani amekubali kujiweka mwenyewe na milki yake yote chini ya hamaya ya Queen Victoria. Bassi sisi tulipewa siku hiyo siku ya kucheza, tangu assubui hatta jioni, kwani ni jambo kubwa.

Bassi alasiri waalimu wengine tulienda forthani kutazama baraza, kwani chencheni walienda kucheza, walipokwisha askari kucheza mbele yake na kumsalimia Seyid Ali, ndipo ukapigwa ukelele marra tatu Hip! Hip! Hip! Hurrah! ndio mwisho baraza likaisha.

November 28, tumefurahi sana kumwona mwalimu Wilfred Madudu amerudi, kwani alienda Bonde kutazama jamaa zake.

Nov. 26, Ilikuwa siku ya kuimba usiku, Bassi saa 11 unusu watoto wa Mkunazini na waalimu wa Mbweni walikuja hapa, na Wazungu wengi sana walikuja. Bassi saa 12 tulienda kanisani, kiisha tukaenda mezani; tulipotoka tukakaa muda wa nusu saa. Kiisha ikapigwa kengele, tukaingia wote Chuoni; tukaanza kuimba hatta saa nne. Tulipoisha tukashuka tukaingia mezani, Wazungu, wageni na sisi, tukanywa sharbati, na tukala mikate na ndizi. Wengine wote waliosalia nao wakapewa kathalika, kiisha wageni tukaagana nao wakaenda zao; na sisi tukaenda kulala. Mtg.

HABARI ZA MASASI.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu. Ah! mpenzi jambo la huzuni nataka kukwambia baadaye. Bassi tangu ile habari za vita za Wadachi kupiga pwani

MSIMULIZI. 368

mwote mpaka Lindi na Michindani, upande wa pwani za huku, haujaisha uthia wao. Bassi siku hizi kama umesikia kama askari za Wadachi kama 20 walienda kumwamkia na kuangalia kwa Mchemba naye akawatenda visivyo adabu kabisa kwa kuwasumbuasumbua, baadaye askari wale wakarudi Lindi, wakamwarifu mkuu wao habari mbaya za askari za Mchemba, naye mwenyewe kama hakuwaheshimia kabisa.

Wadachi wakakasirika mno kama tusikiavyo, akawaita askari wote wa Kilwa, wa Michindani na Lindi pia. Bassi wakatoka illi kwenda kutembea kwa mzee Nakam, na ndugu yetu Charles Sulemani alikuwamo na watu wangine wa Kondeni pia. Bassi walipofika kwa Liwengwa marra watu wa Mchemba wakatoka wakatupa mshale akapigwa mtu wa Ch. Suilemani. Wakaenda mbele kidogo wamejificha wakapigwa Madachi risasi likampiga. Ch. Sulemani aliyetangulia la kifua akaanguka chini amekufa. Na mtu wa Mchemba akafa mmoja, wakakimbia. Kwanza walitaka kwenda kwa B. Nakam marra wakageuza njia ya kuja Masasi kwanza. Bassi marra ikaja barua kama baada ya siku ao mbili watafika huku, na amri ya kuwa nataka vyakula vya askari wake na masurufu pia ya njiani.

Siku ile tukatoka kwenda kuwaambia watu habari za Wadachi kama wataka vyakula tele wanunue. Edwin Ramathani akaenda upande mwingine nami vile vile, Assubuhi yake tukasikia kama Dachi amewasili humu amefikia kwa Kambona mbali kidogo kadri ya Kiungani na Mbweni. Marra tunaona hawa wanakuja kumwamkia Bwana Smith, mmoja na askari mmoja. Akawaarifu kama amekuja na watu wengi kama askari 300 na wa mizigo 150 na (Officers) Offisa 8, na Sajini 8, na mkuu wao mmoja juu ya wote. Bwana akafuatana naye kambini akarejea jioni. Siku iliyofuata tukaenda nami kuangalia,

MSIMULIZI 369

ndio tukaona wengi askari weusi wa Kimisri na wa Unguja na Wanyamwezi pia, na Wagala pia naye. Watu wakataajabu mno wakiona askari wanavyojipanga kama wanavyopigana vita.

Bassi walikuja Oct. 16, wakaenda Oct. 18, wakaenda Newala kutazama pia. Illakini hatujui kama waenda kwa vita kwa Mchemba ama sivyo. Illa Mchemba anajivuna mno anena kama, Dachhi haji upesi, bassi B. Nakam na Mzee Matola asema atawapiga. Bassi na hapa pia Masasi anapanena kwa mdomo kama killa pahali anapokaa Mzungu nitapapiga pia. Kwani shauri lao moja na Dachhi. Bassi naona kwa ndugu zetu walio karibu na Mchemba maji hayapatikani kabisa.

Hatta njia za kwenda pwani hazipitiki upesi kabisa kwani kwote amepeleka askari wake kuvizia. Lakini twatumaini uthia huu pia utaisha.

HABARI ZA SHAMBA LA MBWENI

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu habari za hapa. Mwezi wa September tulifiwa na watu watatu Temaso na Majaliwa na Yohana Kibwana.

October 2, Mkewe Nicholas Mkwasho amepata mtoto mke; October 8, Alikufa mkewe Adamu, siku ya Juma a tano usiku. October 12, Juma a pili alibatizwa mtoto wa Nicholas Mkwasho akaitwa Caroline Rose, tena ameshuka William S. Mabruki kutoka Tanga, tena mkewe Nyama amepata mtoto mwanamume. November 4, amesafiri Nicholas na mkewe na watoto, na yaya mmoja jina lake Sikujenda. School ya Nicholas Faraji imeingia watoto wawili, Almasi na Deni. N.F.

HABARI ZA NEWALA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya

MSIMULIZI. 870

salamu, nakuarifu habari za hapa Newala.

August 24 ilikuwa furaha kubwa kwa sababu kwanza ilikuwa siku kuu ya Bartolomayo; yalikuwa mambo matatu, la kwanza mtoto mmoja wa Akumikundi jina lake Mattiya Chilanje alikuwa hawezi, la pili Kushukuru kwa mavuno ya mwaka, la tatu Ubatizo wa watoto, lakini wanaojibu wenyewe ndio hawa: William Mpagweje, Bartolomayo Mmeriha, Yusuf Kasembe, Yakobo Jumbe, Edward Lujenje, Yohana Songani, Marko Kasembe, hawa tumefurahiwa kwa sababu jamaa yetu ya Kimasihiya imeongezeka. Wote Wamasihiya wakaja na waanafunzi wakaja pia, nao walimtolea Muungu sadaka ya mavuno yao.

Siku ya pili watoto wakaenda Chitangali, Juma a pili walibatizwa watoto wadogo mume mmoja na wake wawili; mtoto wa Saadi na mkewe Mmasihiya, ndiye Sara, mwanawe jina lake Neema; Mtoto wa Sila na mkewe Mmasihiya, mwanawe Rabeka, mtoto wa Mangwe mkewe Mmasihiya, mwanawe Yuda.

Siku zilipopita tulikwenda kuwinda waliuawa nyama nyingi ndogo, Swala watano na Kiboko mmoja. E.M.

KUFA KWAKE REV. E. VINER.

Naona wengi wenu mmemwona ao mmesikia habari zake Bwana Viner, Kasisi aliyeacha kwao na kutujia sisi watu weusi. Bassi akaenda Magila, kufanya kazi kule, na kwa namna ya matendo yake mema, watu wote na watoto wote wa Magila walimpenda sana. Wallakini kama tujuavyo akapatikana na ugonjwa akaugua sana hatta Daktari akaona ni heri apelekwe Unguja. Lakini asiwe na afya vema, ndipo Daktari akasema afathali arudi kwao Ulaya, akaingizwa ndani ya meli.

Miezi ikipita tukapata habari kama hajambo sana, naye ana shauko mno kabisa kuturudia sisi. Bassi akafunga

MSIMULIZI. 371

safari yake ya kuja Afrika akipitia njia ya kusini pande za Kepi apate kwenda Nyasa. Alipofika Kepi ugonjwa wake ukamrudia vilevile, tena alipopata hajambo ndipo akaendelea mbele hatta Msumbiji; naye akawa mgonjwa vilevile, akauguzwa katika nyumba ya barozi wa Msumbiji. October 18 Juma a pili, akafariki Muungu amependa kwa rehema zake nyingi kumwita astarehe katika Raha yake.

Alipofariki alikuwapo Msumbiji Adimeli pamoja na manovari zake, bassi Wazungu wengi wa merikebuni walishuka kwa maziko yake.

Hii ndio kama sauti ya Muungu kwa Wamasihya wa Afrika, kama waipokee kazi hii ya kuchunga roho za wenzao weusi.

HABARI ZA MAGILA.

Kwa Mtengenezaji wa Msimulizi salamu. Baada ya salamu nakuarifu habari hizi. Katika Sept: 23, Sister Agnes akatoka hapa alasiri akienda zake Ulaya kupumzika katika kazi yake, aliwachukua watoto wake wawili Kate na Nina, akiwarudisha kwao Unguja; twatumaini hatakaa sana Ulaya ataturudia tena.

Katika Sept: 24, ikawa harusi, ya Mmasihya mmoja Isaac Sige. Na katika Sept 25, akatuasilia hapa Bwana Brough na Bwana Bone: pamoja na Carrie Amwitamno. Tukafurahi sana kuwapata, kwa sababu Mr. Brough ndiye fundi wa Sermala mahali pa Bwana Ross aliyechukuliwa Ulaya kwa ugonjwa; na Bwana Bonendiye mwalimu wetu (School-Master) mahali pa Bwana Roberts, Carrie Amwitamno afanya kazi ya kutengeneza Kanisani na kwa Masisters pia. Bwana Roberts kazi yake ni kuangalia School za nje nje tu, baadaye ataenda zake Ulaya.

Katika Sept. 27, akatuasilia hapa mwalimu Hugh Mhina

MSIMULIZI. 372

akitoka Kiungani, aja kukaa afanye kazi yake ya kufundisha.

Oct. 12, akabatizwa mtoto wa Clement Mkabenga, mtu aliye na kazi ya dobi hapa, na jina la mtoto wake James.

Oct. 13, Ikawa harusi tena ya mtu mmoja Ackworth Baruti. Oct. 15, Padre Salfey akatuasilia hapa, pamoja na mwalimu Wilfred Madudu ajaye kutembea kwa mwezi; ni furaha kweli ndugu zetu tujiwe na Kasisi, kazi yetu haitalegea, kwani maskini sisi kwa inchi yetu imepungukiwa sana na Makasisi. Oct. 18, akafa mzee mmoja aitwaye Mdoe, mwanafunzi tu naye, bassi tukaenda usiku, kumfanyia sala fupi fupi tu, kwani alikuwa tayari kubatizwa.

Oct. 20, Tulisafiri kwenda Tanga. Kwanza siku hii tukatoka watoto wote (illa wagonjwa) kwenda Misozwe kwa siku kuu ya Kanisa la Misozwe: nayo ikawa siku ya pili yake ndio Juma a nne. Siku ile ile ya siku kuu tukatoka alasiri Misozwe kuanza safari yetu ya Tanga. Tulikuwa watoto 32 pamoja na watoto wa Mkuzi na mwalimu wao Cyprian Lizani, na wapagazi wanne, na Bwana Bone na Mr. Roberts: bassi jumla yetu tu watu 38 tuliokwenda.

Bassi safari yetu ikawa ya furaha sana, tarumpeta hulia tu njiani mwote; tukafikia mto Zigi kama saa 11, mahali pazuri sana wanapotua watu; tukaona mabanda ya Admeli na wenzake walipopita wakienda zao.

Bassi tukashika njia tukafika mji wa kwanza wa Digo, ndio Hakishihiri, tukalala hapa nje ya mji penyi miti. Juma a tano assubui kabisa tukatoka tushike njia, bassi njiani tuliumia sana na jua, miji yote ya Wadigo hutukimbia hututhania sisi Wadachi wanaposikia tarumpeta yetu: tukakaribia majumba ya Tanga kama saa tano, tukatua, tukapika chakula chetu, tukala, tukapumzika.

Kama saa kenda tukatoka tuingie Tanga kwa Bwana mkubwa, na killa mtu amevalia vizuri.

MSIMULIZI. 373

Bassi tukaingia Tanga, tukapewa nyumba ya kukaa, na tukaheshimiwa na mwenyi nyumba vizuri sana, Mhindi naye. Alhamisi tukakaa kulekule, tukitembea tu. Mji umebadilika vizuri sana, killa jambo kwa amri na yupo mwalimu (Schoolmaster) wa Kidoicha, atafundisha watoto na kufanya Station yake: lakini atakuja hapa Magila aangalie kwanza, ndipo atarudi aanze kazi yake, ni mtu na mkewe. Jumaa alfajiri tukatoka Tanga kuja Magila, lakini tukapitia njia ya Umba safari hii. Tulipopita miji ya Wadigo ya mwisho kama saa nne tukapika na kupumzika kidogo. Tulipoisha tukashika safari yetu, tukafika Umba kama saa kumi, tukala madafu pale; tukapita tukaenda kulala Msaraka. Assubui Bwana Bone na watoto sita wakaenda Magila, na watoto wa Mkuzi pia wakaenda zao. Sisi tukakaa palepale hatta saa nane tukatoka kwenda Magila, tukarudi kwa furaha sana: tukaingia wote salama salimini Magila kama saa kumi na mbili na nussu, wote wazima tukionana tena.

Katika Nov. 11, akaja mwalimu Archie A. Semmanyi na Constantine Mgoma wakitoka Unguja, wamewaacha wenzao Alfred Juma na Herbert Msembeleka kwao Umba, wamekuja kutembea kwa mwezi, tena watarudi. Katika Nov. 12, akafa mtoto wa Clement Mkabenga, yeye niliyemna kwanza, ikawa huzuni kwao kuu kwa mtoto wao mchanga tu. Katika siku hii hii akatuwasilia Aaron Amwitambo akitoka Mkuzi amekombolewa utumwani; ikawa furaha kwa wote waliomjua, na zayidi kwa mkewe.

Katika Nov. 16 ndugu yangu nikaaye naye hapa alishikwa sana na homa, bassi akabatizwa aitwa Geldart Senkoba; naye sasa hajambo. Katika Nov. 24, mwalimu Wilfred Madudu akarudi zake Kitmgani kusoma.

Twataka sana waalimu, weusi, sana tena. Lakini sio

MSIMULIZI. 374

"School master" tu, zayidi Wangoje, kazi huku barra inawangojea, sharti wawahurumie ndugu zao. Tazama, Mwalimu Richard Mhina anafundisha kijiji kiitwacho Potwe, siku hizi na wanamjia watoto 100 na zayidi, naye peke yake. Tena watu wa upande ule wamependa wenyewe wajenge bure School wafundishiwe. Na mwalimu Lewis Bondo anapata watoto kama 50, naye peke yake. Na watu wake wanamjengea School pasipo mali, illa wapate kufundishiwa. Na mahali pengi siku hizi wanataka waalimu, bassi twataka watu kama hawa wapatiwe waalimu, walio Wangoje kuliko "School-master" tu. Lakini nataka kuwaambia jambo moja linalochekesha sana. Mji mmoja Zimbili tumepeleka mwalimu mmoja afundishe, naye alikuwa anapata watoto 90; lakini mkubwa wa mji akamletea Padre Woodward barua hii. "Mpenzi Bwana, salamu, mimi nasema kama wanijaa nami nakujua sana, tena nimekupa mbuzi yangu, wewe hukunipa hatta kitu. Bassi mbona rafiki umenisahau sana, bassi nataka kidogo kama riale tatu unitake rathi kidogo ndipo nitakuwa rathi sana uje hapa Zimbili usomeshe watoto; kama hutaki na mimi sitaki usomeshe watoto."

Katika Nov. 20, Ikawa harusi ya Alfega Mdoe, watoto walimpeleka kwake kwa nyimbo za furaha sana. School ya Masisters inaendelea sana, wengi walio hodari katika waanafunzi wao. Hatta mtoto wao mmoja hodari sana wamemtia asayidie katika kufundisha, aitwa Josephine Mamkuna; na wengine watatu wanamkaribia, bassi Sisters wanafanya kazi sana.

Siku hizi "Day boys" na watoto wa mwalimu Richard Mhina afundishaye Potwe, na watoto wa Kiole, na Zimbili huja wengi sana kwa Juma a pili wake na waume. Bassi waanafunzi na watoto wote waume na wake husalishwa Chuoni na waalimu kwa mafundisho yao mbali: na wazee

MSIMULIZI. 375

na wengine wakubwa wakubwa waume na wake huingia Kanisani. Bassi watoto watokao katika miji wasalishwao chuoni ni wengi sana, hatta pengine huja 320. waume na wake. J.B.M.

JUMA A PILI YA KWANZA YA KUJA.

Leo Bwana Askofu ametufikia salama akitoka Ulaya; ameleta naye Mr. Davies, Kasisi, na Mr. Carnon na Mr. Haines, Mashemasi, na Miss Campbell na Miss Caffin, Mabibi wauguzaji. Bwana Askofu amezunguka kwa Berlin kumtazama mfalme wa Wadoicha. Major von Weisman amerudi naye.

Bwana Askofu atakwenda Magila kwa siku kuu ya Kuzaliwa.

Tena tumefurahi sana sisi leo wa Chama cha Paolo Mtakatifu, kwani Basil Mhada ameingia katika Chama.

Waletaji Habari wasome. Tutajaribu kuwaletea karatasi za kutosha kwa mwaka mzima za kuandikia habari zenu kwa Msimulizi; Lakini msandike pande zote mbili za karatasi. Killa mtu andike awezavyo karasa 2 hatta 4 zenye habari killa safari, akijiliwa na habari kubwa bassi akaongeze karasa ngine. Mtg.